

**UHAKIKI WA MAUDHUI NA FANI KATIKA *UTENZI WA MWANAMANGA*
UTUNZI WAKE FUMO LIYONGO**

HENRY MWALUGHA MWASAFU

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA KUHITIMU KATIKA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA LUGHA
YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA PWANI**

MEI, 2018

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kile ili kutimiza mahitaji ya shahada yoyote ile.



28/09/2018

HENRY MWALUGHA MWASAFU

Tarehe

C50/IB/3163/14

IDHINI

Tunathibitisha kwamba kazi iliyowasilishwa katika tasnifu hii ya shahada ya uzamili ilifanywa na mtahiniwa chini ya usimamizi wetu. Hakuna sehemu ya tasnifu hii ambayo itatolewa kwa namna yoyote ile bila kibali kutoka kwa mwandishi na Chuo Kikuu cha Pwani.

Prof. Rocha Mzungu Chimera

Sahihi.....



Tarehe..... 28/09/2018

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi,

Chuo Kikuu cha Pwani.

Prof. Furaha Chai

Sahihi.....



Tarehe..... 28/09/2018

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi,

Chuo Kikuu cha Pwani.

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu Bw. Paul Maghanga Mwasafu na Bi. Grace Malemba Mwasafu ambao walinihimiza kuendeleza masomo yangu.

SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani kuu kwa Rabana kwa kunipa siha njema na fursa ya kuendeleza masomo yangu. Baraka na neema zake ziliniwezesha kuikamilisha kazi hii licha ya changamoto nyingi. Kazi hii imeweza kukamilika kutokana na ukarimu na hisani za watu wengi ambao ningependa kuwataja baadhi yao. Ushauri na nasaha zao zimefanikisha kukamilisha utafiti huu. Kwanza, nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Rocha Mzungu Chimerah na Prof. Furaha Chai kwa kuniongoza kuanzia mwanzo hadi tamati mwa tasnifu hii. Pili, nawashukuru wahadhiri wangu wa Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi katika Zutafindaki ya Pwani kwa kuniandaa vilivyo ili kuweza kuuendesha utafiti huu: Prof. Yakobo Mutiti, Prof. Beja Karisa (ambaye kwa sasa ni marehemu), Dkt. Nancy Ngowa, Dkt. Catherine Mwangi na wote waliochangia katika utafiti huu wakiwemo Prof. Sheikh Ahmed Nabhany (ambaye kwa sasa ni marehemu), Prof. Kinene wa Mutiso, Mwl. Kevin Bwire, Bw. Bethuel Sanga na Mwl. Anderson Opwaka. Ninawaombea baraka nyingi kwa kila mnachokifanya.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Utafiti huu ulilenga kuchunguza maudhui na vipengee vya fani vilivyodhihirika katika utenzi huo. Utafiti huu vilevile ulilenga kubainisha hisia ambazo mtunzi amezitumia katika utenzi huo kwa kuangazia tamathali mbalimbali za usemi zilizotumiwa kuibua hisia hizo. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya kihemenitiki iliyoasisiwa na Friedrich Schleiermacher, Wilhelm Dilthey na Martin Heidegger. Msingi wa mtazamo wa kihemenitiki ni uchunguzi wa matendo mbalimbali ya binadamu kama usemaji, upendaji na uchukiaji. Nadharia hii inalenga kuchunguza mawasiliano pamoja na ufasiri wa maana za matini mbalimbali kama vile: kazi za kifasihi, vifungu vya Biblia na vya kifalsafa. Utafiti huu ni wa kimaelezo ambapo umehusisha usomaji wa maktabani na vilevile kuzuru nyanjani. Katika usomi wa maktabani, makala, vitabu pamwe na tasnifu mbalimbali za fasihi zilisomwa ili kupata data iliyohusiana na utafiti huu. Utafiti huu kwa kiwango fulani ulihusisha usakuraji na ukusanyaji wa makala faafu kupitia kwa mtandao katika tovuti mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Katika utafiti wa nyanjani, mtafiti alifanya uteuzi wa kimakusudi ili kupata sampuli ya walengwa alionuia kupata data kutoka kwao. *Utenzi wa Mwanamanga* umedhihirisha maudhui ambayo baadhi yanahusiana na wanawake kama vile: urembo, unyumba, sifa, nafasi ya mwanamke katika jamii nakadhalika. *Utenzi wa Mwanamanga* umesheheni vipengee vingi vya fani ambavyo baadhi yavyo ni: tamathali za usemi kama vile: sitiari au mafumbo, taswira, tashbihi, ukiushi katika ushairi na muundo. Mtunzi wa *Utenzi wa Mwanamanga* ametumia hisia kama vile: kuona, kuonja, kunusa, kugusa na kusikia katika kumwelezea mhusika wake kwenye utenzi.

YALIYOMO

Ungamo.....	ii
Idhini.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Ikisiri.....	v
Yaliyomo.....	vi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.1 Kitangulizi.....	1
1.2 Usuli wa mada.....	1
1.3 Swala la utafiti.....	6
1.4 Malengo ya utafiti.....	6
1.5 Maswali ya utafiti.....	7
1.6 Upeo na mipaka.....	7
1.7 Sababu za kuchagua mada.....	8
1.8 Natija ya utafiti.....	9
1.9 Maelezo ya istilahi.....	10

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

2.1 Kitangulizi.....	12
2.2 Mapitio ya maandishi.....	12
2.3 Misingi ya nadharia.....	26
2.4 Mihimili ya nadharia.....	33

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

3.1 Kitangulizi.....	37
3.2 Mpangilio wa utafiti.....	37
3.3 Utaratibu wa utafiti.....	38
3.4 Jumuia na uteuzi wa sampuli	40
3.5 Utaratibu wa ukusanyaji data.....	42
3.6 Vifaa vya utafiti.....	43
3.7 Data itakayokusanywa.....	44
3.8 Mbinu za kukusanya data.....	44
3.9 Uchanganuzi wa data.....	46
4.0 Uaminiki wa utafiti.....	47
4.1 Maadili ya utafiti.....	47
4.2 Vikwazo vya utafiti.....	48

SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.1 Kitangulizi.....	49
4.2 Maudhui.....	49
4.2.1 Mapenzi.....	49
4.2.2. Ushirikiano katika jamii.....	51
4.2.3 Utamaduni.....	52
4.2.4 Dini.....	53
4.2.5 Usanii wa mashairi.....	54
4.2.6 Uzuri wa mwanamke.....	56
4.2.7 Kuheshimiana.....	56
4.2.8 Unyumba.....	58
4.2.9 Ushirikina.....	59

4.2.10 Nafasi ya mwanamke katika jamii.....	60
4.2.11 Ubaharia.....	61
4.2.12 Wasifu wa mwanamke kwa mtazamo wa mwanamume.....	62
4.3 Fani.....	62
4.3.1 Matumizi ya lugha.....	63
4.3.2 Tamathali za usemi.....	64
4.3.2.1 Tashbihi.....	64
4.3.2.2 Takriri.....	65
4.3.2.3 Chuku.....	67
4.3.2.4 Tabaini.....	68
4.3.2.5 Istiari.....	69
4.3.2.6 Matumizi ya taswira.....	70
4.3.2.6.1 Matumizi ya hisia.....	71
4.3.2.7 Matumizi ya lugha fiche.....	76
4.3.2.7.1 Misemo.....	76
4.3.2.7.2 Mafumbo.....	77
4.3.2.8 Tashihisi.....	85
4.3.2.9 Majazi.....	85
4.4 Ukiushi katika ushairi.....	87
4.4.1 Ukiushi wa kitahajia au kihijai.....	87
4.4.2 Matumizi ya hati za lugha nyinginezo.....	88
4.4.3 Matumizi ya lahaja na kikale.....	89
4.5 Muundo.....	94

SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Kitangulizi.....	96
----------------------	----

5.2 Muhtasari wa utafiti.....	96
5.3 Hitimisho.....	98
5.4 Kuhusu malengo ya utafiti.....	98
5.5 Mapendekezo.....	99
MAREJELEO.....	101
VIAMBATISHO.....	107
Kiambatisho cha 1: Mwongozo wa majadiliano.....	107
Kiambatisho cha 2: Tafsiri ya Kiunguja ya <i>Utenzi wa Mwanamanga</i>	110
Kiambatisho cha 3: Msamiati katika <i>Utenzi wa Mwanamanga</i>	114
Kiambatisho cha 4: Muundo wa <i>Utenzi wa Mwanamanga</i>	115
Kiambatisho cha 5: Fomu ya idhini.....	117
Kiambatisho cha 6: Cheti cha nasaha.....	118

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Kitangulizi

Sehemu hii ndiyo iliyotanguliza utafiti huu. Katika sehemu hii mtafiti ameangazia kwa ujumla kuhusu ushairi wa kale katika fasihi ya Kiswahili na kuweka bayana sababu zilizompelekea kufanya utafiti kuhusu *Utenzi wa Mwanamanga*. Mtafiti pia ameweka bayana pengo lililopo na kuonyesha jinsi utafiti huu utakavyoliziba. Changamoto ambazo mtafiti alikabiliana nazo katika uchaguzi wa mada ya utafiti pia zimewekwa bayana.

1.2 Usuli wa mada

Kulingana na Wamitila (2002) suala la historia ya ushairi wa Kiswahili limezishughulisha kalamu za wahakiki wengi. Licha ya kuweco kwa maandishi mengi, swala hili linakuwa na ugumu kuyajibu maswali ya kimsingi kama: Ushairi wa Kiswahili ulianza lini? Ni upi ambao unaweza kuitwa utungo wa kwanza katika fasihi ya Kiswahili? Maswali haya yanatatizwa na kutokuweco kwa tarehe za kihistoria za kutegemewa na uhusiano uliopo kati ya fasihi andishi na simulizi. Baadhi ya tungo ambazo zinaelezwa kama zilitungwa wakati fulani, huenda zilikuwa zikikaririwa au kupokezwa kwa njia ya masimulizi na hatimaye kuishia kuandikwa wakati huo unaosemwa. Mfano ni *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Huu ni utungo uliotungwa na Mohamed Kijumwa katika mwaka wa 1913. Zipo sababu kuamini kuwa kulikuwako na utendi simulizi kumhusu Fumo Liyongo kabla ya wakati huo. Inamkinika utungo huo ulisahuliwa na kubakia kama visehemu vya tungo tu.

Kwa mujibu wa wahakiki wengi kama vile Kezilahabi na Knappert wanaeleza kuwa utungo wa kwanza wa kishairi ni *Hamziya*. Huu ni utungo wa kikasida unaomsifu Mtume Mohamed. Utungo huu unasemekana ulitungwa mwaka wa 1652 au hata kabla

na ni tafsiri ya utungo wa Kiarabu (*Umma Ul Qura*) (*Mama wa Miji*) wa mshairi wa Kisufi kutoka Misri. Isitoshe, wapo wahakiki wengine kama vile Shariff, Mulokozi na Nabhany wanaoshikilia kuwa utungo wa Fumo Liyongo *Sifa za Mwanamanga* au *Utenzi wa Mwanamanga* ndio wa zamani sana na ulitungwa mwaka wa 1517 Mulokozi (1999). Tarehe hizi zinazua maswali kwa kuwa hadi leo hamna ithibati ya kihistoria ya kutegemea kuhusu wakati alioishi Liyongo. Wasomi kama vile Nabhany, Mulokozi, Shariff na wengineo hata hivyo wanaelekea kuamini kuwa Fumo Liyongo ni msingi mkuu wa kuchunguza historia ya ushairi wa Kiswahili. Inahalisi hapa kuzitaja baadhi ya tungo za zamani za fasihi ya Kiswahili. Tungo hizi ni *Utenzi wa Mwanamanga*, *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, *Siri L*, *Asirar*, *Utenzi wa Qiyama*, *Al-Inkishafi*, *Takhmisa ya Liyongo*, *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na *Utenzi wa Mwanakupona*.

Tenzi nyingi za wakati huu zinafanana kidhamira na kifani. Asilimia kubwa zina dhamira ya kidini. Baadhi zinatokana na visa, hurafa na mighani ya Kiarabu au tafsiri za moja kwa moja. Kimtindo, tungo hizi hutumia fomula za fasihi simulizi, fomula sawa za ufunguzi na mwisho wa utungaji, msuko na mgogoro wa msuko unaokaribiana, matumizi ya lugha ya kilahaja (hasa Kiamu na Kipate) kwa mfano *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Al-Inkishafi*.

Shariff (1988), anafafanua dhana ya utendi au utenzi kuwa ni ubeti mmoja wa utungo wa mishororo miwili uliokuwa na vina vitatu: kati na mwisho wa mshororo wa kwanza na kati ya mshororo wa pili. Sauti ya kina cha mwisho huwa sauti yoyote aipendayo mtunzi. Watungaji wengi tokea zamani walipendelea sauti ya mwisho ya kila ubeti iwe moja na vina pia. *Utenzi wa Mwanamanga* ulitungwa naye Fumo Liyongo aliyekuwa shujaa wa Pate. Inakisiwa kuwa utungo huu ulitungwa kabla ya mwaka wa 1202.

Ingawa mtunzi wa utenzi huu alikuwa Fumo Liyongo aliyeweka katika maandishi alikuwa ni Muhammad bin Sheikh mwaka 937H, sawa na 1531 M. Hii ni kwa sababu Fumo Liyongo alikuwa na kipawa maridhawa cha utunzi wa mashairi ila dosari iliyokuwepo ni kwamba katika wakati huo alioishi Liyongo, Waafrika walikuwa bado hawana stadi ya kuandika.

Utenzi ni ushairi mkongwe katika fasihi ya Kiswahili. Utendi au utenzi ni utungo wenye maudhui yanayosimulia kwa kirefu tukio fulani maalum Mbatiah (2001). Utenzi ni shairi refu lenye beti nyingi kuliko shairi la kawaida. Utenzi hugawika katika beti zenye mishororo minne katika kila ubeti. Utenzi huwa na kipande kimoja chenye mizani nane.

Kulingana na Mulokozi (1999) anadai kwamba ushairi andishi wa Kiswahili una historia ndefu. Tangu mwanzo uandishi uliambatana na imani ya dini ya Kiislamu kwani tungo nyingi zilizoandikwa wakati huo zilihusu dini. Mulokozi ameweza kuigawa historia ya ushairi wa Kiswahili kabla ya ukoloni katika vipindi vitatu vya kifasihi kulingana na vipindi vya kihistoria - kisiasa walivyopitia Waswahili. Kipindi cha kwanza ni kile cha ustawi wa miji, utamaduni na tawala za Waswahili, ambacho kilidumu miaka kama 600 (k. 900 - 1500). Kipindi hiki kilimalizwa na uvamizi wa Wareno. Kipindi cha pili ni kile cha utawala wa Wareno na upinzani wa wananchi dhidi yao (k. 1500 - 1730). Kipindi hiki kilimalizwa na maingiliano ya dola ya Oman. Kipindi cha tatu kilianza wakati wa kuasisiwa kwa utawala wa Waarabu wa Omani (kama mwaka 1730) na kumalizika wakati wa maingilio ya ukoloni wa Kiingereza na Kidachi (kama mwaka 1890). Kifasihi, kila kipindi kati ya vipindi hivi vitatu kilikuwa na tungo muhimu zilizokitambulisha. Mulokozi katika kitabu chake anadai kwamba tungo tatu zilizomo humo ni miongoni mwa tungo hizo zinazotambulisha vipindi hivyo

mbalimbali. Kipindi cha kwanza kinatawaliwa na tungo zilizodaiwa kuwa za Liyongo. Kutokana na mapokeo, inaarifiwa kwamba mshairi wa kale zaidi anayefahamika ni Fumo Liyongo, ambaye anasemekana kuwa aliishi maeneo ya Shaka, Kipini na Pate huko pwani ya Kenya katika karne ya 13 ambapo huenda ikawa kabla au hata baadaye. Inadaiwa kwamba hakuna hakika kama kweli Liyongo ndiye mtunzi hasa wa tungo hizo, ila jambo la hakika ni kwamba nyingi ya tungo hizo zilimhusu yeye mwenyewe. Iwapo Liyongo ndiye mtunzi, yaelekea kuwa alitunga kwa ghibu bila kuandika. Tungo zake nyingi zilihifadhiwa katika bongo za watu hadi zilipoandikwa katika miswada karne nyingi baadaye. Utungo “wake” wa kale zaidi uliotiwa katika maandishi unaitwa “*Swifa ya Mwanamanga*” au “*Kumsifu Yanga*” uliosawidiwa kama mwaka wa 1531 Masihiya.

Mulokozi (keshatajwa) anadai kuwa, ingawa Liyongo aliishi kabla ya karne ya 16, lakini tungo zinazomhusu (zilitungwa na watu wengine) ambazo zilizopo ziliandikwa mwanzoni mwa karne ya 19. Tungo hizi ni “*Takhmisa ya Liyongo*” (Sayyid Abdallah bin Ali, kama 1800M) *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulioandikwa na Muhamadi Kijumwa mwaka wa 1913. Hata hivyo, tungo za baadaye zilitokana na fasihi simulizi inayomhusu Liyongo na iliyotungwa zama za Liyongo mwenyewe, hivyo kwa kiasi fulani kimaudhui na kihisia zinaakisi kipindi cha 900 - 1500M. Kama ilivyoainishwa awali wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wameeleza kwa ujumla kuhusu wakati alipoishi Fumo Liyongo na ni lini *Utendi wa Mwanamanga* ulipotungwa. Ni vyema ieleweke kwamba tarehe hizi ni za kukisia na hakuna ithibati mwafaka kuthibitisha swala hili. Habari zinazoelekea kuwa na mashiko kuhusu wakati alioishi Liyongo zimeelezwa na El-Maawy (2011). El-Maawy anaeleza kuwa asili ya Mwanakupona ni Wabatawi, lililokuwa ndilo kabila la asili la Pate. Wabatawi walikuwa ni watawala wa asili, kabla ya kuja Nabhany. Mtawala alijulikana kwa jina la Mwenye Mui, kabla ya

kugeuzwa kuitwa Sultani, tokea siku za nyuma mpaka kuja Nabhany. Yasemekana kuwa Mwenye Mui wa mwisho wa Kibatawi alitwa Isaaka aliyekadiriwa kuwa alitawala Pate baina ya 1170 na 1202 BK. Mwaka wa 1202 ndiyo mwaka uliodaiwa alikuja Suleiman bin Suleiman bin Mudhafar Nabhany kutoka Oman, akaoa binti ya Mwenye Mui wa Kibatawi na akampa uongozi wa kuitawala Pate. Tokea hapo kizazi cha Nabhany kilirithi ufalme wa Pate kuanzia kutoka kwa mama yao mpaka kuja kwa Mwingereza. Mfalme wao wa mwisho alikuwa ni Fumo Bakari, aliyetawala Witu (1890 - 95) na aling'olewa kwa mizinga ya Kiingereza katika vita vya Witu, katika miaka ya 1891 - 1892 BK.

Kutokana na maelezo haya, inadhihirika kuwa Mfalme Daudi Mringwari ambaye alikuwa Mbatawi (Mbantu) alitawala kitambo zaidi kabla ya mfalme wa mwisho wa Kibatawi aliyetwa Isaaka aliyetawala kati ya 1170 na 1202 BK. Fumo Liyongo inadaiwa aliishi katika kipindi alichotawala mfalme wa Kibatawi Daudi Mringwari ambaye waliondokea kupigania uongozi wa Pate (*Utenzi wa Fumo Liyongo*). Katika muktadha huu haingewezekana Liyongo aliishi wakati wa Wareno kisha Wareno washindwe kumtaja katika kazi zao walizoandika kuhusu historia ya pwani ya Afrika Mashariki tukitilia maanani kuwa Liyongo alikuwa shujaa wa kivita. Hii ni ithibati kuwa Liyongo aliishi kabla ya karne ya 12.

Liyongo alitunga utendi huu kwa madhumuni ya kumsifu mkewe na ndilo shairi pekee katika fasihi ya Kiswahili kuwahi kutungwa kwa lengo la kumsifu mwanamke. Fumo Liyongo ametumia lugha yenye mafumbo ili kuweza kuuwasilisha ujumbe wake kikamilifu kwa msomaji. Utenzi huu kwa ujumla unasifu umbo la mkewe Fumo Liyongo aliyekuwa akiitwa Mwanamanga. Fumo ametumia mtindo wa namna ya safari

ambapo anasafiri kuanzia kichwani akiteremka akisifu kila kiungo hadi kufikia kwenye miguu.

1.3 Swala la utafiti

Utafiti huu ulichunguza maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* na vilevile kubainisha hisia ambazo mtunzi amezitumia katika utenzi huu. Utenzi huu umeandikwa kwa kutumia lahaja tatu za lugha ya Kiswahili: Kipate, Kiamu na Kingozi. Utenzi huu vilevile umedhihirisha matumizi ya lugha ya Kiarabu. Msanii wa utenzi huu ametumia sitiari kwa kiwango cha juu katika kuwasilisha ujumbe wake. Sitiari hizi amezijenga kwa kutumia vihimili mbalimbali kama vile: msamiati teule wa ubaharia na wa porini kwa kuzingatia mtindo wa safari. Kutokana na matumizi ya lahaja, lugha ya Kiarabu pamoja na mafumbo, utenzi huu unakuwa changamano na usiofasilika kwa urahisi.

Kulingana na ujuzi wa mtafiti ni kwamba, hajakumbana na utafiti wowote wa kitaaluma ambao umeshughulikia maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa mtazamo wa kihemenitiki. Ni kutokana na hali hii, mtafiti aliweza kupata mshawasha na msukumo wa kutaka kuufanyia utenzi huu utafiti wa kitaaluma ili kuliziba pengo hili na kuutia utenzi huu katika usomi zaidi wa fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu ulilenga kuweka wazi maudhui na fani katika utenzi huu na vilevile kuchunguza hisia ambazo msanii amezitumia kwa makusudi katika kumwsawiri mhusika wake katika utenzi huu.

1.4 Malengo ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

- i. Kufafanua maudhui katika *Utenzi wa Mwanamanga*.
- ii. Kuchanganua vipengele vya fani vinavyodhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

- iii. Kubainisha hisia ambazo mtunzi amezitumia katika kumsawiri mhusika wake kwenye *Utenzi wa Mwanamanga*.

1.5 Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- i. Ni maudhui yapi yanayojitokeza katika *Utenzi wa Mwanamanga*?
- ii. Ni vipengele gani vya fani vinavyodhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga*?
- iii. Ni hisia gani zilizotumiwa na msanii katika kumsawiri mhusika wake kwenye *Utenzi wa Mwanamanga*?

1.6 Upeo na mipaka

Utafiti huu ulijikita katika uhakiki wa madhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Maudhui yaliyodhihirika katika utenzi huu yalichanganuliwa na vilevile yale yaliyohusiana na wanawake kuwekwa wazi. Vipengele vya fani vilivyodhihirika katika utenzi huu pia vilichanganuliwa na kuwekwa bayana. Kadhalika utafiti huu ulichunguza na kubainisha hisia ambazo mtunzi amezitumia kwa makusudi kumsawiri mhusika wake katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kihemenitiki na haukujishughulisha na maswala kama vile: historia ya mtunzi wa *Utenzi wa Mwanamanga*, kipindi ama tarehe aliyoshi mtunzi wa *Utenzi wa Mwanamanga*, tarehe ya kuandikwa kwa *Utenzi wa Mwanamanga* na historia ya ushairi katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu tarehe hizi zina utata na hazina ithibati tosha za kitaaluma na zile zilizotolewa na baadhi ya wahakiki na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili ni za kukisia tu na hazina mashiko yoyote.

1.7 Sababu za kuchagua mada

Utenzi wa Mwanamanga una sifa za kipekee ukilinganishwa na tenzi zingine za fasihi ya Kiswahili. Wamitila (2002) anadai kuwa wapo wahakiki wengine wanaosema kuwa utungo wa Fumo Liyongo, *Sifa za Mwanamanga/Utenzi wa Mwanamanga*, ndio wa zamani sana na ulitungwa mwaka wa 1517. Hata hivyo tarehe hizi zinazua maswali kwa kuwa mpaka leo hamna ithibati ya kihistoria ya kutegemewa kuhusu wakati hasa alioishi Liyongo. Baadhi ya wasomi wanaelekea kuamini kuwa Fumo Liyongo ni msingi mkuu wa kuichunguza historia ya ushairi wa Kiswahili. Shariff (1988:189) anaeleza kuwa, kuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa mtungaji wa awali wa Kiswahili ambaye tungo zake zipo ni Fumo Liyongo wa Bauri. Pili hakuna ushahidi wowote wa tungo za ‘Kibantu’ za zamani kushinda za Fumo Liyongo. *Utenzi wa Mwanamanga* una sifa za kipekee ukilinganishwa na baadhi ya tenzi za kale kama vile: *Utenzi wa Fumo Liyongo, Kasida ya Hamziya, Utenzi wa Al-Inkishafi, Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* miongoni mwa nyinginezo.

Sifa hizi za upekee wa *Utenzi wa Mwanamanga* ni kama zifuatazo:

- a) Tenzi nyingi za Kiswahili huwa na fomula sawa za kuanzia tenzi hizo. Watunzi wa tenzi hizo walianza kwa kumshukuru, kumsifu na kumwomba Maulana awape uwezo wa kukamilisha kuandika tungo zao. Waliamini kwamba, Rabana ndiye aliyekuwa msanii mkuu na wao ni vikaragosi tu vyake vya kupitisha ujumbe wake. Hali hii haipo katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwani mtunzi haanzi kwa kulitaja jina la Mola wala kumsifu au kuomba dua bali anaanza kazi yake moja kwa moja. Hali hii inadokeza kuwa huenda ikawa labda wakati utenzi huu ulipokuwa ukitungwa mtindo huu wa kumsifu, kumshukuru na kumwomba Maulana haukuwepo. Jambo hili linaweza pia kudhihirisha uwezekano wa utenzi huu ukawa ndio mkongwe zaidi na ndiposa tofauti hii inajitokeza.

Hali hii vilevile inadokeza kuwa mtunzi wake yaani, Fumo Liyongo huenda hakuwa mfuasi sana wa dini ya Kiislamu na ndiyo maana hakuona haja ya kuomba dua katika utenzi wake.

b) Tungo nyingi za wakati huu zilifanana kidhamira na kifani. Asilimia kubwa zina dhamira ya kidini. Kimtindo, zinafanana kwa kutumia fomula za fasihi simulizi, kama vile ufunguzi na mwisho wa utungaji. Katika kuutathmini *Utenzi wa Mwanamanga* ni kwamba huenda ulitungwa kale mno kabla ya kuwekwa kwa sheria kama vile kuanza kwa dua na kushuhulikia maudhui ya dini katika uwanja wa mashairi. Hili linadhihirika kwa kuwa maudhui ya dini hayajitokezi mno katika utenzi huu.

c) Upekee mwingine wa *Utenzi wa Mwanamanga* ni kwamba ndio utenzi pekee katika historia ya fasihi ya Kiswahili kuwahi kutungwa kwa lengo la kumsifu mwanamke.

d) Lugha iliyotumika katika kuuandika utenzi huu ni ya kale mno. Utenzi huu, mtu anapoanza kuusoma si rahisi kuelewa. Sababu ni kwamba, mtunzi ametumia lahaja tatu za Kiswahili na vilevile lugha ya Kiarabu. Mtunzi pia ametumia mbinu ya sitiari kwa kiwango kikubwa jambo linaloufanya utenzi huu kutoeleweka kwa urahisi. Hamu ya kutaka kuelewa kindakindaki utenzi huu ndiyo iliyomfanya mtafiti kuamua kuutafitia.

1.8 Natija ya utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatachangia sana katika kukuza zaidi, kuiongezea hadhi, kuirutubisha na kuinawirisha zaidi fasihi ya Kiswahili hususan katika sehemu ya tenzi za kale. Utafiti huu utawawezesha wanajamii na wanaakademia mbalimbali kuweza

kuuelewa *Utenzi wa Mwanamanga* ambao ni moja wapo ya tenzi za kale katika fasihi ya Kiswahili ulioandikwa kwa lahaja tatu za Kiswahili ambazo ni: Kipate, Kiamu, Kingozi na kwa kiduchu lugha ya Kiarabu. Utafiti huu umedondoa msamiati wa lahaja hizi na kutoa fasili kulingana na jinsi ulivyotumika katika utenzi kulingana na kipindi cha kihistoria ulipoandikwa utenzi huu. Utenzi huu kwa hivi sasa haueleweki kwa urahisi kwa waja wanaokumbana nao wakiwa na hamu ya kuusoma. Matokeo ya utafiti huu pia yatakuwa nyongeza kubwa kwa maandishi yanayozidi kuongezeka kila wakati kuhusu tenzi za kale katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu utauweka wazi zaidi *Utenzi wa Mwanamanga* ambao haujulikani sana kwa sababu haujafanyiwa tafiti nyingi za kitaaluma. Jambo hili litaibua fursa nzuri kwa watafiti wengine ili kuweza kuutafitia zaidi. Utafiti huu utauweka wazi *Utenzi wa Mwanamanga* na kuutia katika usomi wa fasihi ya Kiswahili hivyo kuirutubisha zaidi fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu kwa ujumla utaliziba pengo lililopo la kutohakikiwa kitaaluma kwa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa mtazamo wa kihemenitiki.

1.9 Maelezo ya istilahi

AH – Baada ya Hijrya. Mfumo wa Kiislamu wa kuhesabu miaka kama vile 600AH inamaanisha mwaka 1200 BK.

Bainisha – Tofautisha, dhihirisha.

k – kuanzia.

BK – Baada ya kifo cha Kristo.

Bulbul – Iliyo wazi.

Fani – Vipengee vinavyodhihirisha ufundi wa kisanaa katika shairi.

Jazanda/sitiari – Mbinu ya lugha inayohusisha matumizi ya ishara zilizo na maana fiche.

Maudhui – Maswala yote yanayoshughulikiwa na msanii katika kazi yake ya fasihi.

M Masihiya – (baaada ya kifo cha Kristo).

Mvuli – Mvulana.

Natija – Umuhimu.

Ninga – Ndege mkubwa mwenye kupendeza wa jamii ya njiwa mwenye rangi ya kijani na miguu myekundu anayeishi kwenye vilele vya miti hasa msituni na hupenda kula matunda.

Wabatawi – Wenyeji Wabantu asilia wa Pate.

Yanga – Mwanamke mzuri.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

2.1 Kitangulizi

Katika sehemu hii maandishi katika tahakiki, tasnifu na majarida mbalimbali yanayoshughulikia maudhui na fani katika tenzi mbalimbali yameangaziwa. Aidha, tahakiki na kazi za watafiti mbalimbali zinazohusiana kwa namna moja au nyingine na utafiti huu zimeangaziwa, kuchanganuliwa na kuwekwa bayana. Vilevile misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu imefafanuliwa ili kutoa mwongozo faafu uliotumiwa kuumulika utenzi huu na kuongoza utafiti huu.

2.2 Mapitio ya maandishi

Kulingana na ujuzi wa mtafiti ni kwamba hajakumbana na utafiti wowote uliohakiki maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa mtazamo wa kihemenitiki. Hata hivyo, kuna wahakiki ambao wameshughulikia swala la maudhui na fani katika tenzi na mashairi mengine na vilevile kazi zingine za fasihi andishi ya Kiswahili.

Arege (2014) anafafanua dhana ya maudhui kama, jumla ya ujumbe na mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika shairi fulani. Anaeleza kuwa, maudhui ni mambo yanayotajwa katika shairi na yanaweza kujumuisha mawazo zaidi ya moja kwa hivyo, maudhui husaidia katika kujenga dhamira ya shairi husika. Naye, Mbatiah (2001) anafafanua dhana ya maudhui kama jumla ya mawazo, fikra, dhamira na hisia vinavyowasilishwa na kazi ya kifasihi. Kwa upande mmoja maudhui yanajibu swali la nini kazi ya kifasihi inazungumzia na kwa upande mwingine fani inajibu swali la vipi maudhui yanavyowasilishwa. Kimsingi, Mbatiah anadai kuwa vipengee hivyo viwili havitenganishiki ingawa wahakiki huvitenganisha kukidhi mahitaji ya kimaelezi. Maudhui na fani huwa na sura mbili za sarafu moja.

Wamitila (2003) anafafanua dhana ya maudhui kama neno linalotumiwa kujumlisha yaliyomo au jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi yoyote. Wamitila anaeleza kuwa katika uchambuzi wa maudhui, msomaji anapaswa kuangalia dhamira, ujumbe na falsafa ya mshairi. Naye, Msokile (1993) anaeleza dhana ya maudhui kuwa ni jumla ya mambo yanayoelezwa ama kujitokeza katika kazi ya fasihi. Maudhui ya kazi ya fasihi hujumuisha dhamira, mtazamo ama msimamo, ujumbe, maadili na falsafa.

Kulingana na ujuzi wa mtafiti ni kwamba, maudhui huwa ni maswala yote yanayojitokeza au kuangaziwa katika kazi fulani ya fasihi. Maudhui hubeba dhamira, msimamo au mtazamo pamoja na falsafa ya mwandishi.

Mbatiah (2001) anafafanua dhana ya fani akidai kuwa dhana hii ina maana mbili: Kwanza ni jumla ya vipengee vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Pili, ni kategoria ya fasihi, yaani utanzu kama ushairi, drama na riwaya. Msokile (1993) anafafanua dhana ya fani kama, jumla ya vipengele vya kisanaa katika kazi ya fasihi. Anaeleza kuwa ni vipengele vinavyojenga umbo la kazi ya sanaa. Mara nyingi vipengele vya fani ni pamoja na muundo, mtindo, mandhari (mazingira), wahusika na lugha. Si lazima vipengele hivyo vya kisanaa kujitokeza kwa uzito uleule katika kila kazi ya kifasihi.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuiwasilisha dhamira na maudhui yake. Mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kuitumia lugha. Lugha hiyo huwa na sifa fulani kwa mfano, ina vikolezo au vitia ladha fulani na imesheheni au kujaza mbinu za kila aina. Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kuwa haiwezekani kwa mwandishi kuiwasilisha

dhamira yake au kuyapitisha maudhui yake bila ya kutegemea fani. Ikiwa mwandishi atataka kuwasiliana na hadhira yake vyema, kuishawishi na kuiathiri ipasavyo lazima aiteue lugha yake vyema au ahakikishe kuwa lugha yake ina uwezo wa kuuwasilisha ujumbe huo. Uhusiano wa fani na maudhui ni muhimu sana na ni wa kutegemeana. Uchunguzi wa fani katika kazi yoyote ile ya fasihi unaviangalia vipengele kadha ambavyo ni: matumizi ya lugha, muundo, mtindo, wahusika na mandhari.

Kwa mujibu wa mtafiti, fani ni jinsi msanii anavyoifinyanga kazi yake ili kueleza hisia na mawazo yake kwa njia ya ufasaha. Ufinyanzi wa kazi ya fasihi ni ule mchakato wa kuipanga kazi kwa kuteua msamiati bora na tamathali za usemi faafu ili kuweza kutoa maelezo kikamilifu na kwa ufundi na kuifanya kazi husika kuwa na lugha inayodhihirisha mvuto na mnato mkubwa wa kisanaa. Katika fasihi fani ni jumlisho la vipengee vyote vya fasihi ambavyo msanii anavitumia katika juhudi za kueleza hisia au maoni yake ili kubainisha taratibu za maisha ya binadamu kwa njia ya ubunifu zaidi.

Kulingana na Mulokozi (1999) amezishugulikia tenzi tatu ambazo ni: *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Al-Inkishafi* na *Utenzi wa Mwanakupona*. Mulokozi ameshughulikia maudhui na fani katika tenzi hizi. Aidha, Mulokozi amezungumzia kumhusu kila mtunzi wa tenzi hizi na katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ameongezea kwa kumzungumzia Fumo Liyongo ambaye ni mhusika mkuu katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na historia fupi ya ushairi wa Kiswahili. Mtaalamu huyu anadai kwamba ushairi wa Kiswahili una historia ndefu mno. Lugha ya Kiswahili ilianza kuandikwa kwa kutumia hati ya Kiarabu katika karne ya 10 au kabla. Tangu hapo uandishi uliambatana na imani ya dini ya Kiislamu na tungo nyingi ambazo ziliandikwa wakati huo zilihusu dini. Anaelezea kuwa Fumo Liyongo ni mhusika muhimu katika ushairi wa Kiswahili ambaye hawezi kukwepeka wakati mtu anapoishughulikia historia ya

ushairi wa Kiswahili. Liyongo aliishi kabla ya karne ya 16, tungo zinazomhusu zilitungwa na watu wengine na kuandikwa mwanzoni mwa karne ya 19.

Shariff (1988) anadai kuwa makundi mbalimbali ya wenyeji wa bara na ya waarabu kwa mfano, yalihamia pwani katika karne mbalimbali. Anayaangazia mapisi ya Pate na kugunduwa kuwa ukoo wa Nabhany waliokuja na Suleiman bin Suleiman bin Muzaffar walihamia Pate kutoka Omani mnamo 1204 B.K, yaani miaka zaidi ya mia saba iliyopita. Na hao Wanabhany waliwakuta watu wa ukoo wa Ai-Batawy (ambao pia asili yao imetoka Bara Arabu) na ufalme wao hapo Pate. Pia inasemekana kuwa kabla ya ufalme wa Kibatawy kulikuwa na ufalme wa Mwanamsuri na kabla ya hapo palikuwa na Fumo Liyongo al-Baury katika enzi ya Daudi Mringwari.

Maandishi mengine ya zamani yanayohusishwa na Liyongo ni utungo wa “*Swifa ya Mwanamanga*” ambao pia ulijulikana kwa jina “*Kumsifu Yanga*” ambao unadaiwa kuwa ulitungwa na Liyongo kumsifia mkewe. Utungo huu ulihifadhiwa kimapokeo hadi ulipoandikwa katika mswada na Muhammad bin Sheikh mwaka 937H, sawa na 1531 M. Utungo huo unamsifu mwanamke aitwaye Mwanamanga kuanzia kichwani hadi miguuni, na ni miongoni mwa tungo za kale zaidi za Kiswahili zinazofahamika. Kulingana na Mulokozi (keshatajwa) ni kwamba, habari zilizopo kumhusu Liyongo zinaonyesha kuwa mtu huyu aliishi pwani ya kaskazini mwa Kenya kwenye maeneo ya Pate na Ozi katika karne ya 14 au kabla. Kwa kuzingatia mapokezi ya jamii ni kwamba, mama yake aliitwa Samoa Mwana: ingawa katika nyimbo nyingi mama yake alijulikana kwa jina la Mbwasho. Liyongo alikuwa kiongozi katika jamii yake, japo hakuna hakika kama alikuwa mfalme. Alikuwa shujaa, manju wa ngoma na malenga na mwindaji hodari. Kwa upande wa dini, hakuna ushahidi kuwa alikuwa Mwislamu: kama aliishi kabla ya karne ya 8, yumkini alikuwa mfuasi wa dini ya jadi ya Waswahili

(nyimbo zake nyingi, mathalan zile za kusifu pombe, zinatuelekeza huko); kama aliishi karne ya 13 au 14, pengine alikuwa Mwislamu, kwani kipindi hicho watu wengi wa pwani walikuwa wamekwisha kusilimishwa. Liyongo alikuwa akizunguka kuwinda na kufanya biashara sehemu za bara karibu na Pate, aliweka makazi yake Ozi, na alifia na kuzikwa Kipini, mahali paitwapo Ungwana na Mashaha. Katika kuangazia maudhui, Mulokozi amefafanua maudhui ya tenzi tatu. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* anadai kwamba maudhui katika utenzi huu ni yale yale tunayokuta katika tenzi nyingi za Kiafrika na hata za kilimwengu: kutetea nchi, taifa au jamii: kugombania utawala, wivu, usaliti, ushujaa, na siri ya ushujaa. Liyongo ni muhanga wa tamaa ya utawala ya Sultani na tamaa ya mali na cheo ya mtoto wake. Ni mtu mwema anayeponzwa na wema na uwezo wake. Dhamira ya usaliti inasawiriwa vizuri – tunamwona mwana wa Liyongo akirubuniwa hadi kumsaliti baba yake kwa tamaa ya mali na hadhi. Mwisho imeelezwa kuwa usaliti haulipi; yule mtoto badala ya kutunzwa anafukuzwa, kufedheheshwa na hatimaye kufa kwa majonzi. Utenzi huu vilevile unasawiri mgongano wa mifumo ya kijamii; mfumo wa maisha ya shamba na pori, na ule wa mjini. Mgongano huu unajitokeza vizuri zaidi katika nyimbo za Liyongo, kwa mfano “wimbo wa nyika.” Wimbo huu unatupa picha ya maisha ya pori ambayo yana uhuru, furaha na mshikamano, na ni tofauti na ya mjini kwa kila hali kwa upande wa chakula, mtindo wa maisha, tabia na elimu. Katika tenzi na nyimbo za Liyongo, pori ni mahali panapompokea na kumkirimu Liyongo; ni mahala penye upendo na udugu, licha ya ufukara ulioko. Mjini ni mahali penye utajiri, starehe na ulafi unaoambatana na ubinafsi, ukatili na maonevu.

Kwa upande wa fani katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* Mulokozi ameangazia yafuatayo: Anadai kwamba utungo huu umetungwa katika bahari ya utenzi ambayo huwa na mishororo miwili kila ubeti yenye jumla ya mizani 32. Katika maandishi ya kizungu,

mishororo hiyo kwa kawaida huchapwa katika vipande vinne vya mizani nane nane. Lugha iliyotumika ni Kiamu, na kwa jumla ni nyepesi, haina utata. Ni lugha ya masimulizi isiyotumia sana picha na taswira. Mpangilio wa vina na mizani ni ule wa kawaida wa mizani 8 kila kipande, vina vya mwisho vinavyobadilika kila ubeti, na kina kimoja cha bahari cha [- ya] kisichobadilika mwishoni mwa kila ubeti.

Msuko wa matukio katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* hauna utata. Liyongo ni shujaa aliyependwa na watu kwa kuwa anawapigania na kuwasaidia. Mfalme anamwonea wivu na kuogopa kwa kuwa anaweza kumpoka ufalme. Anafanya njama ya kumuua ingawa njama hizo hazifanikiwi. Inabidi mfalme atafute ujanja mwingine na kufanikisha azima yake. Anaamua kumtumia mwanawe Liyongo ili amsaliti baba yake kwa matarajio ya kuozwa binti mfalme na kupewa uwaziri. Njia hiyo inafanikiwa; Liyongo anauawa. Mwanawe aliyesababisha kifo chake vilevile anaadhibiwa kwa matendo yake na kuaga dunia. Fumo Liyongo ni hadithi yenye msuko na mshikamano mzuri na imekamilika, japo ni fupi.

Mulokozi (keshatajwa) pia ameangazia maudhui na fani katika *Utenzi wa Al-Inkishafi* wake Sayyid Abadallah bin Ali bin Nassir. Anadai kuwa msingi wa maudhui katika utenzi huu ni Kurani Tukufu; mwandishi anachukua mafundisho ya Kurani kuhusu maisha na mwenendo bora wa muumini na kuyafafanua kwa vielelezo vinavyotokana na historia na mazingira ya Pate na Afrika Mashariki kwa jumla. Anaelekea kuamini kwamba kweli anayoisema inathibitishwa na uzoefu wa watu wa Pate na kwingineko katika upwa wa Afrika Mashariki.

Dhamira kuu ya *Al-Inkishafi* ni kufafanua maana ya maisha na maana anayoitoa Sayyid ni ile ya kidini – ya Kiislamu. Anayaona maisha kama sura mbili – ya unyofu na

upotovu. Sura ya upotovu ni sura ya maisha ambayo yanamghibu na kumhadaa mwenye kuyaishi hata anaikumbatia dunia moja kwa moja na kumsahau Muumba wake. Kwa mtazamo wa mtunzi, mtu wa namna hiyo anadanganywa na malimwengu, anakubali kutenda maovu, na hivyo anafurahia raha na fahari ya muda mfupi wa maisha ya kimwili na kuipoteza raha ya milele ya maisha ya ahera. Kwa upande wa mnyofu, maisha yake yanaonyeshwa kuwa ni ya kusalimu amri mbele za Mungu, ya kunyenyekea, kusali, kujinyima na kutenda mema, kwa matarajio ya kupata thawabu bora zaidi na raha ya kudumu baada ya kifo (cha mwili). Picha ya magofu ya Pate na mateso ya maiti kaburini anayotusawiria mtunzi imekusudiwa kutuambia kuwa maisha haya hayana maana bila kumshirikisha Mungu; lengo la maisha si kuishi bali ni kujiandaa kwa maisha ya baadaye ambayo ni bora na ni ya milele. Maisha haya ni mafupi na ni ya kupita kwa haraka, ilhali utukufu wa Mungu ni wa milele. Kwa upande wa fani Mulokozi amejaribu kuuchambua utenzi huu wa *Al-inkishafi* kama ifuatavyo:

Mulokozi anadai kwamba utenzi huu ulipata nguvu yake kutokana na lugha tukufu inayotumika na taswira anazotumia mtunzi kutupa picha halisi na isiyosahaulika ya kile anachokieleza. Mfano: Mtunzi anaanza kwa kutuahidi kututungia koja au kidani cha lulu.

Katika ubeti wa kwanza tunapata picha ya vito vya thamani vilivyotungwa pamoja ili kumvutia na kumpamba mhusika. Hili koja ambalo mtu yeyote angelitamani, na msomaji anashawishika kuendelea kusoma ili kulifaidi koja hilo. Mulokozi vilevile ameshughulikia maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Anadai kwamba utenzi huu umezua mjadala mkali miongoni mwa wanataaluma ya Kiswahili. Mjadala huo hasa umejikita katika itikadi yake Mwanakupona kijinsia, hususan namna Mwanakupona anavyotazama uhusiano wa mke na mume katika ndoa.

Mulokozi anadai kwamba mjadala wa wataalamu hao unadhihirisha utata wa maudhui ya Mwanakupona, hasa katika mazingira ya leo. Ni bora kukumbuka kwamba sehemu kubwa ya maudhui hayo si mawazo ya Mwanakupona binafsi, bali ni mawazo yanayotokana na vyanzo vikuu vinne: kwanza, yanatokana na mafundisho ya dini ya Kiislamu kama yanavyoelezwa katika Kurani na hadithi na vitabu vingine. Pili, yanatokana na mila, desturi na imani za jadi za Waswahili na baadhi ya Waafrika wa maeneo ya pwani. Tatu, baadhi yake yanatokana na mila na desturi za waarabu zinazofuatwa na baadhi ya wenyeji wa pwani waliosilimu. Nne, maudhui yanatokana na imani na desturi, mitazamo na uzoefu wa tabaka la pwani.

Kwa upande wa fani Mulokozi anadai kwamba *Utenzi wa Mwanakupona* si utenzi uliojipambanua sana kisanaa hata hivyo mtunzi ameumudu vizuri ushairi wa bahari ya utenzi (mizani 8 kila kipande). Kwa upande wa lugha, Mwanakupona ametumia lahaja ya Kiamu na anaimudu vizuri. Lugha yake ni nyepesi kiasi, hana mbwembwe wala haonyeshi maksudi ubingwa wake kwa kutumia maneno mazito na msamiati mgumu kama wafanyavyo baadhi ya washairi. Mwanakupona hatumii sana lugha ya picha, hususan tashbihi, sitiari na taswira ila katika sehemu chache anapoitumia lugha ya aina hiyo anafanikiwa sana. Mifano: picha ya hirizi, koja na kidani/kifungo katika ubeti 8 hadi wa 10 imewekwa vizuri ili kutupa dhana ya utenzi kama kinga (hirizi) ya kumlinda anayetungiwa dhidi ya matatizo ya unyumba.

Swaleh (1992) ameshughulikia maudhui katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Katika uhakiki wake, alisema kuwa maudhui ya dini yamejikita katika mafundisho ya Kiislamu yaliyomtunukia mwanamke nafasi anayostahiki katika jamii yake. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa hadhi anayopewa mwanamke katika jamii yake inamstahiki. Mtafiti huyu anadai kuwa majukumu apewayo mwanamke kwa jamii hiyo ndiyo

yanayochangia kumnyanyasa. Kazi ya mhakiki huyu imemfaa mtafiti katika kuhakiki maudhui ya urembo, nafasi ya mwanamke, unyumba na utamaduni katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

Mberia (1989) alihakiki *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa kutathmini sifa za Fumo Liyongo, kama shujaa wa masimulizi. Katika kazi yake, amempa mtafiti mwelekeo kuhusu kuhakiki maudhui katika utenzi kwa ujumla.

Harries (1962) alijizatiti na kufanya uchunguzi wa tungo za Uswahilini hususan kifani ukiwemo *Utenzi wa Al-Inkishafi* na kufikia mkataa kuwa uketo wake unawiana kabisa na tungo za kishairi bara Uropa zilizokuwa zikichukuliwa kama upeo wa umbuji wa sanaa. Baadhi ya maudhui aliyoyaangazia ni dini, umaskini, utajiri na maangamizi ya binadamu. Kazi hii imetoa mwelekeo wa kijumla wa kuhakiki maudhui katika tenzi.

Mlamali (1980) alichapisha kitabu kuhusu *Al-Inkishafi* kihistoria na hususan tafsiri yake ambayo imeondokea kutoa maelezo mazuri katika kuweza kuelewa ujumbe wa Sayyid Abdallah bin Ali bin Nassir katika utenzi wake. Utafiti huu umenufaika kutokana na fasiri hii katika kuchunguza matumizi ya lugha na tafsiri za msamiati wa lahaja ya Kiamu ambayo pia imetumika katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

Mutiso (1985) ameshughulikia swala hili la maudhui, ameangazia maudhui ya hurafa na uyakiniifu katika *Utenzi wa Hamziya*. Katika kazi yake hii pia ameshughulikia sifa apewazo Mtume Mohamed (S.A.W) na zile za mashujaa wengine duniani. Kazi yake imemfaa mtafiti katika kupata mwelekeo wa uhakiki wa maudhui katika tenzi. Naye, Mungai (2005) ameshughulikia fani katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* ambapo amelinganisha *Utenzi wa Nguvumali* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa kifani*. Kazi

yake hii imemsaidia mtafiti katika kuhakiki baadhi ya maudhui katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

Kwa mujibu wa Gerard (1981) *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* ulitiwa katika maandishi miaka ya 1950. Awali, utenzi huu ulikuwa katika hali ya masimulizi. Utenzi huu unasimulia kisa cha ajabu katika eneo la Kilwa kuhusiana na jinsi mauaji ya mwanamke mmoja yalivyosababishwa na wachawi, ambao baadaye walitambuliwa na mganga maarufu ajulikanaye kama Nguvumali. Utenzi huu ni hazina ya utamaduni wa jamii ya bara ambayo japo ilikuwa imeathiriwa na utamaduni wa Uislamu haikuwa imeachana na imani za uchawi na ushirikina. Maudhui mengine ambayo yanapatikana katika utenzi huu ni kama vile ya kejeli kwa maongozi ya serikali yasiyofaa, usaliti, umuhimu wa ushirikiano na taasubi za kiume.

Mukuthuria (2008) alihakiki maudhui na fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa katika utenzi huu maudhui ya uchawi yanajitokeza kwani kuna wachawi wanne. Bwana Shambi bin Dima ambaye ni kinara wa wachawi, Binti Jizi aliyekuwa kiongozi wa wachawi, Binti Ramadhani, na Binti Hanifu ambaye anaagizwa na wachawi wenzake amtote nduguye mhanga kwa wachawi wenzake.

Inabainika kwamba kawaida ya wachawi ni kuwa baada ya muda, huhitaji kafara ambayo aghalabu huwa ni ya mwanadamu. Kafara hii ina masharti kwani anayeagizwa kuitoa akishindwa, basi ndiye huifidia kafara ile kwa kupoteza maisha yake kama tunavyoarifiwa katika utenzi. Mhakiki huyu pia ameangazia maudhui ya usaliti ambayo pia yamejitokeza katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Anaelezea usaliti kama hali ya mtu kutoa habari za uongo ama ukweli kutoka kundi moja hadi lingine kwa ajili ya

kuchonganisha wahusika. Katika utenzi huu, Binti Ramadhani na Binti Jizi wanajitokeza kama wasaliti; naye Bw. Shambi anajisaliti mwenyewe.

Mukuthuria pia ameangazia maudhui mengine aliyoyaita umoja ni nguvu. Anaeleza kuwa ushirikiano umedhihirishwa wazi kuwa ndio njia ya pekee ya kutatua matatizo. Anafanua kuwa ushirikiano wa jamii katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* unajitokeza pale watu kama Shambi wanalazimika kujiunga na shughuli za kumtafuta Salima hata ikiwa alikuwa miongoni mwa wauaji. Lau angejitenga, angejulikana mara moja. Mhakiki huyu pia ameshughulikia kipengele cha fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Anadai kuwa lugha iliyotumiwa katika utenzi huo ni ya moja kwa moja isiyo na mafumbo mengi. Anaeleza kuwa katika huu pana matumizi ya jazanda. Anafanua jazanda kama hali ambapo neno hupewa maana nyingine isiyo ile ya asilia; mfano, neno ‘ngoma’ ubeti wa 37 na ‘ngozi’ ubeti wa 36 yametumiwa kijazanda kumaanisha ‘kitu cha kuchezea’ Vilevile ‘ngozi ubeti wa 354 limetumiwa likiwa na maana sambamba na hiyo. Jazanda nyingine ambayo imetumika katika utenzi huo ni ile ya neno ‘watu’ ubeti wa 351 kumaanisha wahalifu.

Mukuthuria ameangazia mbinu ya taashira na utohozi jinsi zilivyotumika katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Kwa mfano, anaeleza kuwa katika ubeti wa 210 ‘nyoka wawili’ wanaashiria mabaya yaliyokuwa karibu kumfika Bw. Shambi. Kuna utohozi wa msamiati; kwa mfano, neno ‘jajimenti’ ubeti wa 377 limetoholewa na kutumiwa. Limetokana na neno la Kiingereza ‘Judgement’.

Kazi hii, imetoa mwongozo wa kuhakiki vipengee vya maudhui na fani katika tenzi za kale katika ushairi wa Kiswahili. Mukuthuria ameangazia maudhui na fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Katika kazi hii Mukuthuria hajahimilisha uhakiki wake

katika misingi ya nadharia yoyote. Jambo hili ndilo linalotofautisha kazi hii na utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kihemenitiki katika kuhakiki vipengee vya maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

Peck na Coyle (1984) wanaeleza kuwa uhakiki huchukuliwa kama utathmini, ufasili na uainishaji wa kazi za fasihi. Haimaanishi 'kuitafutia makosa' kazi hiyo. Uhakiki kama kitendo cha kiakademia humaanisha maoni ya msomaji kuhusu kinachotendeka kitabuni. Coombes (1953) anaeleza kuwa mhakiki bora awapo katika shughuli yake huwa anazingatia mambo mawili au moja ya hayo mawili hutupatia maoni yake kamili na yaliyo wazi kuhusu mtunzi, tamthilia, riwaya, shairi au tungo ili kutuwezesha tufurahie kazi ile. Vilevile mhakiki hulenga kuwafanya wasomaji kuelewa tajriba iliyomo katika utunzi pamoja na ile inayozingatia utunzi huo. Katika kutathmini kazi husika kwa makini jambo hili hudhihirisha vipengee vinavyoipa thamani.

Kutokana na fasili hizi ni kwamba, uhakiki ni shughuli inayohusisha kusoma kwa kina kazi fulani ya fasihi kwa minajili ya kuitathmini, kuichambua na kuweka wazi sehemu kuu zinazoiunda. Lengo kuu la uhakiki ni kumwezesha mhakiki kutoa maoni yake kuhusu kazi husika na kuweza kuwafanya wasomaji kuelewa zaidi na kuifurahia kazi husika ya fasihi.

Kulingana na Wamitila (2003) dhana ya fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kutumia lugha. Lugha hiyo huwa na sifa fulani, kwa mfano ina vikolezo au vitia ladha fulani, imesheheni au kujaza mbinu za kila aina. Haiwezekani kwa mwandishi kuiwasilisha dhamira yake au kuyapitisha maudhui yake bila ya kutegemea fani. Ikiwa mwandishi atataka kuwasiliana na msomaji wake vyema

pamoja na hata kumshawishi na kumwathiri ipasavyo lazima aiteue lugha yake vyema au ahakikishe kuwa lugha yake ina uwezo wa kuuwasilisha ujumbe huo. Uhusiano wa fani na maudhui ni muhimu sana na ni wa kutegemeana, mmoja ni kama upande mmoja wa sarafu.

Senkoro (2011) anaeleza fani kuwa ni ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mtunzi wa kazi ya kifasihi katika kuisana kazi yake. Ufundi huo wa kisanaa unapatikana katika vipengele vya matumizi ya lugha, wahusika, mtindo na mandhari katika kazi ya fasihi. Ni kutokana na ufundi huo ndio wasomaji husema wanavutiwa au kutovutiwa na kazi fulani wakati wanaposoma au kusikiliza kazi husika ya fasihi kama riwaya, ushairi, hadithi fupi, tamthilia, vichekesho na maigizo. Watafiti ambao wamehakiki na kuchambua fani katika riwaya ni wengi kwa kiasi cha kuridhisha huku kila mmoja akichambua au kuhakiki kwa nia tofauti.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002:54), maudhui ni dhana pana inayoweza kuelezewa kwa jinsi mbili ambazo kimsingi zinahusiana. Kwanza, maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi za kifasihi. Masuala haya hutokana na jinsi mtunzi au mwandishi anavyoikuza mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake. Jinsi ya pili ni kutumia maudhui kukirejelea kiwango cha kimaana cha matini au kazi ya kifasihi. Maudhui hujumlisha vipengele vingine kadha kama vile dhamira, falsafa, itikadi na msimamo wa mwandishi pamoja na maadili na mafunzo yanayopatikana katika kazi ya fasihi. Dhamira na maudhui havitokezi tu katika kazi ya kifasihi bali ni zao la mahusiano na maingiliano ya vipengele na mbinu kadha katika kazi inayohusika.

Kutokana na ujuzi wa mtafiti ni kwamba, kwa ujumla fani hurejelea matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi kwa kuchunguza vipengee kama vile tamathali za usemi, uteuzi na mpangilio wa maneno, sajili za lugha kutegemea mazingira mbalimbali, matumizi ya

nahau na misemo mbalimbali. Ni kutokana na utumiaji wa vipengee vya fani ndiposa kazi ya fasihi huweza kuvutia, kuwa na mnato na msisitizo mkubwa kisanii.

Maudhui ni jumla ya masuala yaliyomo katika kazi ya fasihi ambayo mwandishi anayazungumzia. Maudhui huibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira ya kazi fulani ya fasihi. Kutokana na mtazamo huu dhamira husawiriwa kama sehemu kuu ya maudhui.

Lambert katika Bulletin No 2 of the East African Inter-Territorial Language committee ameunukuu *Utenzi wa Mwanamanga*, kisha akaufasiri katika lahaja ya Kiunguja na kutoa tafsiri za baaadhi ya maneno katika utenzi huu kwa lugha ya Kiingereza. Lambert katika kazi yake hii hajafanya uhakiki wowote wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* bali amefanya utafsiri tu.

Chimerah (2013) amezungumzia kwa kiduchu tu kuhusu Wasifu wa Mwanananga (*Utenzi wa Mwanamanga*) ambapo anaeleza kuwa mtunzi wa Wasifu wa Mwanananga alikuwa Liyongo ambaye ni mmoja wa wahusika katika riwaya ya *Siri Sirini* ambaye alimtungia mkewe Mwanananga shairi la kumsifu ambaye pia ni mhusika riwayani. Katika kazi yake hii Rocha hajafanya uhakiki wowote wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* bali amemtumia mhusika wake Liyongo kueleza kwa kifupi utenzi huu kwa lugha ya kinathari.

Nabhany (1996) ameeleza kumhusu Liyongo kama shaha na gwiji wa mashairi. Nabhany ameunukuu *Utenzi wa Mwanamanga* na kisha kuutafsiri kwa lugha ya Kiingereza. Mtaalamu huyu pia ameeleza kwa kifupi kuhusu utungo huu ambapo anadai kuwa beti zote katika utenzi huu zimeandikwa kisitiari na ni vigumu msomaji kuelewa maana fiche za beti hizo. Nabhany katika kazi yake hii ameweka wazi maana

fiche za beti mbili katika utenzi huu wa Mwanamanga. Beti hizi ni: ubeti wa 39 na ubeti wa 41. Katika kazi hii Nabhany hajafanya uhakiki wowote wa maudhui na fani katika utenzi huu.

Roy (2013) ameshughulikia baadhi ya tenzi za Kiswahili zilizoandikwa kati ya karne ya 16 na 20. Katika kazi yake, Roy amefanya utafsiri wa baadhi ya tenzi hizi kama vile: *Utenzi wa Mwanamanga*, *Utenzi wa Al-Inkishafi*, *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya ngonjera vilevile kwa lugha ya Kifaransa. Katika kazi yake hii Roy pia ameangazia swala la urari wa vina katika maghani ya Kiswahili. Katika kushughulikia *Utenzi wa Mwanamanga* yeye amefanya utafsiri wa beti sita za kwanza pekee za utenzi huu kwa lugha ya Kifaransa. Katika kazi yake ya kutafsiri yeye hajafanya uhakiki wowote wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Hili ni pengo ambalo utafiti huu unalenga kuliziba.

2.3 Misingi ya nadharia

Nadharia iliyoteuliwa kuongoza mchakato wa utafiti huu ni nadharia ya kihemenitiki ambayo baadhi ya waasisi wake ni: Friedrich Schleiermacher, Wilhelm Dilthey na Martin Heidegger.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) anaeleza kuwa neno hememitiki linatokana na neno la lugha ya Kiyunani au Kigiriki lenye maana ya “mfasiri” au anayetafsiri kazi fulani. Aghalabu neno hili hutokeza sana katika theolojia ya Kikristo ambako linatumwa kwa maana ya njia za kuchunguza na kufasiri ukweli wa kiroho katika Bibilia. Huu ndio msingi wa kile kinachojulikana kama hememitiki za “Ki-bibilia”. Msingi wa mtazamo wa Kihemenitiki ni uchunguzi wa matendo mbalimbali ya binadamu kama usemaji, upendaji na uchukiaji.

Nadharia hii imejengwa katika imani ya kuwa matendo ya binadamu yanaathirika kwa njia mbalimbali na asasi tofauti zilizoko katika mazingira yake. Hizi ni asasi za kisiasa, asasi ya kitamaduni na asasi ya kiuchumi. Tunaweza kusema kuwa lengo kuu la nadharia hii ni kuchunguza mawasiliano pamoja na ufasiri wa maana za matini mbalimbali. Nadharia hii huchunguza jinsi wasomaji wanavyoielewa matini au kazi fulani pamoja na mbinu au njia za uelewaji au uelewa wenyewe.

Schleiermacher (1998) ameshughulikia suala la uelewaji wenyewe. Kwa maoni yake, suala mojawapo kubwa na muhimu katika fasiri ni kujiepusha na uelewaji mbaya wa kazi inayohusika. Hata hivyo, ni vigumu kujiepusha kabisa na uelewaji mbaya. Kwa maoni yake, uhakiki au fasiri iliyo sahihi inahitaji kukibuni upya anachojaribu kukielewa mhakiki au mfasiri. Kubuni upya huku kunaegemezwa kwenye msingi na kanuni maalum. Mtaalamu huyu aliamini kuwa mhakiki anayeifasiri kazi fulani ana uwezo wa kuielewa kazi hiyo atakayoibuni upya bora kuliko mwandishi. Ubunifu mpya au ufufuaji wa hali halisia ya kazi yoyote unapaswa kufanywa katika viwango viwili maalumu.

Kwanza, kuna ufufuaji wa kisarufi. Katika kiwango hiki kipashio au elementi ya kazi fulani inaeleweka vizuri kwa kuutazama muktadha wake wa kilugha pamoja na kuitazama kazi inayohusika katika muktadha wa kazi mbalimbali za wakati ilipoandikwa. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, kazi ya kifasihi haina maana finyu kwani mawezekano ya maana hayana mipaka.

Katika kiwango cha kisarufi pana umuhimu wa kuichunguza lugha au sifa za kilugha za jamii asilia ya kazi inayohusika pamoja na mpatano au mfuatano fulani wa maneno.

Anatofautisha kati ya ‘lugha’ (sprache) na ‘usemi’ (Rede) wa lugha hiyo ambao hujitokeza katika kazi fulani ya kifasihi. Hili ni suala ambalo liliishia kupendekezwa na Ferdinand de Saussure kwa dhana zake mbili maarufu za “langue” na “parole”.

Saussure (1959) anaibua mambo mawili muhimu katika isimu muundo ambayo ni: langue (mfumo wa lugha) na parole (matumizi lugha). Langue ni mfumo dhahania wa lugha fulani unaotumiwa na jamii mahususi. Mfumo huu huwa jumla ya tajriba – lugha au kanuni za lugha fulani ambazo kila mzawa wa lugha hiyo huweza kuzibwia akilini mwake kutoka kwa jamii tumizi – lugha husika. Langue hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na hufafanua mambo yanayohusu utamaduni wa jamii husika. Langue ni jumla ya ishara zote (sauti na maneno) zilizohifadhiwa akilini mwa watumizi lugha husika. Viambajengo vya mfumo lugha vimo akilini mwa kila mtumizi lugha ambaye hana uwezo wa kuathiri mfumo huo kwa sababu unamilikiwa na ushirika wa jamii husika. Mfumo huo ni changamano sana na ndani yake mna mifumo mingine kadha ambayo pia ni changamano na huchagua muundo wa lugha. Mifumo hiyo inahusu miundo ya sauti (fonolojia), miundo ya maneno (mofolojia) miundo ya sentensi (sintaksia) na maana (semantiki). Mifumo hii inahusiana na kutegemeana kiasi cha kusema kwamba inakamilishana. Langue ni dhahania, kwa maana ya kwamba huwa akilini mwa watumizi lugha. Mfumo huu unajumuisha miongoni mwa mambo mengine ujuzi wa sauti na matumizi ya sarufi. Parole (matumizi lugha) ni hali halisi ya usemaji unaofanywa na mtu binafsi. Parole ni jambo ambalo hutokea katika wakati na mahali mahususi na hivyo basi huwa yale matumizi ya langue (mfumo lugha) anayoyatekeleza mtu binafsi katika mawasiliano. Parole huhusu muktadha mahususi na hili ni suala la kibinafsi linalohusu jamii yaani kama uwili hali; mtu binafsi (matumizi) huitumia lugha ili kuwasiliana na jamii (mfumo).

Kiwango cha pili cha ufufuaji ni cha kisaikolojia. Hapa kinachosisitizwa ni uchunguzi wa usemi au lugha sambamba na mawazo ya anayeyatamka kwa mfano, mwandishi wa kazi inayohusika ya kifasihi. Ingawa mtaalamu huyu anakieleza kiwango hiki kama cha kitaalamu au kisaikolojia, pana umuhimu wa kuiweka mipaka iliyopo kati yake. Kwa kutumia neno “kitaalamu” anasisitiza umuhimu wa kuuelewa mtindo wa mwandishi au msanii anayehusika. Mtindo sio tu matumizi ya lugha bali anasisitiza uchunguzi wa ‘muktadha mzima’ wa mfumo wa kilugha pamoja na ‘muktadha’ wa karibu wa sentensi.

Suala jingine muhimu linaloibuka katika mawazo ya mtaalamu huyu na ambalo linaendelezwa na wana - hementiki wengine, linahusiana na dhana ya ‘kujitambulisha’ au ‘ujitambulishaji’. Hii ni dhana anayoitumia kwa maana ya kuwa msomaji au mfasiri wa kazi ya kifasihi anapaswa kujitahidi awezavyo kujitambulisha kihisia na mwandishi wa kazi hiyo. Mhakiki anaweza tu kubuni na kuisawiri hali ya kiakili ya mwandishi ikiwa atajitahidi kujitambulisha kihisia naye. Tahakiki bora kwa hiyo, zinatokana na wahakiki au wafasiri ambao wana uwezo mzuri zaidi wa kujitambulisha na waandishi wa kazi zinazohusika. Msingi wa kipengele hiki ni kuuvunja mpaka wa kiwakati uliopo kati ya mhakiki na mwandishi wa kazi ya kifasihi. Hili sio jambo jepesi kutekelezeka. Hapa ieleweke kuwa mtaalamu huyu haiweki mipaka wazi kati ya viwango vyote viwili. Vyote ni sehemu ya uelewaji wa kazi fulani na vinapaswa kuchangizana.

Dhana nyingine muhimu inayohusishwa na mtaalamu huyu ni ‘duara ya kiheminitiki’. Msingi wa duara ni kuwa, katika usomaji na uchunguzi wa maana; msomaji anaanza kwa hatua ya kukisia maana ya kazi nzima kabla ya kuzichunguza sehemu mbalimbali zinazounda kazi hiyo nzima. Baadaye anaishia kuibadili maana aliyokisia baada ya uchunguzi huo. Hili litatuelekeza kwenye jambo moja: kuwa sehemu za kazi na uzima

wenyewe vinategemeana. Duara ya kihemenitiki imejengwa katika kweli - kinzani kuwa, haiwezekani kuzielewa au kuzifahamu sehemu (kwa mfano kazi ya kifasihi) bila ya kukielewa kitu kizima chenye na kwamba huwezi kukielewa hicho kizima bila ya kuzifahamu sehemu zake. Mtaalamu huyu anasisitiza kuwa uelewaji wa kazi fulani haupaswi kuegemezwa kwenye lengo la mwandishi katika kuiandika kazi yake. Maelezo yanayofungamana na lengo mara nyingi hayahusiani na uhalisi wa kazi yenyewe. Sababu ya kusema hivi ni kwamba, hakuna njia ya kuweza kulifikia lengo la mwandishi na kwamba, hata kama ingewezekana, huo haufai kama msingi wa kuupima uzuri au ufanifu wa kazi fulani.

Dhana nyingine muhimu katika uwazaji wa mtaalamu huyu inahusiana na kile alichokiita ‘utukuzaji’. Neno hili linaakisi mwelekeo fulani wa kidini lakini maana yake ni tofauti kabisa. Mtaalamu huyu anaamini kuwa msomaji au mfasiri anapoichukua kazi fulani huwa ana makisio fulani ambayo analazimika kuyapitia upya labda hata kupuuza baadhi yao aisomapo kazi fulani kwa mfano, tunapoichukua riwaya kama *Babu Alipofufuka*, tuna makisio fulani ambayo yana misingi mbalimbali kama usomaji wa kazi nyingine za S. A Mohamed, anwani yake, usomi wetu, utamaduni wetu na uelewa wetu wa mielekeo ya kifasihi. Makisio tuliyo nayo yanathibitishwa au tunalazimika kuyapitia tunapoanza kuisoma riwaya hiyo na kuyafuata maisha ya mhusika K ambayo ni istihara ya njia panda ya mataifa yetu, dhihiriko la matokeo ya makutano ya ubepari na ubinafsi kwa upande mmoja na utu na ubinadamu kwa upande wa pili.

Mawazo ya Schleiermacher yanaendelezwa na Dilthey (1996) ambaye alipendekeza kuwa pana haja msomaji au mhakiki kujaribu; kuufufua muktadha asilia wa kazi inayohusika na kujaribu kujiweka katika muktadha huo ili kuweza kuipata maana asilia. Dilthey analisisitiza suala alilolizua Schleiermacher. Yeye aliamini kuwa

kujitambulisha au kujihusisha kikamilifu na mwandishi wa kazi ya kifasihi huwa na lengo kuu la kuhakikisha kurudufishwa kwa tajriba uzoefu, yaani tajriba ya mwandishi wa kazi inayohusika na tajriba ya mhakiki au mfasiri anayejihusisha na kazi yake. Mchango wa Dilthey katika mtazamo wa kihemenitiki ni kuingiza kipengele cha kihistoria. Kwa mujibu wa mawazo yake, kazi ya kifasihi inaweza kuwa na maana mbalimbali kwa wasomaji mbalimbali. Alisisitiza ukweli tunaoujua wazi kuwa kila msomaji anayeikabili kazi fulani ya kifasihi huiendea kazi hiyo akiwa na kiwango maalumu cha ufahamu, chukulizi fulani, akitokana na utamaduni fulani, na akiwa na utaalamu na uzoefu fulani.

Mseto wa sifa hizi huathiri kwa kiasi kikubwa jinsi wasomaji au wahakiki wanavyoihakiki na kuipa maana kazi fulani ya fasihi. Katika msingi huu, msomaji au mhakiki ana uwezo fulani wa kuiunda maana ya kazi za kifasihi. Mawazo ya aina hii yanajitokeza katika nadharia zinazohusika na upokezi wa kazi ya kifasihi au zinazochunguza nafasi ya msomaji.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa nadharia hii imejengwa katika jitihada za kubaini mbinu, nia, mikakati na vipengele vya kuichunguza na kuipata maana ya matini au kazi ya fasihi. Wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa msomaji anachangia kwa kiasi kikubwa katika kubuni maana ya kazi fulani. Hili linaeleza kwa nini kazi fulani inaweza kuwa na maana mbalimbali kwa wasomaji tofauti tofauti katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Mawazo haya yanajitokeza katika nadharia zinazohusika na upokezi wa kazi ya kifasihi au zinazochunguza nafasi ya msomaji.

Mtaalamu mwingine ambaye amekuwa na athari kubwa ni Martin Heidegger (1926) kwa matazamo wake wa kihistoria (historicist) wa njia za kufasiri, mwanafalsafa huyu

aliamini kuwa njia mwafaka ya kuikabili ‘duara ya hementitiki’ ni uhusiano wa huku na huku kati ya msomaji au anayefasiri kazi fulani na utamaduni unaohusika. Mtindo huu unamwezesha kuyafahamu masuala kadha muhimu. Sifa moja inayohusishwa na Heidegger, na ambayo imefumbatwa katika uwazaji huu ni uchunguzi wa masuala ya ki-ontolojia (kuwako) au suala la binadamu na kuwako kwake ulimwenguni. Ameeleza kuwa binadamu kulingana na maumbile yake ni kiumbe chenye uwezo wa kufasiri mambo kilichotawaliwa na uelewa wa maana katika muktadha uliogomezwa kwa mtazamo wa kihisia.

Mwananadharia mwingine ambaye ameyaendeleza mawazo haya ni Han-George Gadamer (2004). Kitabu cha mtaalamu huyu *Wahrheit und Methode* (ukweli na mbinu) kilikuwa msingi mkuu wa nadharia ya hementitiki Ujerumani. Mtaalamu huyu anaikabili kazi ya fasihi kama mchezaji anayeshiriki katika mchezo fulani na afanyavyo hivyo huwa ameupoteza uasili wake: huwa sio mwenyewe tena. Basi sehemu ya mchezo huo kwa mujibu wa Gadamer, uelewaji huzunguka na hurudi kwenye mikondo ya uelewaji maalumu. Usomaji huanzia kwenye chukulizi za kimapendeleo (prejudice). Mhakiki anapaswa kuziondoa au kuzitupilia mbali chukulizi hizo. Mtaalamu huyu anaamini kuwa fasiri sahihi huwa imebagua kati ya uongo na ukweli. Hata hivyo mhakiki anabakia katika mkondo wa ki-uchukulizi wa kimapendeleo ambayo ni sifa moja inayotambulisha ulimwengu wa mhakiki au mfasiri. Mawazo haya yanazua matatizo wazi kama njia za kutambua ni chukulizi zipi sahihi na ni zipi zinazopotosha.

Gadamer anaamini kuwa mkondo wa mfasiri au mhakiki unapanuliwa na mazungumzo yaliyopo kati yake na kazi inayohusika. Mazungumzo hayo au kama asemavyo ‘uelewa’ (Verstehen) huo hujitokeza kwa kuungana kwa mikondo. Kulingana na

mtaalamu huyu, kuelewa ni tokeo la muungano wa mikondo. Mhakiki wa fasihi anazua maswali kwa kazi inayohusika nayo pia inamuuliza maswali. Pana mazungumzo kati yake na kazi ya kifasihi.

Mwandishi kama Ricour (2003) amechangia hoja ambayo inachukua nafasi muhimu katika uhakiki wa Ki-hemenitiki. Hii ni dhana ya 'Hemenitiki za kituhuma'. Dhana hii hutumika kuelezea njia za usomaji na umuhimu wa kuyatilia maanani mambo ambayo hayasemwi waziwazi kuliko yaliyosemwa. Msingi wake ni kuelewa kuwa yasiyosemwa yana nafasi au uzito sawa, au labda hata mkubwa, kuliko yaliyosemwa. Dhana hii ya hemenitiki za kituhuma inahusiana kwa kiasi kikubwa na mawazo ya Pierre Machery kuhusu umuhimu wa kuyaangaza mapengo yaliyoko kwenye kazi ya kifasihi kwa kuchagua yasiyosemwa waziwazi. Dhana hii inaweza kuhusishwa katika upana wake na mitazamo ya Mar, Freud na Nietzsche ambayo haielekei kuridhika na picha za juu ila hupenda kuzama ndani na kutambua maana halisi.

Kwa kiasi kikubwa uhakiki bora wa kifasihi ni ule ambao utapiga hatua na kuibua masuala ambayo yamefichwa. Hii ilikuwa nia kuu ya mtafiti kufanya utafiti huu akitumia nadharia hii ya kihemenitiki: kuchochea usomaji, uelewa na uhakiki wa *Utenzi wa Mwanamanga* ambao ni mojawapo ya tenzi za kale katika fasihi ya Kiswahili.

2.4 Mihimili ya nadharia

Nadharia hii ya kihemenitiki inahusu ufasiri wa kazi za kifasihi. Mihimili ifuatayo iliweza kutumika kuongoza utafiti huu kama ilivyoasisiwa na waasisi wake:

- Kulingana na Dilthey (1996) anasisitiza kuwa pana haja ya msomaji kujaribu kuufufua muktadha asilia wa kazi inayoshughulikiwa na kujaribu kujiweka katika muktadha huo ili mhakiki aweze kupata maana asilia.
- Mtaalamu huyu pia anazingatia kipengele cha kihistoria. Katika msingi huu anasisitiza kuwa kazi fulani ya fasihi yaweza kuwa na maana mbalimbali kulingana na vipindi vya kihistoria.
- Heidegger (1926) anafafanua kuhusu duara ya kihemenitiki. Anaeleza msingi wa duara hii ni katika usomaji na uchunguzi wa maana, msomaji anaanza kwa kukisia maana ya kazi nzima kabla ya kuzichunguza sehemu mbalimbali zinazounda kazi hiyo nzima. Baadaye anaishia kuibadili maana aliyokisia baada ya uchunguzi huo.
- Schleiermacher (1998) anaeleza kuwa nadharia hii inashikilia kuwa uhakiki au fasiri iliyo sahihi inahitaji kukibuni upya anachojaribu kukielewa mhakiki au mfasiri. Ubunifu mpya au ufufuaji wa hali halisi ya kazi yoyote unapaswa kufanywa katika viwango viwili maalumu ambavyo ni:

Kwanza: ufufuaji wa kisarufi. Katika kiwango hiki kipashio au elementi ya kazi fulani inaeleweka vizuri kwa kutazama kazi inayohusika katika muktadha wa kazi mbalimbali za wakati ilipoandikwa.

Pili: ufufuaji wa kisaikolojia. Kinachosisitizwa hapa ni uchunguzi wa usemi wa lugha sambamba na mawazo ya anayetamka kwa mfano mwandishi wa kazi inayohusika ya kifasihi. Msingi huu unasisitiza uchunguzi wa ‘muktadha mzima’ wa mfumo wa kilugha pamoja na ‘muktadha’ wa karibu wa sentensi.
- Mtaalamu huyu pia anaeleza kuwa nadharia hii inahusisha dhana ya kujitambulisha na ujitambulishaji ambapo ina maana kuwa msomaji au mfasiri wa kazi ya kifasihi anapaswa kujitahidi awezavyo kujitambulisha kihisia na mwandishi wa kazi hiyo.

Utafiti huu ulinufaika pakubwa kutokana na nadharia hii. Kwanza, mtafiti alipata kuona jinsi asasi ya ndoa ilivyomwathiri msanii na kuidhihirisha katika utunzi wa utenzi huu kwa lengo la kumsifu mkewe. Mtunzi wa utenzi huu ametumia lahaja ya za Kipate, Kiamu, Kingozi na lugha ya Kiarabu na sitiari pevu. Yeyote anayepata fursa ya kusoma utenzi huu kuna uwezekano mkubwa wa kutouelewa kwa urahisi. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kupata maana asilia za maneno hayo ya lahaja ya Kipate, Kiamu, Kingozi na lugha ya Kiarabu kutoka kwa walengwa walioteuliwa kimakusudi na mtafiti. Mtunzi wa utenzi huu ametumia mbinu ya sitiari/mafumbo kupitisha ujumbe wake. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kwani ilimwongoza katika mchakato wote wa kufumbua mafumbo hayo.

Nadharia hii ya kihemenitiki pia husisitiza sana uzingatiaji wa kipengele cha kihistoria. Msingi huu unasisitiza kuwa kazi fulani ya kifasiri yaweza kuwa na maana mbalimbali kulingana na vipindi vya kihistoria. Namna nyingine ambayo utafiti huu ulinufaika ni kwamba ulizingatia kipengele cha kihistoria ili kuweza kupata fasiri kamili ya maana za maneno yaliyotumiwa katika utenzi huu kwa kurejelea kipindi kile ambacho utenzi huu uliandikwa. Mchakato wote wa kutafuta maana na fasiri za maneno katika *Utenzi wa Mwanamanga* ulijikita katika kile kipindi utenzi huu ulipoandikwa ndiposa maana kamili iliyokusudiwa iliweza kubainika. Msingi huu uliusaidia utafiti huu kupata fasiri sahihi kwani utafiti huu ulipata uwezo wa kubagua kati ya uongo na ukweli.

Nadharia hii pia hulenga kuchunguza mawasiliano pamoja na ufasiri wa maana za matini mbalimbali hivyo basi iliongoza mchakato wote wa kufasiri maneno ya lahaja za: Kipate, Kingozi, Kiamu, Kiarabu, msamiati wa ubaharia na mafumbo yaliyotumiwa ili kuuweka bayana utenzi huu ndiposa uweze kueleweka kwa urahisi. Kwa ujumla, mihimili ya nadharia hii ilitoa mwongozo toshelevu kuhakiki *Utenzi wa Mwanamanga*.

Utafiti huu uliweza kuitumia nadharia ya kihemenitiki kuumulika utenzi huu katika kuhakiki vipengee vya maudhui na fani na kisha kuviweka bayana.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Kitangulizi

Sura hii imehusu ukusanyaji wa data. Sura hii imeeleza kindakindaki kuhusu mchakato wa ukusanyaji wa data kuanzia kwa ukusanyaji wa data wenyewe, utaratibu wa utafiti, data iliyokusanywa, mbinu za kukusanyia data na vifaa vya kukusanyia data. Sura hii pia imefafanua na kuweka bayana utaratibu uliofuatwa katika uchanganuzi wa data.

3.2 Mpangilio wa utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo uliofanyika maktabani na vilevile nyanjani. Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kwamba utafiti wa kimaelezo mbali na kukusanyia data mara nyingi huweza kutoa msingi wa kubuniwa kwa mihimili muhimu ya maarifa na suluhisho kwa matatizo muhimu. Utafiti wa aina hii huhusisha upimaji, upangaji, uchanganuzi, ulinganishi na ufasiri wa data. Maktaba alizozuru mtafiti ni: Maktaba ya Chuo Kikuu cha Pwani, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Nairobi bewa la Mombasa na Maktaba ya Kenya - Werugha. Utafiti huu ulianza maktabani ambapo *Utenzi wa Mwanamanga* ulisomwa pamwe na tenzi nyingine nne zilizokuwa zimeteuliwa. Huko maktabani, tasnifu, makala, pamwe na tahakiki za tenzi zilizoteuliwa zilisomwa ili kupata mwelekeo wa jumla wa jinsi ya kuhakiki maudhui na fani katika tenzi huku maelezo mwafaka yakinukuliwa. Makala zilizohusiana na nadharia iliyoongoza utafiti huu zilisomwa ili kuweza kuielewa na kudondoa misingi ya nadharia ya kihemenitiki iliyomsaidia mtafiti kuumulika utenzi huu wakati wa utafiti.

Baada ya hapo mtafiti alijiandaa kwenda nyanjani. Mtafiti alizuru jiji la Nairobi na Kisiwa cha Mombasa. Huko nyanjani mtafiti aliandaa mahojiano ya ana kwa ana na kila mlengwa kwa kuzingatia maagano yake na walengwa hao. Kwa wale walengwa

ambao mtafiti hakufaulu kukutana nao ana kwa ana kwa mahojiano mtafiti alitumia mahojiano ya simu kama kifaa cha kupata data kutoka kwao. Habari zote zilizopatikana zilinukuliwa vizuri kwenye karatasi na baadaye kufanyiwa uchanganuzi. Baada ya hapo mtafiti alirudi katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Pwani ambapo alichanganua data hiyo pamoja na ile data aliyokuwa ameipata maktabani. Uchanganuzi wa data katika utafiti huu ulikuwa ni ule wa kiuthamano. Kombo na Tromp (keshatajwa) wanafafanua uchanganuzi wa kiuthamano kuwa hurejelea uchunguzi wa data iliyokusanywa katika utafiti na kutoa uamuzi. Huhusisha kuweka bayana viambajengo na kuchanganua kwa kina habari iliyopatikana na kutoa uamuzi. Mtafiti alichanganua data iliyopatikana kiuthamano huku akihakikisha kwamba maswali ya utafiti yamejibiwa. Baada ya hapo mtafiti aliandaa matokeo ya utafiti wake na kutoa mapendekezo yake.

3.3 Utaratibu wa utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na nyanjani. Kwanza, ulianza maktabani lengo kuu likiwa kupata picha halisi kuhusu ushairi wa Kiswahili hususan tenzi za kale katika fasihi ya Kiswahili. Mtafiti pia alilenga kupata kujua ni tenzi zipi katika fasihi ya Kiswahili ambazo zimefanyiwa utafiti na vilevile kuweza kutambua utafiti wowote uliofanyiwa *Utenzi wa Mwanamanga* ili kubainisha pengo lililopo. Maktabani mtafiti alidurusu maandishi kadha ambayo yalihusiana na mada ya utafiti huu ambao ulihusu uhakiki wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Mtafiti aliweza kupata fursa ya kudurusu kazi ambazo zilihusu uhakiki wa maudhui na fani katika baadhi ya tenzi za kale kama vile: *Al-Inkishafi*, *Utenzi wa Mwanakupona*, *Utenzi wa Fumo Liyongo na Swifa ya Nguvumali*. Mtafiti aliweza kugundua kwamba *Utenzi wa Mwanamanga* haujafanyiwa utafiti wa kitaaluma na wale walioandika kuuhusu waliutaja na kuuzungumzia kwa kiduchu tu. Mtafiti aliweza kugundua pia hakuna uhakiki wowote wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa mtazamo wa

kihemenitiki ambao umewahi kufanywa. Hili ni pengo ambalo mtafiti aliamua kuliziba kwa kuendesha utafiti huu. Mtafiti aliamua kujikita katika kuhakiki vipengee vya maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa sababu vipengee hivi hufungamana na kutegemeana na ni msingi mkuu wa kuelewa kikamilifu kazi yoyote ya fasihi. Baada ya kudurusu maandishi kuhusu tenzi za kale mtafiti aliamua kuteua tenzi nyingine nne ili kusaidia katika kuendesha utafiti huu. Lengo la kufanya hivi ni kwamba uhakiki wa maudhui na fani katika tenzi hizi ulimpa mtafiti mwelekeo wa kuhakiki vipengee hivi katika tenzi za kale. *Utenzi wa Mwanamanga* ulipitiwa pamoja na tenzi nyingine nne za kale zilizokuwa zimeteuliwa ili kuufanikisha utafiti huu. Tenzi zilizoteuliwa ni: *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*, *Utenzi wa Al-Inkishafi*, *Utenzi wa Mwanakupona* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Pili, kulifuata utathmini wa kina kuhusu maudhui na fani mbalimbali katika tenzi hizo ili kupata mwongozo wa kuhakiki vipengee hivyo katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Tatu, kwenda nyanjani. Mtafiti alizuru jiji la Nairobi na baadae kisiwa cha Mombasa ili kuwafikia walengwa aliowateua kimakusudi ili kuweza kufanikisha utafiti huu. Lengo la kwenda nyanjani lilitokea baada ya mtafiti kugundua kwamba *Utenzi wa Mwanamanga* uliandikwa kwa kutumia lahaja tatu za Kiswahili ambazo ni: Kingozi, Kiamu na Kipate. Utenzi huu pia ulidhihirisha matumzi ya lugha ya Kiarabu. Kutokana na matumizi haya ya msamiati wa lahaja hizi na Kiarabu mtafiti alijukumika kuzuru nyanjani ili kuwahoji walengwa aliowateua ili kupata ufasiri wa maana za msamiati huo na vilevile kuweza kupata maoni yao kuhusu sitiari nyingi zilizotumiaka katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Mtafiti pia alilenga kupata maoni yao kuhusu maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* ili kuweza kunawirisha data aliyopata maktabani. Mtafiti aliandaa mwongozo wa utafiti ambao ulimwezesha kupata data aliyokuwa akihitaji ili kuweza kujibu maswali ya utafiti na kuwezesha kutimizwa kwa malengo ya utafiti. Wataalamu hawa waliweza

kutoa data ambayo iliweza kuongeza uzito wa utafiti huu na kufanya matokeo ya utafiti huu kuwa ya kuaminika.

3.4 Jumua na uteuzi wa sampuli

Ingawa mtafiti alitambua kuwepo kwa tenzi nyingi katika fasihi ya Kiswahili, mtafiti aliteua mmoja ambao ndiwo alioutafitia, *Utenzi wa Mwanamanga*. Tenzi nyingine nne pia ziliteuliwa ili kufanikisha utafiti huu. Tenzi hizo ni: *Swifa ya Nguvumali*, *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Mwanakupona* na *Utenzi wa Al-Inkishafi*. Tenzi hizi nne mtafiti aliziteua kwa makusudi kwa sababu zote ziliandikwa kabla ya karne ya 19 na pia zimefanyiwa utafiti na kuhakikiwa na watafiti wengine ambapo mtafiti alipata mwelekeo wa kijumla wa jinsi ya kuhakiki maudhui na fani katika tenzi za kale.

Katika kuteua jumuiya, mtafiti alifanya uteuzi wa makusudi ili kupata jumuiya aliyonua kuihoji pindi atakapokuwa nyanjani ili kupata data. Kasomo (2006) anafafanua uteuzi wa kimakusudi kama aina ya uteuzi ambapo mtafiti huchagua jumuiya yake akizingatia misingi fulani. Walengwa walioteuliwa na kuhojiwa na mtafiti ni: Prof. Sheikh Ahmed Nabhany, Prof. Kinene wa Mutiso, Prof. Kyallo Wadi Wamitila, Prof. Rayya Timmamy na Bwana Mohamed Karama.

Mtafiti aliwateua walengwa hawa kwa sababu zifuatazo:

- i. Walengwa hawa ni watu watajika katika fasihi ya Kiswahili kwani ni wataalamu katika fasihi ya Kiswahili na wana uelewa mkubwa kuhusu tenzi za kale za katika fasihi ya Kiswahili. Data waliyotoa ilikuwa ya kuaminika.
- ii. Mtafiti alifanya uteuzi wa kimakusudi wa kina kimukadha ambapo aliwateua walengwa watano. Kulingana na mtafiti walengwa hawa ni wataalamu watajika katika fasihi ya Kiswahili na wangetosheleza mahitaji yote ya utafiti huu kindakindaki.

Kutokana na tajiba zao katika fasihi ya Kiswahili wataalamu hawa walikuwa na ufahamu mkubwa kuhusu *Utenzi wa Mwanamanga* ambao ndiwo uliotafitiwa.

iii. Mtaalamu Prof. Sheikh Ahmed Nabhany alipatikana katika mkoa wa pwani eneo la Lamu - Matondoni. Wataalamu wengine ambao ni: Prof. Kyallo Wadi Wamitila, Prof. Rayya Timmamy na Prof. Kinene wa Mutiso walipatikana Nairobi. Mtaalamu Mohamed Karama naye alipatikana kisiwani Mombasa. Mtafiti alizuru maeneo haya yote ili kuweza kuendesha mahojiano na wataalamu hawa. Mtafiti aliweza kukutana na wahojiwa hawa wote isipokuwa Prof. Wamitila ambaye hakuweza kumhoji kutokana na sababu ambazo hazingeweza kuepukika.

iv. Mtafiti hakuona haja ya kuwahoji watu wa kawaida wanaoelewa lahaja za Kingozi, Kipate, Kiamu na lugha ya Kiarabu kwani baadhi ya wale aliokutana nao na kuwahoji walidai kuwa hakuwa wakiufahamu *Utenzi wa Mwanamanga*. Kutokana na kutofahamu huku mtafiti aliona kuwa watu hao hawatakuwa na mchango wowote na ndio maana hakuwahusisha katika utafiti huu.

Mtafiti aliwahi kuzuru Kisiwa cha Amu wakati wa tamasha za utamaduni wa watu wa Lamu mnamo tarehe 13 Novemba 2016 ambapo alimtembelea Marehemu Prof. Sheikh Ahmed Nabhany nyumbani kwake Matondoni akiandamana na Prof. Rocha Chimerah. Katika matembezi haya mtafiti aliweza kumhoji Prof. Nabhany katika tangulizi-tafiti ya utafiti wake. Prof. Nabhany aliweza kujibu kiasi kikubwa cha maswali aliyokuwa ameyaandaa mtafiti ingawaje mtafiti alipanga kurudi tena kwake kwa mahojiano ya kina zaidi. Mchango wa Prof. Nabhany katika utafiti huu ni muhimu mno kwani umemsaidia mtafiti kuweza kutimiza mahitaji ya utafiti huu kikamilifu. Jambo hili ndilo lililomfanya mtafiti kushindwa kulitoa jina la Marehemu Prof. Nabhany katika orodha ya walengwa aliokuwa amewateua kwa makusudi baada ya mauko yake yaliyotokea tarehe 23 Februari 2017. Mungu ailaze roho yake pahali pema peponi.

Katika mchakato wa kuwahoji wataalamu hao wanne waliokuwa wamebakia mtafiti aliandaa mwongozo wa mahojiano ambao ulimwongoza katika kuendeleza mahojiano kati yake na walengwa.

3.5 Utaratibu wa ukusanyaji data

Utafiti huu ulifanyika maktabani na nyanjani. Ukusanyaji wa data ulihusu kusoma na kuhakiki maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Kadhalika, ili kufanikisha jambo hili, makala, vitabu, pamoja na tasnifu za uhakiki wa tenzi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili zilipitiwa ili kuweza kuurutubisha utafiti huu. Aidha, kazi mbalimbali zilizohakiki vipengele vya maudhui na fani katika tenzi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili zilipitiwa vilevile. Utafiti wa maktabani ulimwezesha mtafiti kupata data ambayo ilihusiana na mada ya utafiti na pia mtafiti alipata mwelekeo wa kijumla kuhusu uhakiki wa maudhui na fani katika tenzi za kale za fasihi ya Kiswahili.

Utafiti huu kwa kiwango fulani ulihusisha kuzuru nyanjani ili kuweza kupata data mbalimbali kutoka kwa wataalamu walioteuliwa kwa makusudi na mtafiti katika fasihi ya lugha ya Kiswahili. Utafiti wa nyanjani ulimwezesha mtafiti kupata (maelezo) ya kina kuhusu maudhui, fani na maana za msamiati uliotumika katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa kujelea kipindi cha kihistoria utenzi huu ulipotungwa. Kadhalika utafiti huu pia ulihusisha usakuraji na ukusanyaji wa makala faafu kupitia kwa mtandao katika tovuti mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Ukusanyaji wa data kutoka kwenye mtandao ulimwezesha mtafiti kupata makala katika nyaraka za kiakademia na vitabu mbalimbali kwenye mtandao ambavyo vilikuwa na maelezo ya kina kuhusu tenzi za kale na lahaja za Kiswahili. Mtafiti alikusanya maelezo hayo yote na kuyapitia kisha kuyachanganua akizingatia malengo ya utafiti huu.

3.6 Vifaa vya utafiti

Mtafiti aliteua mahojiano kama kifaa alichonua kukitumia katika utafiti wake ili kukusanyia data. Mtafiti aliandaa mwongozo wa mahojiano ambao ulimwongoza katika kuendesha mahojiano ya ana kwa ana baina yake na walengwa. Data iliyopatikana kutokana na mahojiano hayo ilinukuliwa kwenye karatasi. Mtafiti pia alitumia kinasasauti alipokuwa akiwahoji wataalamu hao ili kuweza kunasa mahojiano hayo. Baadaye mtafiti aliweza kuyafanyia uchanganuzi wa kina.

Mtafiti pia alitumia mahojiano ya simu katika kuwahoji wataalamu ambao hakuweza kupatana nao ana kwa ana ili kuwahoji. Mtaalamu Rayya Timmamy alihojiwa kupitia njia hii. Mtafiti aliteua vifaa hivi kwa sababu zifuatazo:

- i. Kasomo (2006) anaeleza kwamba mahojiano ya ana kwa ana ndicho kifaa kitumikacho zaidi katika utafiti wa kimaelezo.
- ii. Mahojiano ni kifaa kilicho rahisi kukitumia kikilinganishwa na vifaa vingine kama vile hojaji, kutazama nakadhalika.
- iii. Kupitia mahojiano habari za kina huweza kupatikana.
- iv. Kifaa cha mahojiano hutoa fursa nzuri kwa anayehojiwa kuweza kujieleza vizuri ili mtafiti apate kumwelewa vyema.
- v. Mtafiti huwa na fursa nzuri ya kuuliza maswali kuhusu habari iliyotolewa ili kusawazisha mtafaruku au ugiligili wowote.

Mtafiti aliandaa mahojiano na walengwa hao na kupata habari za kina ambazo aliweza kuzichanganua na kuziweka bayana katika utafiti huu. Mchango wa walengwa hao ulimwezesha mtafiti kutimiza malengo ya utafiti huu.

3.7 Data iliyokusanywa

Utafiti huu ni wa kimaelezo hivyo basi data iliyokusanywa ni maelezo mbalimbali kuhusu maudhui, fani na maana za msamiati wa kilahaja uliotumika katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa mujibu wa kipindi cha historia cha karne ya 12. Data iliyokusanywa ilitokana na usomaji, mahojiano ya wataalamu walioteuliwa na uhakiki wa *Utenzi wa Mwanamanga*. Vipengele vilivyochunguzwa ni maudhui na fani. Katika utafiti wa maktabani mtafiti alipata data ifuatayo: Maudhui yaliyodhihirika katika huu ni: mapenzi, ushirikiano katika jamii, utamaduni, dini, usanii wa mashairi, uzuri wa mwanamke, kuheshimiana, unyumba, ushirikina nafasi ya mwanamke katika jamii, ubaharia na wasifu wa mwanamke kwa mtazamo wa mwanamume. Vipengele vya fani vilivyodhihirika na kuchunguzwa ni: lugha ya kishairi, arudhi za kishairi, muundo, lahaja, tamathali za usemi na idhini za kishairi. Katika utafiti wa nyanjani yafuatayo yaliweza kupatikana: tafsiri za msamiati wa lahaja ya Kiamu, Kingozi, Kipate na wa lugha ya Kiarabu. Walengwa pia waliweza kutoa maoni yao tofauti-tofauti kuhusu mafumbo yaliyotumika kwenye *Utenzi wa Mwanamanga* ambapo mtafiti aliweza kuchanganua na kuwasilisha maoni hayo na kuweka bayana maana ya mafumbo hayo. Utafiti wa nyanjani pia ulimwezesha mtafiti kutambua matumizi ya aina mbalimbali za taswira ili kuchochea hisia mbalimbali za msomaji kama vile: kuona, kuonja, kugusa, kunusa na kusikia. Data iliyopatikana kutoka kwenye utafiti wa maktabani na ule wa nyanjani ulimwezesha mtafiti kuyajibu maswali ya utafiti na kuyatimiza malengo ya utafiti.

3.8 Mbinu za kukusanya data

Utafiti wa maktabani ulimwezesha mtafiti kupata maelezo ya kimsingi kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia iliyoongoza utafiti huu. Mtafiti alizingatia kikamilifu usomaji wa vitabu, makala, tahakiki na tasnifu mbalimbali zilizokuwepo

maktabani. Udurusu wa tahakiki, majarida faafu, tasnifu na vitabu mbalimbali ulimsaidia katika kuelewa tahakiki za awali kuhusu maudhui na fani katika tenzi za kale zilizoteuliwa katika utafiti huu. Uhakiki wa maudhui na fani katika tenzi hizi ulirejelewa na kusomwa ili kuelewa vipengele vya maudhui na fani katika tenzi hizi kisha vipengele hivi katika *Utenzi wa Mwanamanga* kuhakikiwa.

Mbinu ya utafiti iliyotumiwa nyanjani ni ya mahojiano ya ana kwa ana baina ya mtafiti na wale wataalamu walengwa. Mtafiti aliweza kupata maudhui, vipengele vya fani, tafsiri za msamiati mbalimbali na hisia alizotumia mtunzi wa *Utenzi wa Mwanamanga* katika kumwelezea mhusika wake kwenye utenzi. Mtafiti aliandaa mwongozo wake binafsi wa kuendesha mahojiano alioutumia wakati alipokuwa nyanjani. Katika mwongozo huo mtafiti aliandaa maswali ambayo yalihusiana na mada ya utafiti pekee na kuweza kupata data muhimu iliyonufaisha utafiti na kumwezesha kutimiza malengo ya utafiti. Utafiti huu pia ulilenga kupata tafsiri za maneno mengine na ufafanuzi wa kina kuhusu mbinu zingine za uandishi kama vile: sitiari za safari alizotumia msanii katika kuisana kazi yake. Juhudi za kukutana na wataalamu walioteuliwa zilizia matunda isipokuwa kwa mtaalamu mmoja ambaye ni Prof. Kyallo Wamitila. Kutokana na sababu ambazo hazingeweza kuepukika mtafiti hakuweza kuandaa mahojiano kati yake na mtaalamu huyu.

Mchakato wote wa utafiti uliweza kuzingatia nadharia ya Kihemenitiki kwa namna ifuatayo: Kwanza, mtafiti alilenga kuchunguza maana katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Aliweza kusoma makala mbalimbali ambayo yalihusu lahaja za Kiswahili hususan lahaja za Kiamu, Kingozi na Kipate. Nyanjani aliweza kupata fasiri za maneno ya lugha ya Kiarabu pamoja na ya lahaja zilizotumika kwenye utenzi. Katika kupata fasiri hizi mtafiti alizingatia kipengele cha kihistoria ambacho katika utafiti huu mtafiti alizingatia

kipindi cha karne ya 12 ambapo inakisiwa kuwa ndiwo wakati alipowahi kuishi Fumo Liyongo mtunzi wa *Utenzi wa Mwanamanga* kwa mujibu wa El-Maawy (keshatajwa). Lengo la kufanya hivi lilikuwa kuweza kupata fasiri za maneno yaliyotumika ili kupata maana halisi ya maneno hayo kwa mujibu wa kipindi hicho. Hii ni kwa sababu kazi ya kifasihi yaweza kuwa na maana mbalimbali kulingana na vipindi tofauti-tofauti vya kihistoria. Pili, Mtafiti aliweza kuubuni upya *Utenzi wa Mwanamanga* kwa kuuandika kwa tafsiri ya Kiunguja ili kuwezesha ufufuaji wa kisaikolojia ambapo aliweza kuchunguza usemi wa lugha sambamba na mawazo ya mwandishi wa huu. Mtafiti katika mchakato wa kusoma na kuhakiki *Utenzi wa Mwanamanga* alijitahidi kujitambulisha na hisia za mwandishi wa utenzi huu. Alifaulu kutekeleza msingi huu kwa kuchunguza tamathali ya usemi ya taswira na aina zake ili kupata hisia zilizotumiwa na mtunzi kimakusudi katika kumwelezea mhusika wake kwenye utenzi. Mtafiti aliweza kuitumia nadharia ya kihemenitiki kikamilifu kuuendesha utafiti huu na kuweza kupata data ya kuaminika iliyomwezesha kujibu maswali ya utafiti na kutimiza malengo ya utafiti.

3.9 Uchanganuzi wa data

Data iliyotokana na mahojiano, uchambuzi wa *Utenzi wa Mwanamanga* pamoja na maandishi yanayohusu utafiti huu yakiwemo tahakiki za tenzi zilizoteuliwa ilichambuliwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa kufuata utaratibu ufuatao: Kwanza, utenzi unaotafitiwa pamoja na tenzi nne zilizoteuliwa na tahakiki zake zilisomwa kindakindaki huku vipengee vya maudhui na fani vikiangaziwa vilivyo. Pili, vipengee vya maudhui na fani viliangaziwa jinsi vilivyodhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Tatu, Kulifuata usikilizaji makini wa mahojiano yaliyokuwa yamerekodiwa kisha kuyachambua kwa kina kulingana na malengo na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Data iliyokuwa imenukuliwa kutokana

na mahojiano ya wataalamu walioteuliwa ilichanganuliwa na kujumuishwa na data iliyopatikana maktabani na kisha kusawazishwa kulingana na mahitaji ya utafiti. Nne, mtafiti alifanya uchanganuzi wa data iliyosawazishwa na kuitathmini ili kuhakikisha maswali, malengo pamoja na mahitaji ya utafiti huu yameafikiwa kama ilivyoniwa. Matokeo ya utafiti huu yaliwekwa bayana na kwa kiwango fulani mchango wa kila mtaalamu aliyehojiwa pia uliwekwa wazi.

4.0 Uaminiki wa utafiti

Utafiti huu uliendeshwa kwa kuzingatia sheria zinazoongoza tafiti za kiakademia. Data iliyokusanywa ilitokana na kudurusu vitabu, tahakiki, makala na majarida mbalimbali ya kiakademia. Katika utafiti wa nyanjani mtafiti alifanya uteuzi wa kimakusudi ambapo aliwateua walengwa watano ambao wote ni wataalamu katika fasihi ya Kiswahili hivyo basi data iliyokusanywa kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na kila mmoja wao ni data ya kuaminika. Data iliyopatikana kutoka maktabani na nyanjani ilichanganuliwa kwa kufuata utaratibu na sheria za kiakademia na matokeo ya utafiti kuwasilishwa. Kwa ujumla ni kuwa, utafiti huu uliendeshwa kitaaluma jambo linalofanya utafiti huu kuwa na kila sababu ya kuaminika.

4.1 Maadili ya utafiti

Mchakato wote wa utafiti huu ulizingatia maadili yanayoongoza utafiti wa kitaaluma. Mtafiti alikusanya data kwa kudurusu vitabu, tahakiki na majarida mbalimbali ya kiakademia yaliyoandikwa na wataalamu mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili. Data iliyopatikana na ambayo ilisaidia katika utafiti huu ilinukuliwa na vilevile makala hayo kurejelewa ipasavyo ili kuzuia kosa la uchakachuzi. Mtafiti alipata cheti cha maadili kilichompa idhini ya kwenda nyanjani ili kutafuta data iliyohitajika katika utafiti huu. Mtafiti alifanya uteuzi wa kimakusudi na kuwateua wataalamu watano kama sampuli

ya wahojiwa. Mtafiti aliwatumia walengwa hao barua za ualishi kushiriki katika utafiti huu kwa hiari. Data iliyopatikana ilinukuliwa jinsi ilivyokuwa pasi na kuongeza au kupunguza chochote. Mtafiti alizingatia maadili ya utafiti katika uchanganuzi wa data ili kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti huu ni ya kuaminika.

4.2 Vikwazo vya utafiti

Katika harakati za kufanya utafiti huu mtafiti alikumbana na changamoto si haba.

Baadhi ya changamoto hizi ni kama ifuatavyo:

- Uhaba wa hela za kutosha. Mtafiti alikabiliwa na ukosefu wa hela za kutosha katika kuendesha utafiti huu hususan alipofikia sehemu ya kwenda nyanjani ambapo alitakiwa kusafiri hadi pale walengwa walipokuwa.
- Kuna mmoja wa walengwa ambao mtafiti alinuia kuwahoji ambaye ni Prof. Kyallo Wamitila lakini kutokana na sababu ambazo hazingeweza kuepukika mtafiti hakuweza kumhoji.
- Mtafiti alinuia kuandaa mahojiano ya kina zaidi na Mtaalamu Prof. Sheikh Ahmed Nabhany baada ya kuandaa mahojiano naye katika tangulizi-tafiti ya utafiti huu lakini kwa bahati mbaya aliaga dunia.

SURA YA NNE

UWASILISHI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.1 Kitangulizi

Katika sura hii vipengee vya maudhui na fani vinavyodhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga* vimetambuliwa, kuchanganuliwa na kuwekwa bayana. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Tafsiri ya Kiunguja ya *Utenzi wa Mwanamanga* ambayo imewekwa katika kiambatisho, maudhui na fani katika utenzi huu kwa ujumla. Vilevile katika sura hii, vipengee vya hisia zilizotumiwa na mtunzi katika *Utenzi wa Mwanamanga* pia vimechanganuliwa na kuwekwa bayana.

4.2 Maudhui

Maudhui huwa ni jumla ya mambo au masuala yanayoelezwa au yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Maudhui ya kazi yoyote ya fasihi huweza kujumuisha dhamira, mtazamo, ujumbe, maadili na falsafa ya mwandishi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kihemenitiki ambapo maudhui yafuatayo yaliweza kudhihirika:

4.2.1 Mapenzi

Mapenzi ni hali ya mvuto na upendo alio nao mtu kwa mwingine yaani hisia ya upendo aliyo nayo mtu moyoni mwake kuhusu mtu mwingine. Utenzi huu unadhihirisha mapenzi ya dhati aliyo nayo mtunzi kwa mkewe Mwanamanga. Utenzi mzima unamsifu mwanamke huyu kwa urembo wake, na jinsi mumewe alivyokuwa amefurahishwa naye katika maswala ya unyumba. Katika harakati za msanii kudhihirisha mapenzi yake kwa mke wake msanii anaanza kwa kuwaita wenyeji waende alipokuwa ili wamsaidie kutunga beti za kumsifia mkewe. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa msanii alimuenzi mkewe na alitaka pia jamii ifahamu kwani alimsifu pasi na woga au aibu yoyote kiungo baada ya kiungo akianza kichwani

akiteremka hadi kwenye nyayo. Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Kinene wa Mutiso ni kwamba ala ya mawasiliano ilikuwa ikipulizwa hapo awali endapo jambo la dharura lilikuwa limetokea na jamii ilipaswa kujuzwa ili ikusanyike pamoja. Ala iliyokuwa ikipulizwa katika kipindi hicho iliundwa kutokana na upembe wa jamusi (nyati). Jukumu hili lilikuwa la utawala. Mtunzi kutaka umma ujulishwe ili ukusanyike kisa na maana ni kushuhudia urembo wa mkewe na kukariri beti za kusifia urembo wa mkewe ni dhihirisho wazi la mapenzi ya hali ya juu ya mtunzi kwa mkewe. Hili linadhihirika katika beti zifuatao:

- | | | |
|-------------|------------------|---------------------------|
| Ubeti wa 2. | Pijiani p'embe | iliayo Yumbe |
| | Mwangi uwambe | kwa ya ndovu kanga. |
| Ubeti wa 3. | Vumi lende mbali | lamshe ahali |
| | Wake na wavuli | waye ng'a ng'a ng'a ng'a. |
| Ubeti wa 4. | Waye wakeleti | wambeja banati |
| | Watupe baiti | wamsifu Yanga. |

Kutokana na mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na Marehemu Mzee Sheikh Ahmed Nabhany mtafiti aliarifiwa kwamba utenzi huu ndiwo wa kwanza kabisa kuwahi kutungwa lengo kuu likiwa ni kumsifu mwanamke katika jamii za Uswahilini. Utenzi huu ni tofauti na tenzi nyingine za kale zilizotungwa katika kipindi cha kabla ya karne ya ishirini ambazo zilitungwa katika misingi ya dini au kuwasifu majagina au mashujaa wa kale. Marehemu alimwarifu mtafiti kwamba, jambo hilo lilikuwa ni ithibati tosha kuwa mtunzi huyo kuamua kumsifu mkewe ni dhihirisho la mapenzi kwa mkewe kwani sifa zote kwenye utenzi ni chanya na mahali pengine mtunzi alisifu kupita kiasi. Hili linadhihirika katika beti zifuatazo:

- | | | |
|-----------|----------------|-------------------|
| Ubeti 17. | Zakwe zitefute | zizidiye zote |
| | Ya mk'atekate | mafuta ya kwenga. |

Ubeti 23.	Kanwa kiradidi	nyoshi za mkadi
	Au za zabadi	yangawa na fungu.

4.2.2 Ushirikiano katika jamii

Ushirikiano ni hali au tendo la watu wawili au zaidi kuungana na kusaidiana katika shughuli fulani. Kulingana na utenzi huu ni kwamba ushirikiano wa hali ya juu katika jamii inayorejelewa na mtunzi unadhihirika. Maudhui haya yanathibitika kwa namna mtunzi anavyoanza utenzi wake. Mtunzi anaanza kwa kupiga pembe ya jamusi ili kuwaita waja wakusanyike na wamsaidie kutunga beti za kumsifu mkewe. Beti hizi zinadokeza kwamba kulikuwepeo na ushirikiano wa hali ya juu katika jamii inayorejelewa. Maudhui haya yanadhihirika katika beti zifuatazo:

Ubeti 1.	Pijiani basi	pembe ya jamusi
	Kwa cha mtutusi	au mwanananga.
Ubeti 2.	Pijiani p'embe	iliayo Yumbe
	Mwangi uwambe	kwa ya ndovu kanga.
Ubeti 3.	Vumi lende mbali	lamshe ahali
	Wake na wavuli	waye ng'a ng'a ng'a ng'a.
Ubeti 4.	Waye wakeleti	wambeja banati
	Watupe baiti	wamsifu Yanga.

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Kinene wa Mutiso mtafiti aliweza kufahamishwa kwamba katika jamii za Uswahilini umoja ni kitu walichokienzi sana kuanzia zama za kale. Wanajamii hao walikuwa wakiungana ili kutekeleza shughuli zozote muhimu walizokuwa wameitiwa kuzifanya. Beti hizi zinadhihirisha wazi kwamba kulikuwapo na ushirikiano miongoni mwa wanajamii wanaorejelewa na

mtunzi. Hii ndio sababu msanii aliamua kuwaalika wanajamii wenzake wajumuike naye katika mchakato wa kumtungia mkewe utenzi wa kumsifu.

4.2.3 Utamaduni

Utamaduni ni mila, desturi, asili, jadi, imani na itikadi za kundi la watu au jamii fulani. Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Sheikh Ahmed Nabhany ni kwamba katika utenzi huu inadhihirika kwamba njia mojawapo ya kale ambayo ilikuwa ikitumiwa kupitisha ujumbe fulani katika jamii za Uswahilini ilikuwa ni ya kutumia ala ambayo iliundwa kutokana na pembe ya jamusi au ndovu mchanga. Inadhihirika kuwa ala inapopulizwa na lile vumi lake kuwafikia wenyeji basi wenyeji hao wangeamka na kukimbilia kulikotokea vumi lile tena kwa haraka haraka. Inadhihirika kwamba vumi hilo liliashiria kuwa ni lazima kuwe na jambo la dharura. Maudhui haya yanadhihirika katika beti zifuatazo:

- | | | |
|----------|--------------------|---------------------------|
| Ubeti 1. | Pijiani basi | pembe ya jamusi |
| | Kwa cha mtutusi au | Mwananinga. |
| Ubeti 2. | Pijiani pembe | iliayo yumbe |
| | Mwangi uwambe | kwa ya ndovu kanga. |
| Ubeti 3. | Vumi lende mbali | lamshe ahali |
| | Wake na wavuli | waye ng'a ng'a ng'a ng'a. |

Shariff (1988) anaeleza kuwa mafumbo ni nadra sana kutumiwa katika utenzi. Kulingana na mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Rayya Timmamy ni kwamba mafumbo yalikuwa yakitumika sana katika jamii za Uswahilini wakati wa maongezi ya kawaida. Jambo hili lilikuwa likijitokeza zaidi wakati ambapo mtu alikuwa anapitisha ujumbe wenye mambo ya aibu au yanayovunja heshima kama vile yanayohusiana na maswala ya ngono. Katika utenzi huu tunagundua kuwa Fumo Liyongo hakuwa na budi ila

kutumia mafumbo alipokuwa amefika katika kusifu maungo ya mkewe ambayo mila yake haikumruhusu kutaja na kueleza waziwazi. Katika kuzungumza juu ya utupu wa mkewe na kumwingilia, alipiga mafumbo ya bahari, kutweka jahazi na kusafiri nalo na kupiga mzinga.

4.2.4 Dini

Dini ni imani inayohusiana na kuwapo kwa Mungu au miungu. Maudhui haya ya dini hayajitokezi bayana katika *Utenzi wa Mwanamanga* na hili ni kinyume na jinsi ilivyo katika tenzi zingine za kale kama vile: *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Al- Inkishafi* na *Utenzi wa Mwanakupona*. Maudhui ya dini yamedokezwa kwa kiduchu sana pale ambapo mtunzi anatumia jina ‘Wallahi’ na ‘Manani’ katika beti mbili za utenzi wake. Majina haya aliyotumia msanii kumrejelea Muumba hususan lile la ‘Wallahi’ linaashiria wazi kuwa mtunzi alikuwa mfwasi wa dini ya Kiislamu.

Shariff (keshatajwa) anaeleza kuhusu dini ya Fumo Liyongo. Anaeleza kuwa jambo alilotaka kuliweka dhahiri ni kwamba, mtu yeyote mwenye elimu ndogo tu ya Uislamu na Ukristo kuwa haikubaliwi Mkristo kuamini maneno ya Qurani na kuapia kwa kitabu hicho. Hata hivyo Muislamu anakubaliwa. Uislamu una heshima juu ya vitabu vyote walivyotaja, lakini hawawezi kusema Qur’ani inaheshimiwa na Wakristo kuwa ni maneno ya Mungu. Kwa hivyo, ilivyokuwa katika utungo wa Sayyid Adallah bin Ali bin Nasir, Fumo Liyongo anaapa kwa injili, Zaburi na Qur’ani ni dhahiri kuwa Sayyid Abdallah aliamini kuwa Fumo Liyongo ni Muislamu. Wakiangalia maneno ya Fumo Liyongo mwenyewe katika *Utenzi wa Mwanamanga* wa kuna ubeti wa 32 ambao anaapa hivi:

Ubeti 32.	Naapa Wallahi	asiyeshabihi
	Tanena swahihi	ya makomamanga.

Mtaalamu huyu anaeleza kuwa watungaji wa Kiswahili walipendelea pia kuanza kila jambo lao kwa mwenendo wa kidini, walipendelea sana kuanza beti zao hasa za tungo za kidini kwa majina ya Mungu na kumsalia Mtume na jamaa na masahaba zake na mengineyo ya kidini. Hata hivyo ni dhahiri kuwa, kuanza beti za tenzi kwa namna hii ni hiari ya mtungaji wala sio jambo la lazima wala la kimila lililokuwa halivunjiki. Ingawa ni dhahiri kuwa mara kwa mara Fumo Liyongo alitaja au kuapa kwa majina ya Mungu yanayotumiwa na Waislamu kama ilivyo katika ubeti wa 32 ambapo anaapa kwa ‘Wallahi’ utenzi huu hakuanza kwa majina ya Mungu. Tukichunguza tunagundua kuwa tenzi nyingi za kabla ya karne ya ishirini zinazoanzia kwa mtindo wa kidini huwa ni tenzi za kidini. Mambo ya dini yana mahali pake na ya kidunia yana mahali pake. Inabainika kuwa mara kwa mara mambo haya huingiliana; panapotokea haya mtungaji pia huamua jinsi ya kuanza utenzi wake. Beti za mwanzo katika baadhi ya tenzi kama vile *Utenzi wa Al-Inkishafi* aghalabu humjulisha msikilizaji si maudhui tu ya utungo bali hata hisi za mtungaji zimeelekea upande gani: za ucheshi, za mchezo, za kulalamika, za kuomboleza, na za furaha. *Utenzi wa Mwanamanga* wa Liyongo ni wa kumsifu mke wake Mwanamanga ndiposa alivyoanza namna alivyoanza badala ya kuanza kwa jina la Mungu na mengineyo ya kidini. Mtunzi wa *Utenzi wa Mwanamanga* hakulenga kupitisha ujumbe unaohusu masuala ya kidini.

4.2.5 Usanii wa mashairi

Usanii ni kazi au shughuli za sanaa kama uchoraji, uchongaji, ufumaji, uimbaji, ufinyanzi na utungaji. Usanii wa mashairi ni maudhui ambayo yanajitokeza katika jamii ya mtunzi wa *Utenzi wa Mwanamanga*. Inadhihirika kuwa jamii hii ni jamii iliyokuwa inaenzi sanaa ya ushairi na ndiposa mtunzi anapiga pembe ya nyati ili waja waje wamsaidie kutunga au kukariri beti za kumsifia mkewe. Beti hizi zinadhihirisha kuwa utunzi wa mashairi lilikuwa jambo la kawaida katika jamii ya mtunzi. Shariff

(keshatajwa) anaeleza kuwa katika sanaa zote kama vile uchongaji, uchoraji, ngoma na muziki hakuna sanaa ambayo Waswahili wengi wanaipenda kuliko sanaa ya tungo na kwamba Waswahili wenyewe wengi ni wasanii. Anaendelea kueleza kuwa hadhani kama kuna mahali pengine duniani ambapo wasemaji wa lugha fulani wanatumia sanaa ya tungo kwa kadiri zaidi ya waitumiavyo Waswahili. Maudhui haya usanii yanadhihirika zaidi katika beti zifuatazo:

Ubeti 4.	Waye wakeleti	wambeja banati
	Watupe baiti	wamsifu yanga.
Ubeti 5.	Tupane baiti	tukizitafiti
	Njema ziwe kiti	mbee tukitenga.
Ubeti 6.	Kisa kuziona	baiti kufana
	Yatupe kunena	zawe mwanamanga.
Ubeti 7.	Basi tawakifu	yasiwe marefu
	Swifa tuswanifu	zawe mwanamanga.

Beti hizi nne zinadhihirisha jinsi jamii hii ilivyoenzi utunzi wa mashairi. Beti hizi zinadokeza kuwa kutunga beti za mashairi lilikuwa jambo la kawaida kwa jamii hii tena lililothaminiwa sana na ndipo waja wanaitwa wafike kule alikokuwa msanii upesi upesi kutekeleza shughuli hiyo ya kutunga beti za kumsifu yanga. Maudhui haya pia yanadhihirika katika utenzi mzima kwani utenzi huu umedhihirisha ufundi wa hali ya juu wa mtunzi kwani mafumbo yalikuwa nadra sana kutumika katika utenzi lakini tunagundua kuwa Fumo Liyongo hakuwa na budi ila kutumia mafumbo alipokuwa amefikia katika kusifu maungo ya mkewe ambaye mila yake haikumruhusu kutaja na kueleza waziwazi. Hili linadhihirika katika ubeti 41-47. Fumo Liyongo ametumia ufundi wa lugha ya mafumbo wa hali ya juu.

4.2.6 Uzuri wa mwanamke

Uzuri ni hali ya kupendeza, hali ya kuvutia, haiba, wema na jamala. Uzuri pia unahusishwa na vipodozi kama vile manukato, marashi, uturi, udi, poda na wanja au rangi. Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Kinene wa Mutiso ni kwamba, maudhui haya ndiyo makuu katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Mtunzi wa utenzi huu alitunga utenzi huu kwa lengo la kumsifu mkewe kwa uzuri wake. Mtunzi anatumia mtindo wa safari ambapo anasifu kila kiungo kwa mtindo wa safari akianza kichwani akiteremka hadi nyayoni pasi kuacha kiungo chochote. Katika safari hii mtunzi anasafiri katika mwili wa mkewe akielezea kuanzia kichwani akisifu kila kiungo hadi kwenye maungo ya mkewe ambapo anaanza safari nyingine ya majini akitumia safina na baada ya kufikia kikomo anaendelea na safari ya kueleza kuhusu viungo vya mkewe hadi nyayoni. Safari hii inaleta muumano katika utenzi huu na kumpa mtunzi uwezo wa kueleza aliyotaka kikamilifu kwani safari hii ni ya kisitiari. Uzuri wa mwanamke unaodhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga* ni kwa mtazamo wa mwanamume. Utenzi mzima umesheheni msamiati ambao unahusishwa na sifa za mkewe. Utenzi mzima umesheheni sifa za Mwanamanga ambaye ni mke wa mtunzi. Zifuatazo ni baadhi ya beti kuthibitisha hali hii:

Ubeti 8.	Tawakanda kitwani	nduza sikiyani
	Hariri laini	zakwe nyee singa.
Ubeti 9.	Kitwache huramu	ni kama ruhamu
	Enga jaizimu	taole kuzinga.
Ubeti 11.	Uso wake mwana	napa siyaona
	Utengee sana	na kuta miyanga.

4.2.7 Kuheshimiana

Kuheshimu ni kumwonyesha mtu kuwa unamthamini au kumfanyia adabu. Pia, neno heshima linamaanisha kutukuza mtu kwa kumweka katika daraja la juu. Maudhui ya

kuheshimiana yamejitokeza katika utenzi huu kama ifuatavyo: Kwanza, msanii anamthamini sana mke wake na ndiyo maana katika kudhihirisha jambo hili anaamua kumtungia utenzi mzima akimsifu kwa uzuri wake. Kulingana na mahojiano kati ya mtafiti na Marehemu Prof. Ahmed Nabhany ni kwamba katika fasihi ya Kiswahili hususan katika jamii ya Waswahili hakuna utenzi wowote mwingine ambao uliwahi kutungwa kwa lengo la kumsifu mwanamke kando na *Utenzi wa Mwanamanga*. Hali hii inadhihirisha kuwa licha ya mtunzi kumpenda mkewe pia alimheshimu mno na ndio maana akamtungia utenzi huu ili kumdhihirishia heshima yake kwa mke wake. Heshima pia katika utenzi huu inadhihirika pale ambapo anatumia sitiari katika kuelezea maungo ya mkewe ili kuzuia kumvunjia heshima. Hili linadhihirika katika ubeti ufutao:

Ubeti 33.	Naapa siwenepo	zishuhudiyepo
	Matunda ya p'epo	yakwe mwana Manga.

Mtunzi amekwepa kuyataja waziwazi matiti ya mkewe bali anatumia jazanda na tasfida ili afikishe ujumbe wake bila kumvunjia mkewe heshima. Jambo hili pia limedhihirika katika ubeti wa 41 hadi 48 wakati mtunzi alipokuwa akizungumzia juu ya utupu wa mkewe na kumwingilia kwani alipiga mafumbo ya bahari, ya kutweka jahazi na kusafiri nalo na kufika pwani na kupiga mzinga. Beti zifuatazo zinadhihirisha jambo hili:

Ubeti 41.	Na yake safina	nalipoiyona
	Ni nyire si p'ana	iyaliye nyonga.
Ubeti 42.	K'akunduwa ndume	matanga yakwime
	Haswa la galime	shairaa kasonga.
Ubeti 43.	Kwalina mawingu	na pepo nyengwangu
	Zot'e zombo zangu	kazifungafunga.
Ubeti 44.	K'azungua bao	kapinga shikio

	Mbwene yavutao	mai henda Manga.
Ubeti 45.	Ngamani k'akingiya	ili kutungiya
	K'esa kuzengeya	ngama isikinga.
Ubeti 46.	Ikimikamika	ikinukanuka
	Vumba la kimaka	yake mwana Manga.
Ubeti 47.	Kangiya ngamani	k'enga uziwani
	Niyeyepo p'wani	k'apinga mzinga.

Jazanda hizi alizotumia mtunzi alifanya hivyo kwa kumheshimu mke wake. Heshima aliyokuwa nayo mtunzi haikumruhusu kueleza maungo, utupu wa mkewe na kitendo cha kumuingilia kwa lugha iliyo wazi. Hali hii inatokana na utamaduni wa mtunzi ambao haukuruhusu waja kuzungumzia waziwazi masuala ya maingiliano kati ya mwanamume na mwanamke.

4.2.8 Unyumba

Unyumba ni hali au tendo la kuishi pamoja kama mume na mke na vilevile neno hili pia linamaanisha ngono. Katika utenzi huu tunamuona msanii akieleza kuhusu mke wake akikisifu kila kiungo cha mwili wake kuanzia utosini akisafiri kuelekea miguuni. Anapofika chini ya tawangu anatumia jazanda ambapo anatweka safina ambayo anaitumia kusafiria. Kwa kutumia jazanda, msanii anelezea kuhusu uke wa mkewe na vilevile kuhusu kufanya naye mapenzi. Maudhui haya yanadhihirika katika ubeti wa 41-47.

Ubeti 41.	Na yake safina	nalipoiyona
	Ni nyire si p'ana	iyaliye nyonga.
Ubeti 42.	K'akunduwa ndume	matanga yakwime

	Haswa la galime	shairaa kasonga.
Ubeti 43.	Kwalina mawingu	na pepo nyengwangu
	Zot'e zombo zangu	kazifungafunga.
Ubeti 44.	K'azungua bao	kapinga shikio
	Mbwene yavutao	mai henda Manga.
Ubeti 45.	Ngamani k'akingiya	ili kutungiya
	K'esa kuzengeya	ngama isikinga.
Ubeti 46.	Ikimikamika	ikinukanuka
	Vumba la kimaka	yake mwana Manga.
Ubeti 47.	Kangiya ngamani	k'enga uziwani
	Niyeyepo p'wani	k'apinga mzinga.

Katika beti hizi msanii anaelezea kuhusu utupu na maungo ya mkewe na tendo la ndoa kati yake na mke wake. Msanii anaeleza hisia zake kwa kutumia jazanda ya safari ya majini ambapo inabainika wazi kuwa mtunzi alifurahia tendo la ndoa kati yake na mke wake.

4.2.9 Ushirikina

Ushirikina ni tabia ya kuamini mambo ya uchawi. Katika utenzi huu maudhui ya ushirikina yamejitokeza lakini kwa kiduchu tu katika ubeti ufuatao:

Ubeti 48.	Niinusheepo	kafanya kitapo
	K'asabibu papo	kivuza waganga.

Msanii anadhihirisha ushrikina kwani aneleza kuwa baada ya kufanya mapenzi na mke wake alikaa hapo kwa kitambo kana kwamba kapagawa na pepo. Ikalazimu atafutiwe waganga waje wamuague.

4.2.10 Nafasi ya mwanamke katika jamii

Maudhui haya yanakaribiana na yale ya unyumba kwa namna fulani. Katika jamii ya msanii inadhihirika kwamba hii ni jamii inayomuenzi na kumheshimu sana mwanamke. Hili linabainika kwani shairi lote limetungwa kwa madhumuni ya kumsifu mwanamke. Katika utenzi huu imejitokeza bayana kuwa mwanamke ana jukumu la kumtimizia mwanamume haja zake za kimapenzi. Hili limejitokeza katika beti za 41-47. Mwanamke katika utenzi huu amesawiriwa kama kiumbe cha kumfurahisha mwanamume kutokana na jinsi alivyoubwa. Mwanamume anafurahia jinsi mwanamke alivyo na ndiposa anastaajabia, kumpongeza na kumsifu.

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Kinene wa Mutiso ni kwamba, mwanamume anafurahishwa sana na jinsi mwanamke alivyoubwa na kubarikiwa kwa namna nyingi na vitu vingi ambavyo mwanamume hanavyo. Mtafiti alifafanuliwa kuwa urembo ni kitu ambacho wanawake wanakienzi mno kuanzia jadi hata mpaka jamii ya kisasa kwani wanawake wote wanathamini sana kupendeza machoni pa wanaume na wanaamini kuwa hilo ni jukumu lao. Hii ndiyo maana utawapata wengi wakijirembesha ili waweze kutekeleza jukumu hilo kikamilifu.

Kutokana na mahojiano kati ya Prof. Nabhany na mtafiti ni kwamba urembo wa mwanamke ulithaminiwa sana katika enzi za kale katika jamii za Uswahilini. Wanawake walisawiriwa kama mapambo kwa wanaume. Na kulikuwepo mapambo na vipodozi aina tofauti-tofauti ambavyo vilitumiwa na wanawake katika kujirembesha. Beti zifuatazo zinadhihirisha hali hii:

Ubeti 13	Ni nyeusi mno	zizidiye wino
	Zitolee k'ono	na tandu za Mnga.
Ubeti 15	P'uwaye ajabu	zifungo huribu
	Ni sita hisabu	mwenye kuziwanga.

Prof. Nabhany alimjuza mtafiti kwamba katika kipindi cha kabla ya karne ya 12 Waswahili walikuwa hawana stadi ya kuandika na stadi hiyo ililetwa na Waarabu ambao walianza kuzuru katika pwani ya Afrika Mashariki katika karne ya 12. Walianza kuandika lugha ya Kiswahili wakitumia hati za Kiarabu. Wino unaorejelewa katika utenzi huu unarejelea wino ambao ulitumika katika kupambia wanawake na kuwachora miili yao bali sio ule wa kuandikia. Kutokana na mahojiano kati ya Bw. Mohamed Karama na Mtafiti ni kuwa, zifungo zinazorejelewa katika ubeti huu ni kwamba katika muktadha wa kipindi cha kihistoria ulipoandikwa utenzi huu ni vipuli ambavyo vilivaliwa kwenye pua na wanawake kama aina ya pambo.

4.2.11 Ubaharia

Ubaharia ni taaluma ambayo huhusisha vyombo vya majini kama vile meli, majahazi na madau. Maudhui ya ubaharia yamejitokeza kwa kiduchu katika utenzi pale ambapo tunaona mtunzi anaamua kutumia msamiati wa ubaharia katika kuulezea uchi wa mkewe na kitendo cha ndoa kati yake na mke wake. Msamiati huu wa ubaharia uliotumika kwenye utenzi unadokeza wazi kuwa kulikuwa na shughuli ya ubaharia ambayo mtunzi pia alikuwa akijishughulisha nayo. Sababu hapa ni kwamba, mtunzi anaeleza kindakindaki hatua zote za kutweka safina na kutayarisha matanga na kusafiri nayo huku akieleza kuhusu mandhari ya bahari. Maudhui haya yamejitokeza katika beti zifuatazo:

Ubeti 42.	K'akunduwa ndume	matanga yakwime
	Haswa la galime	shairaa kasonga.
Ubeti 44.	K'azungua bao	kapinga shikio
	Mbwene yavutao	mai henda Manga.

4.2.12 Wasifu wa mwanamke kwa mtazamo wa mwanamume

Wasifu ni ufafanuzi au taarifa ya maisha ya mtu kuhusu mienendo, hulka na tabia zake kwa ujumla. Wasifu ulioko katika utenzi huu ni kwa mtazamo wa mwanamume. Mtunzi ametumia sitiari mbalimbali kuonyesha jinsi mwanamke alivyobarikiwa kwa mambo mengi ambayo mwanamume hanayo. Utenzi huu kwa ujumla ni kwamba ulitungwa kwa dhamira ya kumsifu mwanamke ambaye alikuwa mke wa mtunzi. Fumo Liyongo alitungia mkewe Mwanamanga utenzi huu. Ameanzia kichwani akikisifu kila kiungo cha mwili wa mke wake akiteremka polepole kwa mtindo wa safari. Anapofika katika maungo ya mkewe anapachika jazanda la safari ya majini ambapo anatomia safina kusafiria akitalii na kuelezea kuhusu uchi wa mkewe na kumingilia kisha anaendelea na safari yake hadi kwenye nyayo za mkewe. Kwa ujumla urembo wa Mwanamanga ndiwo unaosifiwa katika beti zote kwenye *Utenzi wa Mwanamanga*. Beti zifuatazo zinadhihirisha maudhui haya:

Ubeti 8.	Takwanda kitwani	nduza sikiyani
	Hariri laini	zakwe nyee singa.
Ubeti 11.	Uso wake mwana	napa siyaona
	Utengene sana	na kuta miyanga.
Ubeti 18.	Miyomo myembamba	asipoifumba
	Atakapokwamba	helewa muyinga.

4.3 Fani

Kwa ujumla fani ni mbinu za lugha na za kimtindo ambazo msanii huzitumia katika kupanga mawazo yake ili kuhakikisha kuwa lugha anayoitumia ina mvuto wa kisanaa na inayoeleza mawazo, dhamira na hisia zake kwa ufasaha na kueleweka vizuri. Katika

utafiti huu vipengele vya fani vilivyochunguzwa ni: matumizi ya lugha, muundo, mtindo na wahusika.

4.3.1 Matumizi ya lugha

Fasihi ni sanaa inayowasilisha maudhui yake kwa kutumia lugha. Katika utanzu wa riwaya msanii huwaumba wahusika wanaoendeleza matendo fulani ambayo msimulizi ndiyo hutumia lugha katika kuyasimulia. Lugha anyaoitumia msimulizi huwa lugha teule iliyosheheni vipengee vya fani na kuifanya kuwa na mvuto mkubwa wa kisanaa. Ushairi nao hutumia lugha yenye mpangilio maalumu wa maneno yaliyoteuliwa ili kuwasilisha ujumbe wake. Takriban kila kijelezi hulenga kueleza dhana inayohusiana na ushairi kimetilia mkazo umuhimu wa lugha iliyoteuliwa tena ya mkato. Mwananadharia Jakobson (katika Eagleton, 1988) amewahi kuifafanua lugha ya ushairi kama “nguvu za kimabavu” zinazotendewa lugha za kawaida. Anavyosema Jakobson lugha ya kishairi hujivimbisha kiasi cha kuvuta nadhari za wasomaji au wasikilizaji wa tungo hizo. Kwa sababu hiyo, ushairi una uwezo wa kuzungumza mambo chungu nzima kwa muhtasari kuliko maelezo yanayotolewa na waandishi wa tanzu nyinginezo za fasihi kama vile: riwaya, tamthilia na hadithi fupi.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa lugha ndiyo nyenzo kuu ya kazi ya fasihi. Dhamira na maudhui ya kazi ya kifasihi hayawezi kuwasilishwa na kuwafikia wasomaji bila kuwako kwa lugha. Uchunguzi wa matumizi ya lugha basi ni muhimu katika uhakiki wa fasihi. Anaendelea kueleza kuwa katika kuchunguza matumizi ya lugha mambo ambayo huchunguzwa ni: tamathali za usemi, uteuzi na mpangilio wa maneno, sajili za lugha kutegemea mazingira na hali tofauti-tofauti, matumizi ya nahau na misemo mbalimbali.

4.3.2 Tamathali za usemi

Kulingana na Msokile (1993) anafafanua kuwa tamathali za usemi ni maneno, nahau, au semi ambazo hutumiwa na waandishi wa fasihi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na pengine sauti katika maandishi hayo. Tamathali za usemi hutumiwa pia kuipamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha naye Mbatiah (2001) anafafanua dhana ya tamathali ya usemi kama, ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kahigi na Mulokozi (1982) wanazieleza tamathali za usemi kuwa ni: "...vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti. Ni usemi wenye kupanua, kupuuzwa au kubadilisha maana dhahiri za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi kuchelewesha uelewa wa ujumbe alioufumbata katika kazi yake ya kisanaa." Kwa mujibu wa utafiti huu tamathali za usemi zifuatazo ziliweza kudhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga*:

4.3.2.1 Tashbihi

Arege (2013) anafafanua dhana tashbihi kama mbinu ya lugha inayolinganisha vitu viwili au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha ambayo baadhi ni: kama, mithili ya, sawa na, na ja. Mbinu ya tashbihi imejitokeza katika *Utenzi wa Mwanamanga* kama ifuatavyo:

Ubeti 9.	Kitwache huramu	ni kama ruhamu
	Enga jaizimu	taole kuzinga.
Ubeti 10.	Yakwe masikio	apulikiayo
	Yatendele tao	kama kombe nanga.
Ubeti 12.	Nshize zifene	Nta zilingane

	Shina lifungene	kama lalofungwa.
Ubeti 25.	Shingoye ndefu	muwandi sharifu
	Ipambiwe kufu	kama za kutunga.
Ubeti 27.	Mafuzi kadiri	hayakudhihiri
	Kama bilauri	taole kuzinga.
Ubeti 29.	Nyaaze launi	kama marijani
	Napa hutamani	mwenye kuziwanga.

Mbinu hii katika utenzi inamfanya msomaji kupata picha halisi ya viungo vya mwanamke anayeelezewa kwenye utenzi kwa kuvilinganisha na vitu vinavyofananishwa na kila kiungo husika. Kwa namna hii ujumbe wa msanii unakuwa na nguvu zaidi na wa kusiona.

4.3.2.2 Takriri

Msokile (keshatajwa) anaeleza takriri kuwa ni marudiorudio ya neno, sauti, herufi au wazo katika kazi ya sanaa ya kifasihi naye Wamitila (2002), anaeleza kuwa dhamira na maudhui ya kazi ya kifasihi hukuzwa kwa njia mbalimbali mojawapo kubwa ikiwa ni urudiaji ambao unaweza kujitokeza pia kwa mageuzo. Urudiaji unaweza kutokeza katika kazi ya kifasihi katika viwango mbalimbali. Inawezekana ukawa wa sauti, mizani, neno, kirai, kishazi, msitari au muundo wa kisintaksia. Katika kiwango cha sauti kuna matumizi ya urudiaji katika takriri-irabu na takriri-konsonanti. Katika mashairi mapokeo urudiaji unaojitokeza huwa katika kiwango cha kina na mizani na kwenye kiitikio au kibwagizo. Kibwagizo cha shairi mapokeo hukariri ujumbe muhimu wa shairi. Katika mashairi mengi ya muundo huu, mshororo wa mwisho hukariri dhamira ya shairi zima au ubeti unaohusika. Kwa njia hii mshororo huo au kipokeo hicho huyachimuza maudhui au dhamira ya utungo unaohusika na pia huchangia katika

kuzua usambamba wa kimaudhui. Urudiaji una nafasi kubwa katika kuimarisha wizani wa kazi ya kifasihi. Hata hivyo haitarajiwi urudiaji uwe uleule wa maneno yale yale pekee. Lazima pawepo na mageuzo katika urudiaji huo. Mageuzo hayo yanaweza kuwa ya matumizi ya visawe, miundo badalia na minyambuliko ya maneno.

Urudiaji katika *Utenzi wa Mwanamanga* umetokea katika viwango vya sauti, neno na kirai au kipande cha mshororo. Kina ‘nga’ kimerudiwa katika mwisho wa beti zote kwenye utenzi. Kina hiki kinajenga urari na wizani katika utenzi mzima. Kuna urudiaji katika kiwango cha neno kwenye utenzi. Yapo maneno ambayo mtunzi ameyarudia ili kutoa msisitizo na vilevile kujenga wizani na urari wa vina kwenye utenzi. Urudiaji wa viwango mbalimbali umejitokeza katika beti zifuatazo: Urudiaji wa kiwango cha sauti na neno.

Ubeti 24.	Shani ni kidevu	si k’ungu piyavu
	Ni k’ungu tekevu	k’ungu kungumanga.
Ubeti 35.	Ziwavuze zana	ziwavuze nana
	Hutisha kuvina	mwenye kumsinga.

Urudiaji wa kiwango cha kipande.

Ubeti 6.	Kisa kuziona	baiti kufana
	Yatupe kunena	zawe Mwanamanga.
Ubeti 7.	Basi t’awakifu	yasiwe marefu
	Swifa tuswanifu	zawe Mwanamanga.
Ubeti 15.	P’uwaye ajabu	zifungo huribu
	Ni sita hisabu	mwenye kuziwanga.

Ubeti 16.	Sitaajabuni Hata ishirini	kuliko manani zifungo hupanga.
Ubeti 45.	Ngamani ka'kingiya Kesa kuzengeya	ili kutungiya ngama isikinga.
Ubeti 47.	Ka'ngiya ngamani Niyeyepo pwani	ke'nga uziwani kapinga mzinga.

Katika *Utenzi wa Mwanamanga* matumizi ya takriri yametumika kususitiza ujumbe wa mwandishi, kuleta urari wa vina na mdundo ulio na utamu wa kishairi. Takriri katika beti 45 na 47 inajenga msisitizo na kudokeza maana ya ujumbe unaopitishwa kwa njia ya kisitari. Takriri pia katika *Utenzi wa Mwanamanga* imetumika kuipamba lugha. Marudiorudio ya maneno na mchezo wa maneno umetumika kuupamba utenzi huu na kuwafurahisha wasomaji kwa namna ya kipekee.

4.3.2.3 Chuku

Wamitila (2003) anaeleza kwamba chuku hurejelea hali ya msanii kukuza sifa fulani kupita kiasi. Kukuzwa huko huwa kwa udogo au ukubwa. Nia hasa ya kuitumia chuku ni kulifanya jambo fulani litokeze kwa uwazi zaidi, kuikuza sifa fulani na kumfikirisha msomaji kwa kuuona uzito uliopo naye Arege (2013) anaeleza dhana ya chuku kama ni hali ya kutumia maneno yaliyotiliwa chumvi ili kususitiza ujumbe fulani au kusifia kitu fulani. Mbinu ya chuku katika *Utenzi wa Mwanamanga* imetumika kama ifuatavyo:

Ubeti 11.	Uso wake mwana Utengee sana	naapa siyaona na kuta miyanga.
Ubeti 13.	Ni nyeusi mno (nshize) Zitolee k'ono	zizidiye wino na tandu za mnga.

Ubeti 14.	Mato avikapo	haswa avumapo
	Mtu akiwapo	hutesha kiyenga.
Ubeti 16.	Sitaajabuni	kuliko manani
	Hata ishirini	zifungo hupanga.
Ubeti 18.	Miyomo myembemba	asipoifumba
	Atakapokwamba	helewa muyinga.
Ubeti 23.	Kanwa kiradidi	nyoshi za mkadi
	Au za zabadi	yangawa na fungu.
Ubeti 31.	Huleta harufu (makwapaye)	zaidi ya ufu
	Au matukufu	mafuta ya manga.
Ubeti 34.	Yakiwa nguwoni (matunda peponi)	hutisha uyuni
	Yawapo bayani	aqili hutanga.

4.3.2.4 Tabaini

Mbatiah (2001) anafanua istilahi tabaini kama tamathali ya usemi ambayo ina mtwezo ambapo badala ya kutumia kauli chanya kikanushi kinatumiwa kutwezea (vunjia mtu heshima au aibisha) kitu au hali fulani naye Msokile (1993) anaelezea dhana ya tabaini akidai kuwa wakati mwingine waandishi hutumia sentensi ambazo ukiziona zinaonyesha ukinzano. Aina hii ya maelezo huelezea kweli inayoonekana kama uongo, yaani neno linaloonekana kama kinyume kumbe ni sahihi. Kulingana na mtafiti ni kwamba, tabaini ni mtindo wa kutumia lugha ambapo msemaji husisitiza kauli au ukweli fulani kwa kutumia maneno yenye ukinzani. Neno ambalo hutumika mara nyingi katika kudhihirisha matumizi ya mbinu hii ni 'si'. Mbinu hii katika *Utenzi wa Mwanamanga* imejitokeza katika beti zifuatazo:

Ubeti 20.	Si ya ahadharu	si ya ahamaru
	Hufana na nuru	iwaayo Manga.

Ubeti 21.	Si ya mkakasi	si rangi nyeusi
	Ni kufana basi	kwa wanda wa Manga.

4.3.2.5 Istiari

Mbuvi (2013) anafafanua istiari kama mbinu ya kulinganisha kitu na kingine, chenye sifa sawa nacho, moja kwa moja kama vile: jambo hilo ni nanga, kumaanisha ni zito. Mtaalamu huyu anadai kuwa zipo pia sitiari ambazo hazichukui muundo huu. Hizo hutaja neno tu bila kulihusisha na kitu. Kwa mfano, blanketi la giza liliyagubika maisha yangu, kumaanisha matatizo yaliandama maisha yangu. Mbinu ya istiari katika *Utenzi wa Mwanamanga* imejitokeza katika beti zifuatazo:

Ubeti 38.	Kitovu ni kuka	kezo la kimaka
	Mwenye kumnuka	puwa damu yenga.
Ubeti 37.	Matumbo makuto	ndiya ya masito
	Kitovu ni kito	huvuta kafunga.
Ubeti 49.	Ziweoze ndiya	ni tako la siwa
	Watu hula ngowa	na kumzimanga.
Ubeti 50.	Maondo ni swifa	yana maarifa
	Henda kwa miswafa	na kuiviringa.
Ubeti 52.	Nyaoze ashashi	vaole ni koshi
	Kazi ya naqishi	ni kazi Manga.

Katika utenzi huu istiari hizi zimetumiwa kujenga picha ya mhusika Mwanamanga hivyo basi ujumbe wa msanii unakuwa na nguvu zaidi ya kisanii.

4.3.2.6 Matumizi ya taswira

Wamitila (2003) anaeleza kuwa taswira ni picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Wamitila anauliza iwapo picha hizo hutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi anazotumia? Mtaalamu huyu anafafanua kuwa kuna taswira zinazotokana na maelezo na ambazo hazina maana nyingine ya ziada. Hizi hujulikana kama taswira za kimaelezo. Zipo taswira ambazo huwa na maana nyingine ya ziada (yaani sio ile picha tu, kuna ujumbe wa ziada). Hizi nazo huitwa taswira za kiishara. Wamitila anaendelea kueleza kuwa waja wanavyofahamu ni kwamba binadamu ana hisia mbalimbali. Picha zinazopatikana katika kazi za kifasihi hulenga hisia hizo tofauti tofauti. Kuna picha zinazolenga kuchochea kutazama, kunusa, kuonja na kusikia. Kutokana na msingi huu, tunapata aina mbalimbali za taswira. Hizi ni:

- i. Taswira za uoni: Picha inayojengwa inalenga mtazamo wa macho.
- ii. Taswira za mnuso/harufu: Picha zinazojengwa zinalenga viungo vya harufu. Kwa mfano, katika utungo maarufu wa *Al-Inkishafi*, mshairi anapolinganisha dunia na mzoga wa mnyama, sitiari anayoitumia inasaidia kujenga picha ya uoni (kuuona mzoga uliopo) pamoja na mnuso (kwa kuwa sura ya mzoga huchochea pia harufu mbaya inayohusiana nao).
- iii. Taswira za mguso: Huleta picha ya hali ya kugusa kitu au vitu fulani kugusana.
- iv. Taswira za mwonjo: Hizi hulenga kwenye hisia za kuonja; kwa mfano kama maelezo yanayohusiana na chakula.
- v. Taswira ya usikivu: Msanii analenga hisia za kusikia kwa kujenga picha zinazohusiana na sauti. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Al-Inkishafi* ambapo mshairi anasema kuwa, mtu akienda walikoishi matajiri wa Pate na kuita, hajibiwi isipokuwa na mwangwi wa sauti yake.
- vi. Taswira za mwendo: Hizi ni zile zinazotuletea picha ya mwendo.

- vii. Taswira za joto: Picha zinazohusiana na joto humjia msomaji.

4.3.2.6.1 Matumizi ya hisia

Msingi wa kutumia taswira (na umuhimu wake pia) ni kuweza kuchochea hisia mbalimbali za msomaji. Kwa njia hii mwandishi anaupitisha ujumbe wake kwa nguvu zaidi na kazi yake inakuwa na mvuto mkubwa wa kisanaa.

Kulingana na utafiti huu ni kwamba mojawapo ya misingi ya nadharia ya kihemenitiki inayoongoza utafiti huu ni kwamba, inahusisha dhana ya kujitambulisha na ujitambulishaji ambapo ina maana kuwa msomaji au mfasiri wa kazi ya kifasihi anapaswa kujitahidi awezavyo kujitambulisha kihisia na mwandishi wa kazi hiyo. Katika uchunguzi wa mtafiti, aligundua kuwa msanii wa utenzi huu amefaulu kuchochea hisia zote za msomaji katika utenzi wake. Msomaji wa utenzi huu anapokuwa katika mchakato wa kuusoma anapata mvuto wa kisanaa wa namna ya kipekee kwani hisia zake zote zinachochewa kiasi kwamba anaweza kujitambulisha kihisia na mwandishi wa utenzi huu. Msomaji wa utenzi huu anapokamilisha usomaji wake hubakia na athari mbalimbali katika hisia zake.

Msanii wa utenzi huu amefaulu kunata hisia mbalimbali za msomaji kwa kutumia mbinu ya taswira kama kifaa muhimu. Msanii wa utenzi huu ametumia mbinu ya taswira na aina zake ili kuweza kuibua na kuchochea hisia mbalimbali za msomaji. Msanii amefanya hivi ili kuifanya kazi yake kuwa na mvuto na mnato mkubwa wa kisanaa ili kuweza kuupitisha ujumbe wake kwa nguvu zaidi na vilevile kudhihirisha ubingwa wake katika sanaa ya ushairi kwa ujumla.

Msanii ameitumia mbinu ya taswira na kuweza kumfanya msomaji kujenga picha mbalimbali katika akili yake ambazo zinaibua na kuchochea hisia mbalimbali za msomaji. Aina mbalimbali za hisia zimejitokeza katika *Utenzi wa Mwanamanga* kama ifuatavyo:

- i. Kuona. Hisia hii imejengwa kwa kutumia taswira ya uoni ambayo hunuia kujenga picha inayolenga mtazamo wa macho. Mtunzi hutoa maelezo ambayo humfanya msomaji kujijengea picha ya akili na kuona kile kinachozungumziwa katika akili yake. Hisia hii inachochewa kwa msomaji wa utenzi huu katika beti zifuatazo:

Ubeti 6.	Kisa kuziona	baiti kufana
	Yatupe kunena	zawe mwana Manga.
Ubeti 8.	Takwanda kitwani	nduza sikiyani
	Hariri laini	zakwe nyee singa.
Ubeti 10.	Yakwe masikio	apulikiayo
	Yatendele tao	kama kombe nanga.
Ubeti 12.	Nshize zifene	nta zilingane
	Shina lifungene	kama lalofungwa.
Ubeti 13.	Ni nyeusi mno	zizidiye wino
	Zitolee k'ono	na tandu za mnga.
Ubeti 29.	Nyaaze launi	kama marijani
	Napa hutamani	mwenye kuziwenga.

Kwa kutumia taswira ya uoni msanii ameiteka hisia ya msomaji ya kuona kwa kumjengea picha ambayo inamfanya msomaji kumwona yule mhusika Mwanamanga katika akili yake jinsi umbo lake linavyoelezwa. Picha hii inamleta mhusika anayesifiwa karibu na msomaji kana kwamba mhusika yule yupo pale pale karibu na msomaji bali yumo tu akilini mwake.

ii. Kunusa. Mtunzi amechochea hisia hii kwa kutumia taswira ya harufu ili kujenga picha akilini mwa msomaji zinazolenga viungo vya harufu. Hisia inayoibuliwa na aina hii ya taswira ni kunusa. Neno kunusa lina maana ya kuvuta hewa kupitia puani ili kutambua harufu au mnuko. Hisia ya kunusa inachochewa kwa msomaji wa *Utenzi wa Mwanamanga* kupitia beti zifuatazo:

Ubeti 23.	Kanwa kiradidi	nyoshi za mkadi
	Au za zabadi	ya ngawa na fungu.
Ubeti 30.	Makwapaye nduza	mato kituliza
	Mbwene ukimeza	mti mpakanga.
Ubeti 31.	Huleta harufu	zaidi ya ufu
	Au matukufu	mafuta ya Manga.
Ubeti 38.	Kitovu ni kuka	kezo la Kimaka
	Mwenye kumnuka	pua damu yenga.
Ubeti 46.	Ikimikamika	ikinukanuka
	Vumba la kimaka	yake Mwanamanga.

Msanii ametumia maneno kama vile: nyoshi za mkadi, zabadi, ufu, ikinukanuka na vumba la Kimaka katika kumwelezea mke wake. Maneno haya yanamfanya msomaji kujijengea picha akilini mwake ambayo inachochea neva za harufu hivyo basi kuibua hisia ya kunusa. Msomaji anapata harufu ya vitu vinavyorejelewa kwenye utenzi.

iii. Kugusa. Hisia hii imejengwa kwa kutumia taswira ya mguso amabyo huleta picha ya hali ya kugusa kitu au vitu fulani kugusana. Taswira hii inaibua hisia ya mguso kwa msomaji. Hisia ya mguso ya msomaji inachochewa katika beti zifuatazo:

Ubeti wa 35.	Ziwavuze zana	ziwavuze nana
	Hutisha kuvina	mwenye kumsinga.

Ubeti wa 39.	Tawangu ni nzito	kwa yuu la peto
	Tena lina keto	pesi la kuzinga.
Ubeti wa 40.	Wema wa duara	angaliya dira
	Usipoidara	yendapo kuzinga.
Ubeti wa 45.	Ngamani k'akingiya	ili kutungiya
	Kesa kuzengeya	ngama isikinga.
Ubeti wa 47.	Kangiya ngamani	keng'a uziwani
	Niyeyepo pwani	kapinga mzinga.

Msanii ametumia mbinu ya taswira ya mguso ambapo taswira hii imebeba ujumbe mzito wa kisitiari. Tamathali hizi mbili zimemwezesha msomaji kusafiri na msanii katika safari ya ubunaji ambapo hisia ya mguso inachochewa vilivyo na kufungua milango ya msomaji ya kuhisi mguso wa namna fulani.

- iv. Kuonja. Hisia hii huibuliwa na matumizi ya taswira ya mwonjo ambayo hulenga kwenye hisia za kuonja kwa mfano kama maelezo ya chakula. Aina hii ya taswira huibua hisia ya mwonjo. Kuonja ni kitendo cha kutia kitu mdomoni ili kujua ladha yake. Hisia ya mwonjo imechochewa kwa msomaji kupitia beti zifuatazo katika *Utenzi wa Mwanamanga*:

Ubeti 24.	Shani ni kidevu	si k'ungu piyavu
	Ni kungu tekevu	k'ungu k'ungumanga.
Ubeti 32.	Naapa wallahi	asiyeshabihi
	Tanena swahihi	ya makomamanga.
Ubeti 33.	Naapa siwenepo	zishuhudiyepo
	Matunda ya pepo	yakwe mwanamanga.

Msanii ananasa hisia ya mwonjo ya msomaji kwa kutaja matunda kama kungu na makomamanga ambayo humfanya msomaji kujenga picha ya matunda yale katika akili

yake ambayo huchochea hisia ya mwonjo na kumfanya msomaji kupata ladha mbalimbali za matunda yale katika akili yake.

- v. Kusikia. Msanii analenga hisia za kusikia kwa kujenga picha zinazohusiana na sauti. Taswira ya usikizi ndio hutumiwa kuibua hisia hii. Kusikia ni kupokea sauti au mngurumo kupitia masikio. Beti zifuatazo zinachochea hisia ya kusikia katika *Utenzi wa Mwanamanga*:

Ubeti 1.	Pijiani basi	penbe ya jamusi
	Kwa cha mtutusi	au mwanananga.
Ubeti 2.	Pijiani p'embe	iliayo yumbe
	Mwangi uwambe	kwa ya ndovu kanga.
Ubeti 3.	Vumi lende mbali	lamshe ahali
	Wake na wavuli	waye ng'a ng'a ng'a ng'a.
Ubeti 4.	Waye wakeleti	wambeja banati
	Watupe baiti	wamsifu yanga.
Ubeti 5.	Tupane baiti	tukizitafiti
	Njema ziwe kiti	mbee tukitenga.
Ubeti 18.	Miyomo myembamba asipoifumba	
	Atakapokwamba	helewa muyinga.
Ubeti 49.	Ziweoze ndiya	ni tako la siwa
	Watu hula ngowa	na kumzimanga.

Msanii amefaulu kutumia taswira ya usikivu na kumjengea picha akilini msomaji ambayo inachochea milango ya upokeaji wa sauti hivyo basi kumfanya msomaji kusikia kile kinachozungumzwa katika shairi. Msanii ametumia msamiati ambao unahusika na hisia ya usikivu au utoaji wa sauti kama vile alivyomjengea msomaji

picha ya ile ya ala ya mawasiliano ambayo ni upembe wa jamusi/mbogo ukipulizwa ili kutoa vumi ambalo linasikika akilini mwake na ambalo vumi hilo linanuiwa kwenda mbali ili liamshe wenyeji ambao ni wake na waume ambao wangekwenda pale alipokuwa msimulizi ili wajumuike naye katika kutoa na kukariri beti za kumwezesha msomaji kumsifu mkewe.

4.3.2.7 Matumizi ya lugha fiche

Shariff (1988) anaeleza kwa muhtasari kuhusu matumizi ya mafumbo na misemo katika tungo za Kiswahili. Anaeleza kuwa, katika Kiswahili cha kawaida na tungo zake kuna namna tatu ya matumizi ya lugha zinazojitokeza zaidi. Kwanza kuna utumiaji wa lugha iliyo wazi, pili kuna, utumiaji wa misemo na tatu kuna lugha ya kimapumbo. Waswahili ni katika watu wanaopenda sana kutumia misemo na mafumbo katika mazungumzo yao. Mtaalamu huyu anazungumzia kuhusu matumizi ya mafumbo na misemo katika mazungumzo ya kawaida na katika tungo kama ifuatavyo:

4.3.2.7.1 Misemo

Mtaalamu huyu anadai kwamba misemo mingi ya lugha hii hutokana na hekima na wajuzi wenye busara na huwa imepokewa kutokana na wavyele kama lugha yenyewe, kwa jumla ilivyo. Anaendelea kudai kuwa anaweza kusema kuwa baadhi ya misemo ya zamani huenda ikasahauliwa, lakini ni kweli pia kuwa misemo mipya hutungwa na wasemaji wa lugha walio hai. Matumizi ya misemo katika *Utenzi wa Mwanamanga* yamejitokeza katika ubeti ufuatao:

Ubeti wa 49. Ziweoze ndiya ni tako la siwa,
 Watu hula ngowa na kumzimanga.

Watu hula ngowa na kumzimanga ni msemu unaomaanisha watu humuonea wivu, humsengenya na kumlaani.

4.3.2.7.2 Mafumbo

Mafumbo hutumika sana katika tungo za Kiswahili, hasa bahari ya wimbo na ushairi. Si aghalabu kuona mafumbo yakitumika katika bahari ya utenzi na bahari nyinginezo. Mtaalamu huyu pia anaeleza ni kwa nini kuona mafumbo yakitumiwa sana katika bahari ya wimbo na shairi. Yeye anadai kuwa ni bahari hizi mbili ambazo hutumika kuelezana mambo ya kimaisha ya kila siku kuliko bahari nyingine. Katika maingiliano yao, Waswahili hupendelea sana kutumia mafumbo ili kueleza mambo yenye aibu na yale yenye kuudhi, yasiyofaa kujulikana na watu ila waliohusika ili wengine wasielewe msemewa ni nani. Kwa ufupi, Waswahili hupendelea sana kutumia mafumbo katika tungo zao na hata katika uzungumzaji wao wa mambo ambayo mila yao haiwaruhusu kuyazugumza kinagaubaga. Mfano wa mambo kama haya yanayonenwa sana kwa mafumbo ni mambo ya maingiliano baina ya wanaume na wanawake na ya mapenzi. Jambo muhimu sana kulielewa katika maswala haya yanayohusiana na tungo za kimafumbo ni kwamba hazina tafsiri moja tuu – ama zisingalikuwa ni tungo za kimafumbo – na kila mmoja ana haki ya kuyapa mafumbo tafsiri aipendayo, mradi tafsiri isivuke mipaka bila ya kiasi.

Moja katika sababu muhimu sana ya kutumia mafumbo katika tungo ni kuwapa watu wasaa wa kutafakari tungo katika bongo zao na kuwapa uwanja wa kubaini maana iliyokuwa mwafaka na maisha yao. Sababu ya kutumia mafumbo katika kueleza mambo yanayohusiana na maingiliano baina ya wanaume na wanawake ni kwamba mila ya Kiswahili haikuwaruhusu Waswahili kuzungumza mambo hayo na kuyaimba waziwazi. Lakini kwa lugha ya kimafumbo, licha ya kuwa Waswahili wanaweza kuzungumza mambo kama hayo, lakini wanaweza pia kutungia nyimbo habari hizo na nyimbo kutiwa mahadhi na kuimbwa hadharani bila ya kuona haya wala aibu. Ni

muhimu kukariri kuwa maana ya tungo za kimafumbo zinategemea fikra za msikilizaji na kila mmoja ana zake.

Mtaalamu huyu pia ameeleza kuwa mafumbo hutumiwa sana katika lugha ya Kiswahili. Sababu kubwa za kutumia mafumbo ni mbili: Kwanza, mafumbo hutumiwa badala ya lugha hiyo wazi wakati mtu anataka kumpiga mwenziwe vijembe. Kumpiga mtu vijembe ni kumwambia maneno ya kimafumbo kwa madhumuni ya kumsema na kumkejeli. Sababu ya mafumbo aina hii kuitwa “vijembe” ni kuwa, mfano wa vijembe, maneno hayo aghalabu huwa yanaweza kukata na kujuruhi hisi za msemewa na watu wake iwapo wameelewa yaliyonenwa.

Sababu nyingine ya kutumia mafumbo ni kueleza kisichofaa kuelezwa kwa lugha iliyo wazi. Katika mila ya Kiswahili mambo yasiyofaa kuelezwa wazi ni mengi. Kwa hivyo, mafumbo katika lugha ya Kiswahili ni mengi pia kulingana na mahitaji ya Waswahili. Kwa kuangazia *Utenzi wa Mwanamanga*, Shariff (keshatajwa) anaeleza kuwa ingawa mafumbo ni nadra sana kutumiwa katika utenzi, anagundua kuwa Fumo Liyongo hakuwa na budi ila kutumia mafumbo alipokuwa amefika katika kusifu maungo ya mkewe ambayo mila yake haikumruhusu kutaja na kueleza waziwazi. Katika kuzungumzia juu ya utupu wa mkewe na kumingilia, alipiga mafumbo ya bahari ya kutweka jahazi na kusafiri nalo na kupiga mzinga.

Mtafiti alifanya mahojiano na wataalamu aliowachagua na aliweza kupata tafsiri mbalimbali za mafumbo aliyotumia Fumo Liyongo katika *Utenzi wa Mwanamanga* ambazo alizichanganua na kuzisawazisha kama ifuatavyo:

Moja wapo ya misingi iliyoongoza utafiti huu ni kwamba nadharia hii inashikilia kwamba uhakiki au fasiri iliyo sahihi inahitaji kukibuni upya anachojaribu kukielewa

mhakiki au mfasiri. Katika kuzingatia msingi huu mtafiti amefaulu kuubuni upya *Utenzi wa Mwanamanga* kama ilivyodhihirika hapo mwanzoni. Msingi mwingine ambao ulimwezesha mtafiti kupata fasiri sahihi ya mafumbo katika *Utenzi wa Mwanamanga* ni ule ambao unashikilia kwamba ubunifu mpya au ufufuaji wa hali halisi ya kazi yoyote unapaswa kufanywa katika viwango viwili maalumu ambavyo ni:

Kwanza: Ufufuaji wa Kisarufi. Katika kiwango hiki kipashio au elementi ya kazi fulani inaeleweka vizuri kwa kutazama kazi inayohusika katika muktadha wa kazi mbalimbali za wakati ilipoandikwa. Kwa mujibu wa mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Kinene wa Mutiso ni kwamba *Utenzi wa Mwanamanga* umeandikwa kwa kutumia sitiari. Mfano mzuri wa mbinu ya mafumbo umejitokeza kuanzia ubeti 41-47 katika utenzi huu.

Ubeti 41.	Na yake safina	nalipoiyona
	Ni nyire si pana	iyaliye nyonga.
Ubeti 42.	K'akunduwa ndume	matanga yakwime
	Haswa la galime	shairaa kasonga.
Ubeti 43.	Kwalina mawingu	na pepo nyengwangu
	Z'ote zombo zangu	kazifunga funga.
Ubeti 44.	K'azungua bao	k'apinga shikio
	Mbwene yavutao	mai henda manga.
Ubeti 45.	Ngamani k'akingiya	ili kutungiya
	K'esa kuzengeya	ngama isikinga.
Ubeti 46.	Ikimikamika	ikinuk'anuk'a
	Vumba la Kimaka	yake Mwanamanga.
Ubeti 47.	K'angiya ngamani	k'enga uziwani
	Niyeyepo p'wani	k'apinga mzinga.

Pili: Ufufuaji wa kisaikolojia. Kinachosisitizwa hapa ni uchunguzi wa usemi wa lugha sambamba na mawazo ya anayetamka ambaye ni mwandishi wa *Utenzi wa Mwanamanga*. Msingi huu unasisitiza uchunguzi wa ‘muktadha mzima’ wa mfumo wa kilugha pamoja na ‘muktadha’ wa karibu wa sentensi. Muktadha unaorejelewa hapa ni muktadha wa ubaharia na katika kipindi cha kihistoria cha kabla ya karne ya 12 ambapo inadaiwa ndicho kipindi alichowahi kuishi Liyongo. Kwa kuzingatia misingi hii miwili tafsiri za maana za msamiati kwa mujibu wa muktadha wa ubaharia na kipindi hicho cha kihistoria cha kabla ya karne ya 12 mtafiti aliweza kupata data kutokana na mahojiano kati yake na walengwa na akafanya uchanganuzi kama ifuatavyo:

Katika utafiti huu tafsiri ya mafumbo katika *Utenzi wa Mwanamanga* imegawanyika katika sehemu mbili:

i. Tafsiri ya maana wazi

Tafsiri hii inalenga kueleza maana ya juujuu inayojitokeza katika beti zenye mafumbo yaliyohimilishwa kwa msamiati wa ubaharia (muktadha wa ubaharia) ambazo ni kuanzia ubeti wa 41-47. Maana wazi inayojitokeza katika beti hizi ni kama ifuatayo:

Ubeti 41. Na yake safina nalipoiyona
 Ni nyire si pana iyaliye nyonga.

Safina yake nilipoiona ni ndefu si pana na imelalia nyonga.

Safina – chombo cha baharini kilichoundwa kwa mbao cha kuchukulia abiria na bidhaa.

Nyonga – kiungo cha mwili ambacho ndicho sehemu inayogawa kiuno na sehemu ya mapaja.

Ubeti 42. K’akunduwa ndume matanga yakwime
 Haswa la galime shairaa kasonga.

Nikakunjua ndume matanga yawe wima haswa la galime tanga likasonga.

Kakunduwa – nikakunjua, *Matanga yakwime* – matanga ya jahazi yasimame.

Ndume/demani – kamba inayotumika kufungia matanga katika jahazi.

Galime – tanga dogo.

Shairaa kasonga – tanga likafunguka.

Ubeti 43. Kwalina mawingu na pepo nyengwangu

 Z’ote zombo zangu kazifungafunga.

Kulikuwa na mawingu na upepo mwanana. Vyote vyombo vyangu nikafungafunga na kupakia.

Kwalina mawingu – kulikuwa na mawingu,

Pepo nyengwangu – upepo mwanana,

Zote – vyote, *zombo* – vyombo.

Ubeti 44. K’azungua bao k’apinga shikio

 Mbwene yavutao mai henda manga.

Nikageuza usukani, nikapinga shikio. Nikaona mawimbi yavutayo maji yanakwenda Manga.

Kazungua – kugeuza, *bao* – usukani, *mbwene* – nikaona, *mai* – maji.

Ubeti 45. Ngamani k’akingiya ili kutungiya

 K’esa kuzengeya ngama isikinga.

Ngamani nikafikia ili kuchungulia. Kisha kuikagua ngama haikuvuja.

Ngamani kakingiya – nikaingia katikati ya jahazi, *kutungiya* – kuchungulia,

Kesa kuzengeya – nikamaliza kukagua.

Ngama isikinga – ngama haikuvuja.

Ubeti 46. Ikimikamika ikinuk’anuk’a
 Vumba la Kimaka yake Mwanamanga.

Iking’aang’aa ikifiridi kwa uvumba wa Kimaka (ngama) yake Mwanamanga.

Ikimikamika – iking’aang’aa, *ikinukanuka* – harufu ya kile chombo, *vumba* - harufu.

Ubeti 47. K’angiya ngamani k’enga uziwani
 Nieyepo p’wani k’apinga mzinga.

Nikaingia ngamani nikaenda baharini. Nilipofika pwani nikapiga mzinga.

K’angia ngamani – nikaingia katikati ya safina, *ngama* - mahali katikati ya chombo cha bahari kama vila jahazi ambapo huwekwa mizigo, *kenga* – nikaenda, *uziwani* – baharini, *niyeyepo* – nilipofika, *kapiga mzinga* – kupiga mzinga. (goma lenye kutengenezwa kwa gogo la mti mfano wa mzinga wa nyuki ambalo hupigwa vigongo na hutoa sauti kubwa na nzito).

ii. **Tafsiri ya maana fiche.**

Tafsiri hii inalenga kueleza maana fiche kwa kufumbua mafumbo yaliyohimilishwa kwa msamiati wa ubaharia (muktadha wa ubaharia) uliotumika katika utenzi.

Ubeti 41. Na yake safina nalipoiyona
 Ni nyire si pana iyaliye nyonga.

Tupu yake mwana huyu nilipoiona ni ndefu na si pana na tena imejaa katikati ya mapaja yake mwanamke huyu.

Safina – ni sitiari ya kiungo chote (uke) cha mwanamke jinsi mnenaji alivyokiona alipoifikia ile sehemu ya peto.

Ubeti 42. K'akunduwa ndume matanga yakwime
 Haswa la galime shairaa kasonga.

Alijitayarisha kwa kitendo cha ngono kwa kumvua mkewe nguo alizokuwa amevaa kisha akamvua pia chupi na akaanza kusiona.

Ubeti 43. Kwalina mawingu na pepo nyengwangu
 Z'ote zombo zangu kazifunga funga.

Anazungumzia mandhari ya pale walipokuwepo (kwenye chombo cha bahari). Kulikuwa na mawingu na upepo mwanana. Mnenaji akajitayarisha kwa kitendo cha ngono (kuvua nguo zake).

Ubeti 44. K'azungua bao k'apinga shikio
 Mbwene yavutao mai henda manga.

Alimgeuza na kumweka yule mwanamke katika hali nzuri ya kuweza kumpokea. Kisha akaiona ile ngama (uke) ina uoevu fulani ambao ulimpa mshawasha wa kumwingia kwa urahisi.

Ubeti 45. Ngamani k'akingiya ili kutungiya
 K'esa kuzengeya ngama isikinga.

Akafikia uke wa mkewe ili kuuangalia. Alipomaliza kukaguaa, uke ule haukuwa na kizuizi chochote. (ulimridhisha). Alitanguliza kitendo cha kumwingilia mkewe. Alitanguliza kuingiza sehemu ya mbele ya tupu yake kwa uke wa mkewe.

Ubeti 46. Ikimikamika ikinuk'anuk'a
 Vumba la Kimaka yake Mwanamanga.

Uke ule ulikuwa unametameta na kutoa harufu nzuri ya kufurahisha ya vumba la Kimaka.

Ubeti 47. K'angiya ngamani k'enga uziwani
 Niyeyepo p'wani k'apinga mzinga.

Mnenaji akaingiza uume wake wote katika uke wa mkewe na kuendelea kufurahia zaidi. Alipofikia kilele cha msisimko (mshindo) alitoa manii.

Nabhany (1996) anaeleza kwamba katika ubeti huu ni kwamba mtunzi ametumia sitiari katika ubeti wote. Kwa mtu asiye mswahili akitafsiri neno mzinga kwa kiingereza litakuwa “cannon” na atalichukulia kuwa Fumo Liyongo kutumia neno hili watamhusisha na kipindi cha Wareno ambapo walitumia ile mizinga ya kivita. Hatajua kuwa neno “mzinga” katika Kiswahili lina maana mbili:

- i. Mzinga wa nyuki. Kulingana na vile mzinga wa nyuki ulivyo kiumbo ulifanana na kile kifaa cha kivita na ndiyo maana wakakiita hicho kifaa mzinga wa nyuki.
- ii. Pwiru, kulokolo au bata mzinga inamaanisha “turkey”. Mnyama huyu alipewa jina hili kwa sababu hujaza kishau chake na hewa halafu hutoa hewa inayotoa sauti iitwayo mzinga ambayo Liyongo alimaanisha kusema katika ubeti wake kuwa, kile kitendo cha kutoa manii ni kama kupuliza kitu ili kitoe sauti ambayo ni mzinga.

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na Prof. Sheikh Ahmed Nabhany alieleza kuwa mzinga katika enzi hizo za zama alizoishi Liyongo lilikuwa ni goma lenye kutengenezwa kwa gogo la mti (mfano wa mzinga wa nyuki) ambalo hupigwa vigongo na hutoa sauti kubwa na nzito. Asili ya mizinga ya baruti na risasi kuitwa jina hilo ilitokana na mzinga huo wa goma. Maneno kupiga mzinga katika *Utenzi wa*

Mwanamanga hayana maana ya mzinga wa kivita. Mzinga wa baruti na risasi na mizinga ya vita imekuja baadaye sana baada ya kifo cha Liyongo. Waswahili wa kale walikuwa wakitumia mzinga huo katika sambo zao kupiga ili kuwajulisha walioko mjini kuwa jahazi lao liko karibu kuwasili bandarini ili wajitayarisha kuwapokea wageni na mali waliyokuja nayo. Waswahili walikuwa wakizitumia zana zingine kama vile makombe ya pwani – dui au duri – badala ya mzinga na hii ndiyo sababu ya pale mahali wanapotemshwa ng’ombe Unguja kuitwa “Mpiga - duri”.

4.3.2.8 Tashihisi

Mbatiah (2001) anafafanua tashihisi kama tamathali ya usemi ambapo kitu kisichokuwa na uhai kinaelezwa au kuzungumziwa kama kwamba ni binadamu. Kulingana na ujuzi wa mtafiti tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo huhusisha kuvipa vitu visivyo hai sifa za kibinadamu. Mbinu hii pia huhusisha kuwapa wanyama tabia kama za binadamu au viungo vya mwili uwezo wa binadamu kama vile kucheka, kushauri, kuogopa na kulia. Tamathali hii ya usemi imejitokeza katika ubeti ufuatao:

Ubeti 50:	Maondo ni swifa	yana maarifa
	Henda kwa miswafa	na kuiviringa.

4.3.2.9 Majazi

Wamitila (2003) anaeleza kwamba wahusika huweza kupewa majina ambayo yana maana fulani. Majina haya yanaweza kuhusiana na tabia zao, maisha yao, matabaka yao, mitazamo yao na elimu yao. Inawezekana pia mwandishi akasawiri mahali au mandhari na kuyapa majina yenye maana fulani. Kulingana na ujuzi wa mtafiti majazi ni mbinu ya kumpa mtu au mahali jina kulingana na umbo au sifa zake. Kimsingi ni majina ya kiistiari kwa sababu yanawakilisha sifa fulani. Majazi ni mbinu muhimu

katika kazi ya fasihi kwani hufumbata maudhui mbalimbali. Majina mengine ya majazi huwa kinyume na tabia ya wahusika na hutumiwa kufanyia tashtiti tabia hasi za wahusika wanaorejelewa katika kazi husika.

Mhusika mkuu katika utenzi huu ni Mwanamanga. Mnenaji ameutaja sana mji wa Manga na kutokana na hilo mnenaji anadokeza kwamba bila shaka mwanamke huyu alikuwa mwenye asili ya Manga. Jina Mwanamanga limeundwa kutokana na maneno mawili ambayo ni Mwana na Manga. Mwana ni neno lionyeshalo heshima unapotaja jina la mwanamke. Manga ni neno linalorejelea mojawapo ya miji ya kale ya Arabuni. Mwanamanga kwa ufupi ni jina moja la Kiarabu linalomrejelea binti wa Kiarabu. Katika utenzi sifa anazopewa Mwanamanga, msanii amezimithilisha na mambo mbalimbali yaliyoko katika mji wa Manga. Haya yanadhihirika katika beti zifuatazo:

Ubeti 20.	Si ya ahadharu Hufana na nuru	si ya ahamaru iwaayo Manga.
Ubeti 31.	Huleta harufu (makwapa) Au matukufu	zaidi ya ufu mafuta ya Manga.
Ubeti 52.	Nyaoze ashashi Kazi ya naqishi	vaole ni koshi ni kazi ya Manga.

Katika beti hizo msanii anasifu meno ya Mwanamanga akidai kuwa si ya rangi ya kijani wala nyekundu bali yanafanana na nuru iwakayo Manga. Anaeleza kuwa makwapa ya Mwanamanga hutoa harufu zaidi ya ufu au mafuta matukufu ya Manga. Viatu anavyovaa mwanamke huyu ni koshi zilizopakishwa na ni kazi ya Manga.

4.4 Ukiushi katika ushairi

Wamitila (2002) amefafanua dhana ya ukiushi katika shairi. Anaeleza kwamba hii ni sehemu ya kile kinachoitwa idhini za kishairi. Je, idhini hii inamruhusu mshairi kufanya nini? Mshairi ana uhuru wa kuzikiuka sifa za lugha ya kawaida. Anaweza kuyaendeleza maneno kwa jinsi tofauti na akautumia msamiati usiokuwa wa kawaida. Uhuru huo unajitokeza katika viwango mbalimbali vya lugha, vya kimaandishi au kitahajia, kisauti au kifonolojia, kisemantiki, kisajili na hata kukiuka kwa awamu za kihistoria.

4.4.1 Ukiushi wa kitahajia au kihijai

Wamitila (keshatajwa) anaeleza kuwa katika ushairi inawezekana maneno yakaendelezwa kwa namna ambayo siyo. Kwa sababu za vina au mizani huenda mshairi akalazimika kuliendeleza neno kwa jinsi tofauti. Anaweza akalifupisha (inkisari) akalirefusha (mazida) au akabadilisha muundo wake (tabdila).

Arege (keshatajwa) anaeleza kuwa mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika utunzi wa shairi. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lizingatie umbo fulani. Uhuru wa mshairi katika *Utenzi wa Mwanamanga* unajitokeza kama ifuatavyo:

Inkisari – Hii ni kunga ya kupunguza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani au vina katika mshororo. Uhuru huu umejitokeza katika *Utenzi wa Mwanamanga* kama ifuatavyo:

Ubeti 9. Kitwache – badala ya kichwa chake.

Ubeti 11. Napa – badala ya naapa.

Ubeti 15. Puwaye – badala pua yake.

Ubeti 18. Helewa – badala ya huelewa.

Ubeti 20.	Hufana – badala ya hufanana.
Ubeti 25.	Shingoye – badala ya shingo yake.
Ubeti 26.	Umbile – badala ya umbo lake.
Ubeti 28.	Zandaze – badala ya zanda zake.
Ubeti 29.	Nyaaze – badala ya nyaa zake.
Ubeti 30.	Makwapaye – badala ya makwapa yake.
Ubeti 43.	Kwalina – badala ya kulikuwa na.
Ubeti 51.	Tafuze – badala ya tafu zake.

Tabdila – ni mbinu ya kubadilisha mundo wa neno kwa kubadilisha silabi ya mwisho ili kutosheleza mtiririko wa vina katika kipande bila kuathiri mizani. Mbinu hii huhusisha kubadilisha matamshi au ulimi na kuyafanya maneno yatamkwe na kuendelezwa tofauti na kawaida. Ufundi huu hata hivyo hutumiwa kwa makini kwa sababu haufai kubadilisha maana ya neno wala idadi ya mizani katika neno. Tabdila imejitokeza katika *Utenzi wa Mwanamanga* kama ifuatavyo:

Ubeti 15.	Puwaye – badala ya puaye.
Ubeti 37.	Ndiya – badala ya ndia.
Ubeti 38.	Puwa – pua.
Ubeti 40.	Duwara – badala ya duara.
Ubeti 45.	K'akingiya – badala ya kakingia.
Ubeti 49.	Ngowa – badala ya ngoa.

4.4.2 Matumizi ya hati za lugha nyinginezo

Arege (keshatajwa) anaeleza kuwa mara nyingi sauti /q/ na /kh/ kutoka lugha ya Kiarabu hutumiwa katika utunzi wa mashairi. Huu ni uhuru wa kutumia hati kutoka lugha nyingine, na ambazo hazipo katika alfabeti ya Kiswahili. *Utenzi wa*

Mwanamanga umedhihirisha matumizi mapana ya hati za lugha ya Kiarabu. Matumizi ya lugha ya Kiarabu katika utenzi huu yamejitokeza katika beti zifuatazo:

	Kiarabu	Kiswahili sanifu
Ubeti 3.	Ahali	ukoo, jamaa
Ubeti 4.	Banati	binti
Ubeti 7.	Tawakifu	kutosha, inatosheleza
	Swifa	sifa
	Tuswanifu	tupange, tubuni
Ubeti 9.	Huramu	kitu cha mviringo
	Ruhamu	kitu cha thamani
Ubeti 14.	Khaswa	haswa
Ubeti 20.	Ahadharu	kijani
	Ahamaru	nyekundu
Ubeti 25.	Sharifu	kubwa
Ubeti 26.	Karima	limekirimiwa
Ubeti 29.	Marijani	kito chekundu
Ubeti 34.	Aqili	akili
Ubeti 51.	Qadiri	kadiri
Ubeti 52.	Naqishi	nakshi

4.4.3 Matumizi ya lahaja na kikale

Malenga anaweza kutumia maneno kutoka lahaja nyingine za Kiswahili au atumie neno la kale lisilotumika kwa maana ile iliyokusudiwa. Maneno ya kale huwa yale yaliyochakaa wala hayatumiki tena katika Kiswahili sanifu. *Utenzi wa Mwanamanga* umedhihirisha matumizi mapana ya lahaja tatu za Kiswahili nazo ni Kipate, Kiamu na Kingozi kama ifuatavyo:

i. Kipate

Kipacha (2003) anaeleza kuwa Kipate ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa maarufu cha Pate kilichopo kaskazini mashariki ya pwani ya Kenya na kiko kaskazini mashariki ya Lamu. Mtaalamu huyu amenukuu beti tano za kwanza za *Utenzi wa Mwanamanga* na kutoa zoezi akiuliza wasomaji wake watambue sifa bainifu za kiisimu za lahaja ya Kipate wakizingatia beti tano za kwanza za *Utenzi wa Mwanamanga*. Lahaja ya Kipate imedhihirika katika Utenzi huu kama ifuatavyo:

	Kipate	Kiswahili sanifu
Ubeti 1.	Pijiani	pigeni
	Jamusi	nyati
Ubeti 2.	Uwambe	unene
Ubeti 3.	Wavuli	waume
	Waye	waje
Ubeti 4.	Wambeja	wanawake
	Baiti	beti
Ubeti 5.	Tupane	tupaze
Ubeti 6.	Kisa	kisha
	Kufana	kufaa
Ubeti 8.	Kitwani	kichwani
Ubeti 9.	Kitwache	kichwa chake
Ubeti 10.	Yatendele	yametenda
Ubeti 11.	Siyaona	sijaona
	Miyanga	mwanga
Ubeti 12.	Nshize	nyusi
	Nta	ncha

Ubeti 14.	Mato	macho
	Hutesha	hufurahisha
	Kiyenga	kuyaangalia
Ubeti 15.	Puwaye	pua yake
	Hisabu	hesabu
	Kuziwanga	kuzihesabu
Ubeti 17.	Zitefute	mashavu
Ubeti 18.	Miyomo	midomo
	Atakapkwamba	atakaponena
Ubeti 19.	Humuengaenga	kumetameta
Ubeti 21.	Wanda	uwanja
Ubeti 23.	Kanwa	kinywa
Ubeti 26.	Uyaliye	imejaa
	Mitulinga	mifupa ya mabega
Ubet 27.	Mafuzi	mabega
Ubeti 28.	Zaandaze	vyanda/vidole vyake
Ubeti 29.	Nyaaze	kucha zake
Ubeti 30.	Mato	macho
Ubeti 35.	Kumsinga	kumkanda
Ubeti 36.	Mele	mbele
	Zilele	zimelala
Ubeti 37.	Ndiya	njia
	Makuto	mikunjo
	Masito	maficho
Ubeti 40.	Dara	kugusa

Ubeti 41.	Nyire	ndefu
Ubeti 42.	Kakunduwa	kakunjua
	Yakwime	yawe wima
Ubeti 44.	Kazungua	kazungusha
	Shikio	usukani
Ubeti 45.	Kutungiya	kuchungulia
Ubeti 47.	Kenga	kenda
Ubeti 48.	Kivuza	kutafuta
Ubeti 49.	Ziweoze	mapaja yake
	Kumzimanga	kumlaani
Ubeti 50.	Maondo	magoti
	Kuiviringisha	kujiviringisha
Ubeti 51.	Tafu	nyama za nyuma ya miguu

ii. Kiamu

Kipacha (keshatajwa) anaeleza kuwa Kiamu ni miongoni mwa lahaja zilizopo katika fungu visiwa vya Lamu. Lahaja hii huongelewa katika kisiwa cha Amu (Lamu) ambacho kiliitwa “Kuwa-ndeo” yaani kisiwa cha majivuno. Jina la Lamu linatokana na jina la kabila moja la Kiarabu “Bami Lami” ambalo limetokea sehemu za ghuba ya Uajemi. Kiisimu Ki-lamu na Ki-pate zinafanana lakini sio kuwa ziko sawa. Lahaja ya Kiamu katika *Utenzi wa Mwanamanga* imedhihirika kama ifuatavyo:

Kiamu	Kiswahili sanifu	
Ubeti 6.	Kisa	kisha
	Zawe	zako
Ubeti 5.	Mbee	mbele

Ubeti 8.	Takwanda	cha kwanza
	Nyee	nywele
Ubeti 11.	Napa	naapa
Ubeti 37.	Ndiya	njia
Ubeti 39.	Yuu	juu
Ubeti 43.	Zombo	vyombo

iii. Kingozi

Kipacha (keshatajwa) anaelezea kuwa dhana ya kuwepo kwa lahaja ya Kingozi ilianza kuonekana mwanzoni katika kazi za Krapf (1882) na Bishop Steere (1919). Krapf alizungumzia kuwepo kwa lahaja iliyokuwa ikizungumzwa sehemu za Malindi na pande nyingine za kaskazini ya ukanda wa Kiswahili. Dhana nyingine ilihusisha Kingozi na lugha bunifu iliyokuwa ikitumiwa na washairi pekee. Askofu Edward Steere naye aligusia kuwepo kwa mashairi ya Kiswahili yanayoandikwa kwa lugha ya kizamani yenye athari ya Kiarabu na maneno kama *umbwene* (nimeona) na *nikomile* (nimekoma). Lahaja ya Kingozi katika *Utenzi wa Mwanamanga* imedhihirika kama ifuatavyo:

	Kingozi	Kiswahili sanifu
Ubeti 4.	Wakeleti	wenyeji, wakaazi
Ubeti 8.	Zakwe	zake
Ubeti 10.	Yakwe	yake
	Yatendele	yametenda
Ubeti 18.	Atakapkwamba	atakaponena
Ubeti 19.	Humuengaenga	humng'aa ng'aa
Ubeti 26.	Mitulinga	mifupa ya mabega

Ubeti 30.	Mbwene	nimeona
	Ukimeza	ukimea
Ubeti 35.	Ziwavuze	mbavu zake
Ubeti 36.	Hazitumbalile	hazikumuka
Ubeti 43.	Kwalina	kulikuwa na
Ubeti 44.	Kuzengeya	kukagua
Ubeti 46.	Ikimikamika	ikimetameta

4.5 Muundo

Kulingana na Arege (keshatajwa) ameangazia muundo au umbo la shairi kama mojawapo ya mambo muhimu yanayoangaziwa wakati wa uchambuzi wa mashairi. Katika kueleza umbo la shairi mhakiki huangalia jinsi shairi lilivyoundwa kwa kuangazia vipengele vifuatavyo:

- Idadi ya beti katika shairi zima.
- Idadi ya mishororo katika kila ubeti.
- Idadi ya vipande katika kila mshororo.
- Idadi ya mizani katika kila mshororo na katika kila kipande cha mshororo.
- Vina jinsi vilivyo katika shairi. Mhakiki anapaswa kuzingatia vina vya kati na vya mwisho kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.
- Hali ya kituo, kiishio au kibwagizo. Lazima mhakiki aeleze ikiwa kimefupishwa, kimerudiwarudiwa au kinabadilika kutoka ubeti hadi ubeti.

Utenzi wa Mwanamanga umedhihirisha muundo ufuatao:

Kama ilivyoielezwa hapo mbeleni, utenzi ni ubeti mmoja wa utungo wa mishororo miwili uliokuwa na vina vitatu; kati na mwisho wa mshororo wa kwanza na kati ya mshororo wa pili. Sauti ya kina cha mwisho huwa nyingine yoyote apendayo mtungaji. Watungaji wengi tokea zama za zama walipendelea sauti moja, iwe kina pia.

Utenzi wa Mwanamanga una beti hamsini na mbili zilizo na muwala na muumano na zinajitosheleza kimaana. Utenzi huu umechukua muundo wa aina ya ushairi wa tathnia kwani kila ubeti una mishororo miwili. Kila ubeti umegawika katika vipande viwili yaani ukwapi na utao na kuufanya utenzi huu kudhihirisha muundo wa bahari ya mathnawi. Katika upande wa mizani kila kipande kina mizani sita hivyo basi mizani katika kila mshororo ni kumi na mbili. Utenzi huu hauna kibwagizo katika kila mshororo wa mwisho wa kila ubeti. Kila ubeti unaishia kwa kimalizio au tamati. Vina katika beti za utenzi huu vinabadilikabadilika kutoka ubeti hadi ubeti isipokuwa kina cha utao wa kila mshororo wa mwisho wa kila ubeti. Beti zote zinaishia kwa kina “nga”. Katika kila ubeti vina vya kipande cha ukwapi cha mshororo wa kwanza na wa pili na kile cha utao wa mshororo wa kwanza vinalingana isipokuwa cha utao wa mshororo wa pili ambacho ni “nga”.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Kitangulizi

Sura hii inahitimisha utafiti huu kwa kuweka bayana malengo na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Sehemu hii imeangazia kudhihirika kwa maudhui katika *Utenzi wa Mwanamanga* ambamo baadhi yake yanahusiana na wanawake na fani mbalimbali zilizojidhihiri. Vilevile, hisia zilizotumiwa na mtunzi katika kumwelezea mhusika wake katika utenzi huu pia zimebainishwa. Aidha, mapendekezo kutokana na utafiti huu yamewasilishwa kwa lengo la kuweka wazi mambo mengine ya kutafitiwa zaidi kwenye *Utenzi wa Mwanamanga*. Matokeo ya utafiti yamemwezesha mtafiti kupima malengo ya utafiti pamwe na maswali ya utafiti huu na kumhakikishia mtafiti kuwa utafiti huu umekamilika kama ilivyokusudiwa.

5.2 Muhtasari wa utafiti

Utafiti huu uliazimia kuchunguza maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Utafiti huu vilevile ulilenga kubainisha hisia zilizotumiwa na mtunzi kwa makusudi katika kumwelezea mhusika wake kwenye utenzi. Tasnifu hii imegawanyika katika sura tano na kila mojawapo imeundwa kwa sehemu zake mbalimbali.

Sura ya kwanza, inahusu usuli wa mada. Mtafiti ametanguliza utafiti huu kwa kuelezea usuli wa mada ya utafiti. Katika sehemu hii mtafiti ametoa maelezo muhimu katika uwanja mpana wa ushairi na kulenga swala hususan la utafiti huu. Katika sehemu hii mtafiti ameeleza kwa kina kuhusu swala la utafiti na jinsi uhitaji wa kuufanya utafiti huu ulivyochipuka. Sehemu hii pia inaeleza kuhusu malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada, na natija ya utafiti huu.

Sura ya pili ya utafiti huu inahusu mapitio ya maandishi na nadharia ya iliyoongoza utafiti huu. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya kihemenitiki iliyoasisiwa na Friedrich Schleiermacher, Wilhelm Dilthey na Martin Heidegger. Sura hii imeonyesha mihimili ya nadharia hii na pia kuonyesha jinsi mihimili ya nadharia hii ilivyoongoza utafiti huu.

Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Katika sura hii mtafiti ameonyesha mpangilio wa utafiti huu, utaratibu wa utafiti, jumua na uteuzi wa sampuli ya utafiti huu, utaratibu wa ukusanyaji data, vifaa ya utafiti, data iliyonuiwa kukusanywa, mbinu za kukusanyia data na jinsi data hiyo ilivyonuiwa kuchanganuliwa.

Sura ya nne inahusu matokeo ya utafiti. Sura hii ndiyo iliyobeba matokeo ya utafiti ambapo imeshughulikia mambo kadhaa yakiwemo: maudhui katika *Utenzi wa Mwanamanga*, vipengee vya fani mbalimbali kwa ujumla kama vile: tamathali za usemi kama vile: tashbihi, mafumbo na taswira, ukiushi katika ushairi, na muundo. Katika sura hii mtafiti pia ameshughulikia swala la hisia zilizotumiwa na mtunzi wa utenzi katika kumwelezea mhusika wake kwenye utenzi. Vilevile tafsiri ya *Utenzi wa Mwanamanga* kwa lahaja ya Kiunguja pamwe na fasiri za baadhi ya maneno zimeonyeshwa kulingana na mwongozo wa nadharia ya kihemenitiki katika sehemu ya viambatisho.

Sura ya tano ndiyo sura ya mwisho ya utafiti huu. Katika sura hii mtafiti ameeleza muhtasari wa utafiti huu, akatoa maelezo kuhusu matokeo ya utafiti kwa kiduchu na ufasiri wa matokeo hayo. Mtafiti pia ametoa mawaidha na mapendekezo kuhusu masuala ambayo yanahitajika kufanyiwa utafiti zaidi katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu umemwezesha mtafiti kutambua kuwa *Utenzi wa Mwanamanga* una maudhui ambayo baadhi yanahusiana na wanawake kama vile: uzuri wa mwanamke, unyumba, nafasi ya mwanamke katika jamii na wasifu wa mwanamke. Utafiti huu umemwelekeza mtafiti kutambua kuwa mtunzi alitumia fani mbalimbali kama vile: tamathali za usemi ili kufanikisha azma yake ya kupitisha ujumbe alionuia kuupitisha. Mtunzi kwa mfano, alitumia mbinu ya mafumbo aliyoihimilisha kwa msamiati wa ubaharia (muktadha wa ubaharia) ili kumsaidia kuzungumza mambo mazito ambapo kulingana na mila ya mtunzi ilikuwa ni mwiko kuyazungumza kwa lugha iliyo wazi. Kutokana na utafiti huu mtafiti amegundua kuwa *Utenzi wa Mwanamanga* ni utenzi ambao unadhihirisha usanii na ufundi wa hali ya juu wa mtunzi kwani katika utenzi huu msanii amefaulu kuziteka hisia zote tano za msomaji. Hisia hizi ni: kuona, kuonja, kunusa, kugusa na kusikia. Msanii alifaulu kwa jambo hili kwa kutumia mbinu ya taswira. Jambo hili linaweza kumfanya msomaji kuweza kusafiri na mtunzi katika safari yake kutoka kichwani hadi kwenye maungo ya mkewe ambapo msanii anatweka jahazi na kusafiri nalo katika safari ya majini kisha kuendelea na safari yake hadi kwenye miguu ya mkewe. Fumo Liyongo alitumia mbinu hii ya kipekee kabisa katika utenzi wa *Utenzi wa Mwanamanga* ili kuhakikisha anwaathiri wateja wake barabara kiasi cha kwamba hawawezi kamwe kuusahau utenzi huo wala mhusika mkuu aliyesababisha kutungwa kwa utenzi wenyewe.

5.4 Kuhusu malengo ya utafiti

Mtunzi Fumo Liyongo ameonyesha ugwiji na kipawa chake katika usanii wa mashairi kwa kujenga na kuendeleza maudhui. Jambo hili limemwezesha mtunzi kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu. Maudhui yaliyochanganuliwa katika *Utenzi wa Mwanamanga* ni kama: mapenzi, ushirikiano katika jamii, utamaduni, dini, usanii wa mashairi, uzuri

wa mwanamke, kuheshimiana, unyumba, ushirikina, nafasi ya mwanamke katika jamii, ubaharia na wasifu. Licha ya kuwa maudhui haya ni ya jadi mno lakini bado yana uamilifu kwani ni muhimu hata katika jamii ya sasa. Maudhui haya yaliyochanganuliwa na mtafiti ni kwamba mtafiti aligundua kuwa yapo baadhi ambayo yanahusiana na wanawake. Baadhi ni kama vile: uzuri wa mwanamke, unyumba, nafasi ya mwanamke katika jamii na wasifu wa mwanamke kwa mtazamo wa mwanamume.

Kulingana na tathmini ya mtafiti ni kwamba utenzi huu umedhihirisha usanii na ufundi wa hali ya juu. Utenzi huu umesheheni vipengee vingi vya fani ambavyo mtunzi amevitumia kindakindaki kama viungo vya kumsaidia kuurutubisha na kuunawirisha utenzi wake ili aweze kuyafikia malengo yake. Msanii ametumia mbinu ya mafumbo na mandhari ya ubaharia kuweza kuzungumzia maungo ya mkewe na kitendo cha kumuingilia mke wake. Ni kutokana na mbinu ya mafumbo ndiposa msanii alifaulu kuueleza ujumbe wake ipasavyo kwani kulingana na utamaduni wake ilikuwa mwiko kuyazungumza maswala ya ngono kwa lugha iliyo wazi. Mtafiti pia aligundua kuwa mtunzi aliamua kutumia aina mbalimbali za taswira kwa makusudi ili kumwezesha kuziteka hisia zote za msomaji. Jambo hili linaufanya utenzi huu kuwa na upekee wa kiufundi wa namna ya kivyake kwani si rahisi kwa msomaji wa utenzi huu kuusahau utenzi huu akisha kuusoma.

5.5 Mapendekezo

Kutokana na utafiti huu ni kwamba swala la maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* ni pana. Katika utenzi huu kuna masuala mengine mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi nayo ni kama vile: historia ya mwandishi wa *Utenzi wa Mwanamanga*, lahaja ya Kipate, Kiamu au ya Kingozi katika *Utenzi wa mwanamanga*, lugha ya Kiarabu katika *Utenzi wa Mwanamanga*, historia ya ushairi

jadi katika fasihi ya Kiswahili na nafasi ya utenzi huu katika historia ya ushairi wa fasihi ya Kiswahili. Kutokana na haya ni kwamba tafiti zingine za *Utenzi wa Mwanamanga* zitakazofanywa zitakuwa hazina kubwa katika ushairi wa Kiswahili kwa ujumla. Aidha kutokana na utafiti huu maudhui na fani katika utenzi huu yameweza kubainika. Pia utafiti huu umeweza kumsaidia mtafiti kugundua kuwa utenzi huu una ufundi wa hali ya juu kwani msanii ameweza kuzitumia hisia zote za binadamu katika kumwelezea mhusika wake kwenye utenzi.

Utafiti huu umeweza kuliziba pengo lililokuwepo katika fasihi ya Kiswahili, la kutokuwepo kwa utafiti wowote wa kitaaluma wa uhakiki wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* kwa mtazamo wa nadharia ya kihemenitiki.

Mwisho ni kwamba zipo tenzi nyingi mno Uswahilini ambazo bado hazijafanyiwa utafiti kwa mtazamo wa nadharia ya kihemenitiki. Nadharia ya kihemenitiki ni nyenzo muhimu ya kufanikisha tafiti zitakazofuata kwani huweza kuhusisha kipengele cha kihistoria ili kuelekeza kupata ujumbe ulionuiwa. Ni muhimu kwa tafiti hizi kufanywa ili kukuza na kuendeleza zaidi ushairi wa Kiswahili na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla.

MAREJELEO

Achieng, (2012). *Sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

(Haijachapishwa).

Arege, T. (2013). *Tunu ya ushairi*. Nairobi: Oxford University Press.

Chimerah, R. (2013). *Siri sirini: Mshairi na mfungwa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Chimerah, R. (2011). *Kiswahili research and development in Eastern Africa*. Mombasa: Jor's Publishers.

Coombes, H. (1953). *Literature and criticism*. Australia: Chatto and Windus.

Dilthey, W. (1996). *Hermeneutics and the study of history (Vol. IV)*. (e - book).

(H.P. Rickman, trans). Retrieved from [http://www.amazon.com/Wilhelm-Dilthey- Selected-Hermeneutics History/dp/0691149313](http://www.amazon.com/Wilhelm-Dilthey-Selected-Hermeneutics-History/dp/0691149313) accessed on 16th August 2018.

El-Maawy, A. A. A. (2011). *Jawabu la Mwanakupona*. Dar es Salaam: Taasisi ya taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Gadamer, H. G. (Ed). (2004). *Truth and method* (3rd ed.). (D.G Marshall & J. Weinsheimer,trans)(e-book).Retrieved from [https://www.amazon.com/method-Continuum-impact- Hans-George-Gadamer/dp108267697X](https://www.amazon.com/method-Continuum-impact-Hans-George-Gadamer/dp108267697X) accessed on 17 August 2018.

Gerard, A. (1981). *African language literatures: An introduction to the literary history of Sub-Saharan Africa*. London: Burnt Mill Harlow.

Harries, L. (1962). *Swahili poetry*. Oxford: O.U.P.

Heidegger, M. (1926). *Being and time*. (Macquarrie & E. Robinson, trans) (e - book).

Retrieved from <http://pdf-objects.com/files/Heidegger-Martin-Being-and-Time-trans-Macquarrie-Robinson-Blackwell-19...> accessed on 20th August 2018.

Kasomo, D. (2006). *Research methods in humanities and education: Research, statistics, measurement, evaluation and testing*. Eldoret: Zapf Chancery.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Kinondoni: Chuo Kikuu huria cha Tanzania.

Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili poetry: An investigation into the concepts of East African Islam as reflected in the utenzi literature*. Leiden: E.J. Brill.

Knappert, J. (1979). *Four centuries of Swahili verse*. London: Heinemann.

Kombo, D. K and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Makuyu: Paulines Publications Africa.

Krapf, J. L. (1882). *A dictionary of the Suahili language* (e - book). Retrieved from <https://archive.org/details/adictionarysuahookrapgoog> accessed on 31st of August 2018.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mberia, K. (1989). Fumo Liyongo. *Mulika*, 21, 25-43.

Mbuvi, K. F. (2013). *Mwongozo wa kidagaa kimemwozea*, Nairobi: Target Publication Limited.

Mlamali, M. (1980). *Inkishafi: Ikisiri ya Muhamadi wa Mlamali*. Nairobi: Longman.

Mohamed, S. A. (1977). *Misemo, milio na tashbihi*. Nairobi: Longman Kenya Limited.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu alipofufuka*. Nairobi: J. K. Foundation.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. Nairobi: English Press Ltd.

Mukuthuria, M. (2007). *Upekee wa Utenzi wa Swifa ya Nguvumali: Utenzi wa mpito, mseto wa imani za jadi na usasa*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
(Haijachapishwa)

Mulokozi, M. M na Sengo, T. S. Y. (1995). *History of Kiswahili poetry, A.D. 1000-2000*: Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi M. M. (1999). *Tenzi tatu za kale (Fumo Liyongo, Al-Inkishafi, Mwanakupona)*. Dar es Salaam: TUKI.

- Mungai, P. (2005). “*Ulinganishi wa kifani wa tenzi za Swifa ya Nguvumali na Mikidadi na Mayasa*” Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Mutiso, K. (1985). *Hurafa na uyaikinifu katika utenzi wa Hamziya*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Nabhany, A. S. (1996). *A Social history of northern Swahili people based on oral evidence*. <https://www.swahilipoetry.humnet.ucla.edu/wp-co...> accessed on 14th November 2017.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi, nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Owallah, K. O. (2011). *Uhakiki wa maudhui na fani katika utenzi wa Nabii Isa*, Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Peck, J na Coyle, M. (1984). *Literary terms and criticism*. London: Macmillan Edn Ltd.
- Ricour, P. (2003). *The Rule of Metaphors: The creation of meaning in language psychology*. (R. Czerny, K. McLaughin & J.S Costello, trans) (e - book). Retrieved from accessed on 30th August 2018.
- Ridhiwani, P. (1997). *Shairi la Fumo Liyongo*. Kiswahili jz, 59, 22-32.

Saussure, F. de. (1959). *Course in general linguistics*. (C.Bally, A. Reideinger & W.

Baskin,trans)(e-book). Retrieved from

https://openlibrary.org/books/OL23291521M/Course_in_ggeneral_linguistics.

accessed on 12th of August 2018.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo zetu: Msingi na mashairi na tungo nyinginezo*. Trenton:

The Red Sea Press.

Shiteni, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili kabla ya karne ya ishirini*. Eldoret: Moi

University Press.

Swaleh, A. (1992). “*Maudhui katika Utenzi wa Mwanakupona*”. Tasnifu ya uzamili,

Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Szondi, P. (1995). *Introduction to literary hermeneutics*. (Martha Woodmansee, trans)

Cambridge: Press Syndicate of the University of Cambridge.

Roy, M. (2013). *Swahili poetry of expression of the 16th-20th centuries: Examples and*

French translations.

[https://www.academia.edu/16042356/Po%C3%A9sie_d_expression_swahilie_d_u_XVI%C3%A8me_au_XX%C3%A8me_si%C3%A8cle_exemples_et_traducti](https://www.academia.edu/16042356/Po%C3%A9sie_d_expression_swahilie_d_u_XVI%C3%A8me_au_XX%C3%A8me_si%C3%A8cle_exemples_et_traduction_fran%C3%A7aise)

[on_fran%C3%A7aise](https://www.academia.edu/16042356/Po%C3%A9sie_d_expression_swahilie_d_u_XVI%C3%A8me_au_XX%C3%A8me_si%C3%A8cle_exemples_et_traducti), accessed on 10th November, 2017.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kautitu Limited.

Schleiermacher, F. (1998). *Hermeneutics and criticism and other writings*. (A. Bowie, trans) e - book) Retrieved from <https://www.amazon.com/Schleiermacher-Hermeneutics-Criticism-Cambridge-Philosophy/dp/0521598489>. accessed 31st of August 2018.

Steere, E. (1919). *A Handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar* (e – book) Retrieved from <http://archive.org/details/handbookofswahilioostee> accessed on 31st of August 2018.

Taylor, W. E. (1915). “*Inkishafi or Swahili speculum Mundi*” in Stigand C.H. *A Grammar of dialect changes in the Kiswahili language*, Cambridge: Cambridge University Press.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi. Misingi na vipengee vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi*. Nairobi: English Press.

VIAMBATISHO

Kiambatisho cha 1: Mwongozo wa majadiliano na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili

1. Taja na ueleze sifa za kipekee za *Utenzi wa Mwanamanga* ukilinganishwa na tenzi zingine za kale katika fasihi ya Kiswahili.

.....

.....

.....

.....

.....

Ni maudhui gani yanayodhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga*?

.....

.....

.....

.....

.....

Fafanua vipengee vya fani vinavyodhihirika katika *Utenzi wa Mwanamanga*?

.....

.....

.....

.....

Bainisha hisia ambazo mtunzi amezitumia katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Fumbua mafumbo aliyotumia msanii katika utenzi wake katika ubeti wa 41 hadi ubeti 47.

.....

.....

.....

.....

.....

Fafanua maana wazi na fiche za mafumbo yaliyohimiliwa kwa msamiati ufuatao wa ubaharia jinsi ulivyotumika katika *Utenzi wa Mwanamanga*.

- i. Safina.....
- ii. Ndume.....
- iii. Matanga yakwime.....
- iv. Galime.....
- v. Shairaa.....
- vi. Pepo nyengwangu.....
- vii. Bao.....
- viii. Shikio.....
- ix. Mbwene yavutao.....
- x. Ngamani.....

**Kiambatisho cha 2: Tafsiri ya
Kiunguja ya Utenzi wa Mwanamanga**

- | | |
|---|---|
| <p>1. Pijiani basi p'embe ya jamusi
Kwa cha mtutusi au mwanananga.</p> | <p>Nipigieni marafiki pembe ya nyati
Kwa kijiti cha mtutusi au mwanananga.</p> |
| <p>2. Pijiani p'embe iliayo yumbe
Mwangi uwambe kwa ya ndovu kanga.</p> | <p>Upige na pembe iliayo bunge
Mwangi unene kama upembe wa ndovu
mchanga.</p> |
| <p>3. Vumi lende mbali lamshe ahali
Wake na wavuli waye ng'ang'ang'ang'a.</p> | <p>Uvumi uende mbali uwaamshe jamaa
Wanawake na wanaume waje haraka
haraka.</p> |
| <p>4. Waye wakeleti wambeja banati
Watupe baiti wamsifu yanga.</p> | <p>Waje wakae chini wasichana
wanaoheshimiwa wakariri beti za
kumsifia Yanga. (Mwanamanga)</p> |
| <p>5. Tupane baiti tukizitafiti
Njema ziwe kiti mbee tukitenga.</p> | <p>Tukariri beti tukizichagua
Zile njema tuzitenganishe na zile mbaya.</p> |
| <p>6. Kisa kuziona baiti kufana
Yatupe kunena zake mwana manga.</p> | <p>Baada ya kuzikariri na kuona zinafaa
Zitupe ya kunena kumhusu
mwanamanga.</p> |
| <p>7. Basi t'awakifu yasiwe marefu
Swifa tuswanifu zake mwana Manga.</p> | <p>Basi tumalizie hapa bila kurefusha huu
utangulizi urembo tuusifu wake
Mwanamanga.</p> |
| <p>8. T'akwanda kitwani nduza
sikiyani hariri laini zakwe nyee singa.</p> | <p>Nitaanzia kichwani ndugu zangu sikieni
Ni Hariri laini nywele zake za singa.</p> |
| <p>9. Kitwache huramu ni kama
ruhamu Enga jaizimu taole kuzinga.</p> | <p>Kichwa chake mviringo ni kama ruhamu
Tazama jaizimu tao lake ni la mviringo.</p> |
| <p>10. Yakwe masikio apulikiyao
Yatendele tao kama kombe nanga.</p> | <p>Yake masikio asikiziayo yametenda
umbo la duara kama kombe la nazi.</p> |
| <p>11. Uso wake napa siyaona
Utengee sana nakuta miyanga.</p> | <p>Uso wake mwana huyu naapa sijaona
umetengea mno na unatoa mwanga.</p> |
| <p>12. Nshize zifene n'ta zilingane
Shina lifungene kama lalofungwa.</p> | <p>Nyusi zake zimefanywa vema ncha zake
zimelingana sawa. Mashina yamefungwa
kama yaliyofungwa.</p> |
| <p>13. Ni nyeusi mno zizidiye wino
Zitolee k'ono tandu za mnga.</p> | <p>Ni nyeusi mno zaidi ya wino
Zimetwalia umbo la matanzu ya mnga.</p> |

14. Mato avikapo haswa avumapo
Mtu akiwapo hutesha kiyenga.

15. Puwaye ajabu zifungo huribu
Ni sita hisabu mwenye kuziwanga.

16. Sitaajabuni kuliko Manani
Hata ishirini zifungo hupanga.

17. Zakwe zitefute zizidiye zote
Ya mk'atekate mafuta ya kwenga.

18. Miyomo myembamba
asipoifumba. Atakapokwamba helewa
muyinga.

19. K'amba takwambaye!
T'atongowa iye! Ajabu menoye
humuengaenga.

20. Si ya ahadharu si ya ahamaru
Hufana na nuru iwaayo Manga.

21. Si ya mkakasi si rangi nyeusi
Ni kufana basi kwa wanda wa Manga.

22. Ulimi mpesi wakase wakase
fenusi Khaswa kidurusi hudighamu
yanga.

23. Kanwa kiradidi nyoshi za mkadi
Au za zabadi ya ngawa na fungu.

24. Shani ni kidevu si k'ungu piyavu
Ni kungu tekevu k'ungu kungumanga.

25. Shingoye ndefu muwandi sharifu
Ipambiwe kufu kama za kutunga.

26. Ni hidaya njema umbile karima
Uyaliye nyama yake mitulinga

Macho afumbapo haswa ayafumbuapo
Mtu akiwa hapo akimuona hufurahia
kuyaangalia.

Pua yake ajabu vipini vimepangika
Hesabu yake ni sita mtu akivihesabu.

Msistaajabu yote Mola amefanya
Hata ishirini vipini vyaweza kupangika.

Yake mashavu ni mazuri zaidi ya yote
Ni ya ufuta mafuta yaliyosafishwa sana.

Midomo yake myembamba asipoifumba
Atakaponena hata mjinga huelewa.

Nikisema nitakwambiaje nitatamka
namna gani. Ajabu meno yake mazuri na
hung'aang'aa.

Hayana rangi ya kijani wala si mekundu
Yafanana na mwanga ung'aao katika
Manga.

Meno yake si (marefu) kama mkakasi
wala si meusi. Bali ni ya kufanana na
kuwa kama uwanja wa Manga.

Ulimi mwepesi ni kama fanusi na hata
akisema neno hurudishwa angani kama
mwangwi.

Kinywa charudisha mivuke ya mkadi
Au zabadi ya ngawa na fungu.

Cha ajabu ni kidevu si kungu iliyokomaa
ni kungu iliyo changa kungu
kungumanga.

Shingo yake ni ndefu, kama mwanzi
mkubwa nayo imepambwa mikufu
iliyotungwa.

Ni zawadi, Mungu karimu ameumba
imejaa nyama mifupa yake ya mabega.

27. Mafuzi kadiri hayakudhihiri
Kama bilauri taole kuzinga.
28. Mikono imiye mbinu zialiyeye
Zandaze ni ziye za t'andu za mnga.
29. Nyaaze launi kama marijani
Napa hutamani mwenye kuziwenga.
30. Makapwaye nduza mato kituliza
Mbwene ukimeza mti mpakanga.
31. Huleta harufu zaidi ya ufu
Au matukufu mafuta ya Manga.
32. Naapa Wallahi asiyeshabihi
Tanena swahihi ya makomamanga.
33. Napa siwenepo zishuhudiyepo
Matunda ya p'epo yake mwanamanga.
34. Yakiwa nguwoni hutisha 'uyuni
Yawapo bayani akili hutanga.
35. Ziwavuze zana ziwavuze nana
Hutisha kuvina mwenye kumsinga.
36. Maungo ya mele sarara zilele
Hazitumbalile hazikumpinga.
37. Matumbo makuto ndiya ya
masito. Kitovu ni kito huvuta kafunga.
38. Kitovu ni kuka kezo la Kimaka
Mwenye kumnuka pua damu yenga.
39. Tawangu ni nzito kwa yuu la
peto. Tena lina k'eto pesi la kuzinga.
- Mabega si makubwa si madogo
hayajatokeza ni kama bilauri tao lake
ukiliangalia.
- Mikono yake yaning'inia na mbinu
zimenyooka. Vidole vyake ni virefu
kama matanzu ya mnga.
- Kucha zake zina rangi kama marijani, na
anayezitazama hupendelea aendelee.
- Makwapaye ndugu zangu mtu akitazama
ataona ukimea mche wa mpakanga.
- Huchochea harufu zaidi ya ufu au
asumini au mafuta matukufu ya Manga.
- Naapa kwa Allah asiye na mshabaha
wake au aliye mfano wake. Nitasema
ukweli habari ya makomamanga. 'Matiti'
- Naapa sikuona wala sikushuhudia
popote matunda ya peponi kama yake
mwanamanga.
- Yakifunikwa nguo hutisha macho na
yakibainika wazi akili hutanga
(hupotea).
- Mbavu zake mwana huyu ni laini
huogopa kuzipapasa mwenye kumkanda
kwani huonyesha dalili ya kuvunjika.
- Mgongo hautokezi sarara zimelala
hazijatokeza wala hazimzuii.
- Tumbo lina mikunjo njia ya maficho
kitovu ni kito na huvutia mtu kukifunika.
- Kitovu ni kuka kerezo la Kimaka
mwenye kumnusa pua yake huwa na
uchepechepe wa damu.
- Tawangu ni nzito kwa kuwa limejaa vito
na lina kina na ni jepesi la miviringo.

40. Wema wa duara angalia dira
Usipoidara yendapo kuzinga.

41. Na yake safina nalipoiyona
Ni nyire si pana iyaliye nyonga.

42. K'akunduwa ndume matanga
yakwime. Haswa la galime shairaa
kasonga.

43. Kwalina mawingu na pepo
nyengwangu. Zote zombo zangu
kazifungafunga.

44. Kazungua bao kapinga shikio
Mbwene yavutao mai henda Manga.

45. Ngamani k'akingiya ili
kutungiya. K'esa kuzengeya ngama
isikinga.

46. Ikimikamika ikinukanuka
Vumba la kimaka yake mwanamanga.

47. Kangiya ngamani kenga uziwani
Niyeyepo pwani kapinga mzinga.

48. Niinushepo kafanya kitapo
K'asabibu papo kivuza waganga.

49. Ziweoze ndiya ni tako la siwa
Watu hula ngowa na kumzimanga.

50. Maondo ni swifa yana maarifa
Henda kwa miswafa na kuiviringa.

51. Tafuze qadiri kowa la zumari
Hazikudhihiri taole kuzinga.

52. Nyaoze ashashi vaole ni koshi
Kazi ya naqishi ni kazi ya Manga.

Makalio yake ni ya mviringo kama dira
bila kuigusa huzunguka na kuzunguka.

Safina yale nilipoiona ni ndefu si pana
bali imejaa katikati ya mapaja.

Nikakunjua demani matanga yawe wima
haswa lile dogo na tanga likasonga

Kulikuwa na mawingu na upepo
mwananana vyote vyombo vyangu
nikapakia vyema.

Nikazungusha usukani nikapinga shikio
nikaona maji yanayovuta yanaelekea
manga.

Nikaenda kwenye ngama ili kuchungulia
na kisha kuikagua ngama haikuvuja.

Iking'aang'aa ikinukanuka vumba la
Kimaka (ngama) yake Mwanamanga.

Nikaingia ngamani nikaenda baharini
nilipofika pwani nikapiga mzinga.

Nilipoinuka nikawa nikifanya kama
mwenye pepo. Nikatafuta waganga.

Mapaja yake ni kama tako la siwa.
Wenziwe hutamani na kuona wivu na
kumalaani.

Magoti yake yanapendeza na yana
maarifa anapotembea. Huenda kwa safu
ya kujiviringisha kwa madaha.

Tafu zake ni kadiri kama kowa la
zumari. Hazijadhihirika sana na umbo
lake ni la mviringo ukilitazama.

Nyayo ni nzuri ajabu. Vazi la nyayo
zake ni koshi. Kazi ya nakshi kazi ya
Manga.

Kiambatisho cha 4: Muundo wa Utenzi wa Mwanamanga

Ubeti	Sehemu	Sifa/ujumbe
1-7	Utangulizi	-Kumtayarisha msomaji kuingia katika ulimwengu wa ubunifu. -Mtunzi anaita jamii imsaidie kutunga beti za kumsifia mkewe.
8-24	Kichwa	Safari ya kusifu maumbile ya mwili kuanzia kichwani Ni cha mviringo.
	Nywele	Hariri.
	Masikio	Ni ya mviringo.
	Uso	Uliotengenea na kutoa mianga.
	Nyusi	Nyeusi zaidi ya wino.
	Macho	Yafurahishayo kuangalia.
	Meno	Si ya kijani si mekundu bali hung'aang'aa.
	Ulimi	Mwepesi wa kukariri vyema.
	Midomo	Myembamba na akizungumza hata mjinga huelewa.
	Pua	Ndefu yenye vivungu.
	Mashavu	Yenye mafuta ya kwenga.
	Kinywa	Chatoa harufu za mkadi.
	Kidevu	Cha mduara kama kungu.
25-30	Shingo	Ndefu iliyopambwa kwa mikufu ya kutunga.
	Mabega	Yaliyojaa nyama, yamelingana vyema na kufanya mduara.
	Mikono	Imening'inia vyema.
	Vyanda	Vipo kama vitanzu vya mnga.
	Kucha	Zatoa rangi kama ya marijani na anayezitamza huzitamani.
	Makwapa	Yatoa harufu nzuri kama ya ufu.
	Matiti	Hajapata kuyaona kama hayo na yawapo bayani akili hupotea.
	Mbavu	Laini na hutisha kuvina mwenye kumkanda.
	Matumbo	Yenye njia ya maficho.
	Kitovu	Mtu akikibusu damu puani humchemka.
	Tawangu	Nzito lenye keto na la mduara.
41-48	Safina	Safari ya majini/kuelezea tendo la ndoa kisitiari Safina ni ndefu na si pana na imejaa kwenye nyonga. Mtunzi anaanza kwa kutayarisha safina yake kwa safari: Anakunjua ndume ili matanga yawe wima. Mandhari ni ya baharini, kuna mawingu na pepo za kuvuma kwa ulaini. Pale chomboni mtunzi anazungua bao na kuona maji yanakwenda manga. Anaingia ngamani ili kuchungulia na baada ya kuikagua ngama haikuvuja. Iking'aang'aa ikinukanuka vumba la Kimaka. Akaingia ngamani na akaenda baharini, alisafiri hadi alipofika pwani kisha akapiga mzinga. Alipoinuka alikuwa akitetemeka kama aliyepandwa na pepo. Alitulia hapo akatafutiwa waganga.

Ubeti	Sehemu	Sifa/ujumbe
49-52	Mapaja	Mwendelezo wa safari ya kusifu maumbile Ni kama tako la siwa na wenzake hutamani na kumwonea wivu.
	Magoti	Yanapendeza na yana maarifa anapotembea huenda kwa safu ya kujiviringisha.
	Tafu	Kadiri kama kowa la zumari, hazijadhihirika sana na za umbo la mviringo ukizitazama.
	Nyayo	Ni nzuri ajabu, vazi la nyayo zake ni koshi (kiatu cha kuvika kanda). Koshi hizo ni kazi ya nakshi, kazi ya Manga.

Kiambatisho cha 5: Fomu ya idhini

IDHINI YA KIMAADILI YA KUFANYA UTAFITI

Anwani: Uhakiki wa Maudhui na Fani katika *Utenzi wa Mwanamanga* utunzi wake Fumo Liyongo.

SEHEMU YA A: UTANGULIZI.

Madhumuni ya waraka huu ni kukualika kuchangia katika utafiti kuhusu uhakiki wa maudhui na fani katika *Utenzi wa Mwanamanga*. Utafiti huu unanuiwa kufanyika katika mkoa wa Pwani hususan maeneo ya Mombasa, Kilifi na Amu. Hii ni kwa sababu mtafiti amefanya uteuzi wa kimakusudi ambapo amewateuwa wataalamu watano ili kuwahoji ambao wanapatikana katika maeneo yaliyotajwa. Bw. Henry M. Mwasafu ambaye ni mwanafunzi wa uzamili katika Chuo Kikuu cha Pwani katika idara ya Lugha, Isimu na Fasihi ataendesha utafiti huu. Mshiriki anapokubali kuchangia katika utafiti huu atahitajika kushiriki katika mahojiano ya ana kwa ana na mtafiti. Mshiriki ana uhuru wa kutojibu maswali ambayo hana majibu yake. Watakaoshiriki katika zoezi hili ni wale wateule waliojitolea kwa hiari yao. Tunawahakikishia watakaoshiriki katika zoezi hili kuwa, habari tutakazokusanya kutoka kwao katika zoezi zima zitahifadhiwa vyema na zitatumika kwa madhumuni ya utafiti huu pekee. Pendekezo la utafiti huu limekaguliwa na kuidhinishwa na bodi ya maadili na ubora ya Zutafindaki ya Pwani ambayo inahusika na maswala ya utafiti. Pia inajihusisha na kuhakikisha haki za wanaoshirikishwa katika utafiti zimelindwa kwa njia zote. Kwa maelezo na marejeleo zaidi wasiliana na:

Henry M. Mwasafu,

Nambari ya simutamba: 0729805190.

Barua pepe – henrymwalugha@gmail.com.

SEHEMU YA B: CHETI CHA KUKUBALI

Mimi Prof/Dkt/Pst/Bw/Bi.....nimepata fursa ya kuuliza maswali muhimu kuhusiana na utafiti huu. Pia nimesoma kwa ukamilifu maswali yanayonuiwa kuulizwa na mtafiti na kuyaelewa. Kwa hivyo, ningependa kuwa mshiriki katika utafiti huu.

Sahihi..... Tarehe

Ungamo la mtafiti

Kulingana na uwezo wangu, nimemsomea mshiriki mtarajiwa maswali na habari zote muhimu zinazohusu utafiti huu. Nimemweleza kwa kina kwamba maswala yafuatayo yatatekelezwa:

- Kushiriki ana kwa ana kwa mahojiano.
- Kumsaidia mtafiti kikamilifu ili kupata majibu ya maswali yote aliyonua kuyauliza.

Ninaungama pia kuwa mshiriki hajashinikizwa wala kuhongwa ili akubali kushiriki katika zoezi hili na kwamba amejiamulia na kujitolea mwenyewe.

Sahihi..... Tarehe

*+